

**ATHARI ZA KIFONOLOJIA KWA WASEMAJI WA DHULUO WANAOJIFUNZA  
KISWAHILI**

**MUDHUNE DENIS RADING'**

**AM12/0629/02**

**EGERTON UNIVERSITY LIBRARY**

**Tasnifu hii Imewasilishwa ili Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya  
Uzamili Katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Egerton**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON - KENYA**

2008

X



Eger233902

89888/16002

X

# UNGAMO NA IDHINI

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya digrii katika Chuo Kikuu chochote.



**MUDHUNE DENIS RADING**

25/09/08

**TAREHE**

## IDHINI

Tasnifu hii imetolewa ili kutahiniwa kwa ushauri wetu na idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na chuo kikuu cha Egerton.



**PROF. F.O ASWANI BULIBA**

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi,  
Chuo Kikuu cha Egerton

25/09/2008

**TAREHE**



**DKT. KIMANI NJOROGE**

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi,  
Chuo Kikuu cha Egerton

26/09/08

**TAREHE**

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa babangu, Nicholas Mudhune Kodida na mamangu Roseline C. Mudhune ambao walinipa motisha na msukumo; kwanza, kwa kutoa chochote walichokuwa nacho kunielimisha; pili kwa kunitia shime masomoni, hadi kuu aliza kazi; na mke wangu Grace Mudhune, ambaye alinifariji wakati wa kuandika tasnifu hii.

## HATILINZI

© MUDHUNE DENIS RADING'

Hairuhusiwi kutoleshwa, kuhifadhiwa au kurekodi tasnifu hiã kwa mfano wowote ule bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

## SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani nyingi kwa wote waliochangia kwa njia mbalimbali ili kufaulisha uandishi wa tasnifu hii. Kwanza kabisa kwa wasimamizi wangu Prof. F. O.

Aswani Buliba na Dkt. Kimani wa Njoroge kwa ushauri na mwongozo walionipa tangu mwanzo hadi mwisho wa kazi yangu. Bila maongozi, maelekezo na ushauri wao mwema kuhusu mada hii, kazi hii haingefikia kiwango hiki cha ufanisi. Ukarimu, uangavu na uwajibikaji wao ulinifaa sana.

Pili, ningependa kuwashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton. Mbali na usaidizi mwingi, walinitia shime na hamasa kwa kuchangia vilivyo, hasa, wakati wa kozi na kuandika pendekezo la utafiti wangu. Miongoni mwa wahadhiri hawa ni aliyekuwa mwenyekiti wa idara Dkt. C. Kitetu; wengine ni Dkt. K. Beja, Dkt. Chai, Bw. Gwachi Mayaka, Bw. Muindi na Bw. Siteti wa Ngero.

Ningependa shukrani nyingine ziwaendee walimu na wanafunzi wa shule za msingi za Ulumbi, Yala Mjini, Jina, Nyamninia na Muhanda kwa kushiriki na kuchangia kazi hii Utafiti wangu usingefanikiwa bila mchango wao

Vilevile, ningependa kuwashukuru wazamili wenzangu – J. Ontieri, G. Ongaki, E. Ongau, P. Ngethe, S. Ngugi, C. Nyandiba, S. Kimani na V. Wangare kwa mijadala ya kiusomi tuliyokuwa nayo, ambayo ilituelekeza ipasavyo katika ulimwengu wa usomi na utaalamu. Sina budi kuwashukuru kwa dhati wasomi wa lugha ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu – Evaline Mudhune miongoni mwa wengine, walionipa muda wao kwa kunisikiliza, kutoa maoni yao na kujibu maswali yangu kuhusiana na mada niliyoiandika katika tasnifu hii.

Katu sitawasahau mke wangu Bi. Grace .A. Mudhune na wanangu Maurice na Shaleen ambao waliniliwaza wakati wa kuandika tasnifu hii.

Mungu awabariki wote.

## IKISIRI

Ripoti za Baraza la Mitihani ya Kitaifa la Kenya (1989 – 2004) zimekuwa zikionyesha kuwa somo la Kiswahili hufanywa vibaya katika mawango vya shule za msingi na sekondari. Matokeo hayo mabaya hutokana na makosa ya hijai, uakifishaji, msamiati miongoni mwa mengine. Wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wilayani Siaya wamekuwa wakipata shida kujifunza lugha ya Kiswahili. Ingawa tatizo hili limekuwa sugu tangu lugha ya Kiswahili kufanywa somo la lazima katika shule za msingi na upili katika mfumo wa 8-4-4, hakuna utafiti wa kina uliowahi kufanywa kubainisha sababu za kifonolojia zinazosababisha ugumu wa kujifunza lugha ya Kiswahili na kutoa mapendekezo ya kutatua tatizo hili. Kwa hivyo utafiti huu ulikuwa jaribio la kuchunguza athari za kifonolojia ambazo hupelekea kutokuwepo kwa matumizi mwafaka ya Kiswahili na wasemaji wa Dholuo. Utafiti huu ulifanyiwa katika tarafa ya Gem Wilaya ya Siaya Mkoa wa Nyanza – Kenya. Tatizo kubwa la matumizi mwafaka ya lugha katika ngazi ya fonolojia ndilo lililokuwa kiini cha utafiti huu. Madhumuni ya utafiti yalikuwa ni kuchunguza iwapo lugha ya Dholuo huathiri Kiswahili kifonolojia, ikiwa ni pamoja na kutolea athari hizi maelezo ya kiisimu. Tulibainisha na kutambulisha vitamkwa vinavyotatiza wasemaji wazawa wa lugha ya Dholuo wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Kisha tulichunguza tofauti za kifonolojia baina ya Dholuo na Kiswahili na jinsi zinavyoathiri wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Kazi hii, pia, ilichunguza na kueleza athari za matamshi mabaya katika maandishi (tahajia). Tulikusanya data kutoka shule tano za msingi wilayani Siaya tarafa ya Gem. Data hiyo ilikusanywa kutokana na masimulizi ya hadithi fupi yaliyonaswa kwenye vinaso sauti kisha kufanyiwa uchanganuzi. Makosa yao ya kimatamshi yalibainishwa na kuainishwa ili kuthibitisha ukuruba uliopo kati ya matamshi na makosa ya hijai. Watafitiwa pia walipewa mazoezi ya imla na Insha. Maneno yenye sauti zinazotatiza yalisomwa kwa sauti kisha wanafunzi kuyaandika. Matokeo yalifanyiwa uchanganuzi baadaye. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu za uchanganuzi thamano na wingiudadi. Katika kuchanganua data, Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi ilitumika zaidi ilhali Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ilitumiwa kama kijalizo. Kazi hii inatarajiwa kuwa mchango mkubwa katika isimu tumizi hasa pana la ujifunzaji lugha ya pili.

## ABSTRACT

The Kenya National Examinations Council reports contained in its newsletters (1989 – 2004 ) indicate that Kiswahili is poorly performed both at primary and secondary levels. Although this problem has been persistent in Siaya District since the inception of 8.4.4 system of education, very few in-depth linguistic research have been carried out to establish the possible causes and give recommendations for possible remedies. This study, therefore, aimed at finding out whether the differences that exist between Luo and Swahili phonology constitute a learning difficulty for Luo speakers learning Standard Swahili. The researcher identified the differences that exist between Luo and Swahili phonological structures and how they constitute learning difficulties among Luo speakers learning Kiswahili as their second language. The study targeted standard five and six pupils selected from five rural primary schools in Gem Location of Siaya District. One hundred respondents from the five primary schools selected by way of purposive random sampling constituted the sample. The study focused on Luo L1 speakers who mainly use Swahili language in school and rarely use this language at home. This area was chosen because it is one of the regions where a population of predominantly Luo L1 speakers with Swahili as L2 are found. The research also attempted to show how poor pronunciation could be transferred to written work. The data was obtained from narrations of experiences, which were tape recorded so as to identify and classify speakers' pronunciation errors in order to establish any relationship between pronunciations and spellings. The researcher dictated words which posed pronunciation difficulty to the Luo learners. Data collected was analyzed by use of quantitative and qualitative methods. Contrastive Analysis theory and Natural Generative theory were used as the main and supplementary theories respectively. It was found that in the acquisition of Standard Swahili by Luo speakers, some learning difficulties occur because of linguistic differences at the phonological levels of the two languages. This study is expected to contribute to applied linguistics especially the wider field of second language acquisition.

# YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
TABARUKU.....	iii
HATILINZI.....	iv
SHUKRANI.....	v
IKISIRI.....	vi
ABSTRACT.....	vii
YALIYOMO.....	viii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xiii
MAELEZO YA VIFUPISHI .....	xiv
MAELEZO YA ISTILAHU.....	xv

## SURA YA KWANZA: UTANGULIZI.....1

1:0.1 Usuli wa Mada.....	1
1:1 Mada ya Utafiti.....	1
1:2 Madhumuni ya Utafiti.....	2
1:3 Nadharia Tete.....	3
1:4 Mchango wa Utafiti.....	3
1:5 Upeo wa Utafiti.....	4
1:6 Mbinu za Utafiti .....	5
1:6:1 Ukusanyaji wa data.....	6
1:6:2 Mbinu za kukusanya Data.....	7
1:6:3 Uchanganuzi wa Data.....	9
1.7 Hitimisho.....	11

## SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO NA MISINGI YA

<b>NADHARIA.....</b>	<b>12</b>
2:1 Mapitio ya Maandiko.....	12
2.2. Misingi ya Nadharia.....	16



2:2:1	Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi.....	16
2:2: 2	Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia.....	19
2.3	Hitimisho.....	21

## **SURA YA TATU: MUUNDO WA KIFONOLOJIA WA LUGHA YA**

<b>KISWAHILI SANIFU NA DHOLUO .....</b>	<b>22</b>	
3:1	Utangulizi .....	22
3:2	Fonimu za Kiswahili na Dholuo.....	23
3:3	Fonimu za Kiswahili .....	23
3:4	Konsonanti za Kiswahili.....	26
3:4:1	Hali ya Glota.....	26
3:4:3.2	Mahali pa Kutamkia.....	28
3:4:4	Jinsi ya Kutamka.....	28
3:5	Vokali za Kiswahili.....	28
3:6	Mfuatano wa sauti katika kuunda maneno ya Kiswahili.....	36
3:6:1	Irabu.....	39
3:6:1:1	Mwanzo wa Neno.....	39
3:6:1:2	Mwisho wa Neno.....	40
3:6:1:3	Katikati ya Neno.....	40
3:6:1:4	Mwambatano wa Irabu.....	40
3:6:2	Konsonanti.....	41
3:6:2:1	Konsonanti mwanzo wa Neno.....	41
3:6:2:2	Konsonanti katikati ya Irabu.....	41
3:6:2:3	Konsonanti mwisho wa Neno.....	42
3:6:2:4	Mwambatano wa konsonanti.....	42
3:6:2:5	Mpangilio wa Konsonanti za Nazali [m] .....	44
3:6:2:6	Mpangilio wa Konsonanti za Nazali [n] .....	45
3:6:2:7	Mpangilio wa Konsonanti zisizo za Nazali.....	45
3:7	Silabi Katika Kiswahilik(v).....	48
3:7:1	Silabi iliyoungwa kwa Irabu/Vokali Pekee [v] .....	48
3:7:2	Silabi ya Konsonanti na Vokali.....	50

3:7:3 Konsonanti ambatano ikifuatwa na Vokali [kv]..	50
3:7:4 Silabi iliyoundwa kwa Konsonanti Pekee [k] ..	51
3:8 Mkazo.....	52
3.9 Mifanyiko ya Kifonolojia inavyoathiri Silabi za Kiswahili.....	53
3:9:1 Udondoshaji.....	54
3:9:2 Uchopekaji.....	54
3:10:0 Sauti za Dholuo.....	54
3:10:1 Konsonanti za Dholuo.....	55
3:10:1. 1 Hali ya Glota.....	55
3:10:1.2 Mahali pa Kutamkia.....	56
3:10:1.3 Jinsi ya Kutamka.....	58
3:10:1.3:1 Vipasuo.....	58
3:10:1.3:3 Sauti za Nazali.....	59
3:10:1.3.4 Vitambaza.....	60
3:10:1.3.5 Vimadende.....	60
3:10:3:5 Viyeyusho.....	60
3:11 Vokali Za Dholuo.....	63
3:11:1 Irabu Fupi.....	63
3:11:2 Irabu Ndefu.....	64
3:11:3 Mahali pa Kutamkia Irabu.....	65
3:11:4 Mwinuko wa Ulimi.....	66
3:11:5 Mkao wa Midomo.....	67
3:12 Mfuatano wa Sauti za Dholuo.....	67
3:12:1 Irabu .....	68
3:12:1:1 Mwanzo wa Neno.....	68
3:12:1:2 Mwisho wa Neno.....	68
3:12:1:3 Katikati ya Neno.....	69
3:12:1:4 Mwambatano wa Irabu.....	69
3:12:2:0 Konsonanti.....	70
3:12:2:1 Konsonanti Mwanzo wa Neno.....	70
3:12:2:2 Konsonanti Katikati ya Irabu.....	70

3:12:2:3 Konsonanti mwisho wa neno.....	71
3:12:2:4 Mwambatano wa Konsonanti.....	71
3:13 Silabi Katika Dholuo.....	74
3:13:1 Silabi za Vokali Pekee [v] .....	74
3:13:2 Silabi ya Konsonanti na Irabu [kv] .....	77
3:13:3 Silabi ya Konsonanti Moja pamoja na nusu Irabu.....	78
3:14 Mkazo.....	79
3:15 Udondoshaji.....	80
3:16 Uchopekaji.....	81
3:17 Ubashiri Wa Makosa Kwa Mujibu Wa Nadharia Ya Uchanganuzi Linganuzi na Fonolojia Zalishi Asilia .....	85
3.18 Hitimisho.....	86

**SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA MAKOSA YA MATAMSHI NA  
MAANDISHI YANAYOTOKANA NA ATHARI ZA KIFONOLOJIA KWA  
WASEMAJI WA DHOLUO WANAOFUNZA KISWAHILI.....86**

4:1 Utangulizi.....	86
4.2 Athari za Utamkaji Wa Sauti za konsonati.....	86
4:3 Usahihishaji Mno.....	88
4.4 Athari Za Utamkaji Wa Sauti za irabu.....	89
4:5 Mkazo.....	90
4. 6Mifanyiko ya Kifonolojia.....	91
4:6:1 Uchopekaji.....	91
4:6:1:1 Uchopekaji wa Irabu.....	92
4:6:1:2 Uchopekaji wa Konsonanti.....	93
4:6:1:3 Uchopekaji wa Silabi.....	94
4:7 Udondoshaji.....	96
4:7:1 Kudondoshwa kwa Konsonanti.....	96
4:7:2 Kudondoshwa kwa Vokali.....	97
4:7:3 Udondoshaji wa Silabi nzima.....	99
4:8 Usilibishwaji.....	100

4:8:1 Silabi ya Irabu katikati mwa neno.....	100
4:8:2 Silabi iliyoungwa kwa konsonanti Endelevi –Nazali [kv].....	101
4:9 Athari zinazotokana na Kanuni za Kifonotaktiki.....	102
4.10 Hitimisho.....	103

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 104**

5.1 Utangulizi.....	104
5:2 Utafiti kwa jumla .....	104
5:3 Vikwazo.....	108
5:4 Mapendekezo.....	108

MAREJELEO.....	110
----------------	-----

VIAMBATISHO .....	117
-------------------	-----

Kiambatisho A: Hojaji.....	117
----------------------------	-----

Kiambatisho B: Hadithi za Kusimuliwa.....	118
---	-----

Kiambatisho C: Insha .....	119
----------------------------	-----

Kiambatisho D: Maneno ya Kusomwa kwa Sauti na Kuandikwa (Imla).....	120
---	-----

Kiambatisho E: Sentensi za Kusomwa kwa Sauti.....	121
---	-----

Kiambatisho F: Taarifa fupi ya Kusomwa kwa Sauti.....	122
---	-----

Kiambatisho G: Ramani ya Tarafa ya Gem.....	123
---	-----

## ORODHA YA MAJEDWALI

3.1	Jinsi ya kutamka konsonanti za Kiswahili .....	27
3.2	Mahali pa kutamkia konsonanti za Kiswahili.....	30
3.3	Konsonanti za Kiswahili.....	36
3.4	Irabu za Kiswahili.....	39
3.5	Mfuatano wa sauti za konsonanti katika Kuunda maneno ya Kiswahili.....	47
3.6	Jinsi ya Kutamka.....	56
3.7	Mahali pa kutamkia konsonanti za Dholuo .....	57
3.8	Konsonanti za Dholuo.....	61
3.9	Unukuzi wa sauti na maneno ya Dholuo.....	62
3.10	Mfuatano wa sauti za konsonanti katika kuunda maneno ya Dholuo.....	74
4.1	Athari za Dholuo kwa matamshi na maandishi ya Kiswahili.....	87
4.2	Usahihishaji mno.....	89

## MAELEZO YA VIFUPISHI

AKIKI	Alfabeti ya kifonolojia ya kimataifa [International Phonetic Alphabet]
K.N.E.C	Kenya National Examinations Council [Baraza la mitihani ya kitaifa la Kenya]
L1	First Language/Lugha ya Kwanza
L2	Second Language/Lugha ya Pili
L.A.D	Language Acquisition Device [Cheche za upataji na ujifunzaji lugha]
N.F.Z.A	Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia [Natural Generative Phonology]
N.U.L	Nadharia ya uchanganuzi linganuzi [Contrastive Analysis Theory]
Nn	Neno
K	Konsonanti
V	Vokali

## **MAELEZO YA ISTILAHU**

### **Athari za lugha**

Ni ujuzi wa lugha fulani ambao ni tofauti na lugha nyingine unaoweza kuvuruga au kuvunja mfumo na mpangilio wa lugha hiyo nyingine.

### **Unukuzi Makinifu**

Aina ya unukuzi ambao hutumia ishara au alama ambazo huzingatia tofauti ndogondogo za sifa za sauti.

### **Lugha ya Kwanza**

Lugha ambayo mtu anajifunza ikiwa ya kwanza.

### **Lugha ya Pili**

Lugha anayojifunza mtu baada ya kujifunza lugha ya kwanza..

### **Jozi Mlinganuo Finyu**

Maneno mawili ambayo tofauti yake inatokana na fonimu moja tu.

### **Kigezo cha utamkaji**

Kanuni ambayo hutawala utamkaji wa sauti.

### **Kipumuo**

Kitamkwa kinachotamkwa kwa kutoa pumzi kali.

### **Shina la Ulimi**

Sehemu ya mwisho nyuma ya ulimi.

### **Silabi funge**

Silabi ambayo huishia na konsonanti .

## **Shadda Funge**

Shadda ambayo huwekwa mahali maalumu

## **Irabu msingi**

Irabu dhahania zinazotumiwa kama kielelezo cha kuelezea mfumo wa irabu katika lugha.

## **Umilisi**

Ujuzi wa kanuni zinazotawala lugha Fulani

## **Uchanganuzi linganuzi**

Utaratibu wa kuchanganua vipashio vya lugha kwa kuzingatia ulinganuzi.

## **Silabi wazi**

Silabi inayoishia na irabu.

## **Othografia**

Tahajia iliyokubaliwa rasmi kuwa ni sanifu

## **Usahihishaji mno**

Huwa unahusu utamkaji mbaya wa maneno au utumiaji wa tungo za kisarufi ambazo hazikubaliki katika jitihada za kujaribu kuepuka athari za kitarafa au za lugha ya kwanza.

## **Ruwaza**

Mpangilio wa vipashio vya lugha unaofuata utaratibu maalumu.

## **Bashiri**

Kutoa taarifa ya kukisia juu ya kitu kinachoweza kutokea.



**Arudhi**

Neno linalojumuisha mabadiliko katika kidatu , mkazo, kiimbo na wakaa, wakati wa utamkaji wa sauti za msingi.

**Nyuzi sauti**

Misuli iliyo kwenye kisanduku cha sauti ambayo hutoa sauti inaporindima.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Usuli Wa Mada

Dholuo (lugha ya Waluo) ni mojawapo ya lugha za Kinailoti ambazo zinazungumuzwa katika mkoa wa Nyanza, Magharibi mwa Kenya, kwenye ufuo wa ziwa Victoria (Omondi 1982:11) Waluo wanaojifunza lugha ya Kiswahili hutatizika kutamka sauti fulani za Kiswahili na hivyo basi kuandika sauti hizo vibaya. Jambo hili limeathiri matokeo ya mtihani wa kitaifa na pia mawasiliano yao kupitia kwa lugha ya Kiswahili. Ili kuthibitisha jambo hili, wanafunzi Waluo ambao ni Wanailoti walichaguliwa ili kufanyiwa utafiti.

Katika kujifunza lugha ya pili, wanafunzi hutatizika; kwa hivyo, hufanya makosa. Katika kuzungumzia hali hii, Lado (1957), anasema kuwa makosa haya ni ushahidi au thibitisho kuwa wanafunzi hukumbwa na matatizo yanayotokana na tofauti ya mifumo sauti ya lugha ya kwanza na ya pili. Weinreich (1953:1) anasema ... "Jinsi tofauti katika mifumo ya lugha ya kwanza na ya pili inavyojitokeza ndivyo inavyokuwa vigumu kwa mwanafunzi kujifunza lugha ya pili"( tafsiri hii na nyingine zitakazofuata ni za mwandishi). Nimeafikiana na Lado na Weinreich kikamilifu. Kwa hakika ukweli huu ndio uliojenga msingi ambamo utafiti huu umejikita.

Hii inaonyesha kuwa makosa yanayoweza kujitokeza katika kujifunza lugha ya pili yanaweza kubashiriwa kwa kulinganisha lugha hizi mbili. Ujuzi wa tofauti hizi husaidia kuvyaza mbinu za kujinasua kutokana na shida hizi kama anavyosema Fries (1945:9) kuwa: ... "Njia mwafaka ni zile zinazofuata hatua za kisayansi ambazo hulinganisha lugha ya kwanza na ya pili".

Kutokana na maelezo haya inabainika wazi kuwa kuna haja ya kufanya utafiti kutafuta kiini cha kiisimu kubainisha athari za kifonolojia kwa wasemaji wa Dholuo kama lugha ya kwanza wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

### **1.1 Mada ya Utafiti**

Jamii ya Waluo ni miongoni mwa jamii za Kenya zinazotumia Kiswahili kama lugha ya pili. Hata hivyo haijulikani ni kwa jinsi gani athari za kifonolojia za mfumo wa lugha ya Dholuo zinavyowatatiza katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu. Kwa jumla mada hii ilishughulikia uchunguzi wa makosa ya matamshi na hijai yanayofanywa na wazungumzaji wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

### **1.2 Madhumuni ya Utafiti**

Katika kuchunguza athari za kifonolojia kwa wasemaji wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili, utafiti huu ulilenga kueleza jinsi tofauti za kifonolojia kati ya Dholuo na Kiswahili huweza kutatiza ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Tumelitimiza lengo hili kuu kwa:

- (i) Kutambulisha vitamkwa vinavyotatiza wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili
- (ii) Kuchunguza tofauti za kifonolojia kati ya Dholuo na Kiswahili kwa kurejelea jinsi tofauti hizo za kifonolojia huathiri wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.
- (iii) Kuchunguza na kueleza athari za matamshi mabaya kwa maandishi (tahijia).

### **1.3 Nadharia Tete**

Katika utafiti huu, tuliongozwa na makisio yafuatayo:

- (i) Baadhi ya vitamkwa vya lugha ya Kiswahili huwatatiza wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

- (ii) Tofauti kati ya lugha ya Dholuo na lugha ya Kiswahili ndizo hutatiza wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.
- (iii) Utamkaji mbaya wa baadhi ya vitamkwa vya Kiswahili na wasemaji wazawa wa lugha ya Dholuo wanaojifunza Kiswahili huweza kusababisha makosa katika maandishi ya maneno ya Kiswahili.

#### 1.4 Mchango wa Utafiti

Kuna kazi au tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu athari za lugha ya kwanza katika kujifunza lugha ya pili hususan katika nchi za ng'ambo. Kazi chache zimefanywa hasa kuhusu uhusiano kati ya lugha ya Kiswahili na Dholuo; kwa hivyo, kazi hii inanuiwa kuziba mwanya au pengo hili.

Watafiti kama Kimani (1971), Wanyoike (1978), Mbaabu (1985) wameweza kutaja kuwa wanafunzi kutoka jamii lugha mbalimbali hutatizika kujifunza Kiswahili kwa sababu ya lugha zao za kwanza. Wanyoike (1978:37) anapendekeza kufanywe utafiti wa kina kuhusu athari za lugha ya kwanza katika kujifunza lugha ya pili. Musau (1993) amelinganisha fonolojia za lugha saba na lugha ya Kiswahili naye Mudhune (1994) ameshughulikia mofosintaksia ya Kiswahili na Dholuo na jinsi inavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Hakuna utafiti wowote uliowahi kufanywa kutambulisha shida za matamshi na jinsi shida hizo huathiri maendeleo na hijai katika uandishi baina ya wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Utafiti huu ulikusudiwa kuliwekea swala hili msingi utakaojengewa watafiti wa baadaye.

Utafiti huu utasaidia katika kuthibitisha au kukanusha madai ya Lado (1957) kuwa kujifunza lugha ya pili, mtu hutatizwa na mfumo wa lugha ya kwanza. Matokeo ya utafiti huu yatapiga hatua kubwa kuwasaidia walimu wa Kiswahili kuzua mbinu mwafaka kuwasaidia hawa wazungumzaji wa Dholuo kama lugha yao ya kwanza. Walimu watanufaika kutokana na kazi hii kwa sababu watapata ujuzi zaidi na waweze kuimarisha mbinu za ufundishaji na kukosoa makosa ya wanafunzi yatokanayo na athari za lugha zao za kwanza kifonolojia katika matumizi ya Kiswahili.

Utafiti huu ni mchango muhimu katika uwanja mpana wa kujifunza lugha ya pili katika taaluma ya isimu na pia ni changamoto kwa wasomi wengine wanaotaka kufanya utafiti zaidi katika taaluma hii. Hii ni kwa sababu data muhimu zimetolewa na zitatumiwa katika kuimarisha matumizi ya Kiswahili. Utafiti huu, pia utasaidia wanaoandaa mitaala na waandishi wa vitabu kuweka mikakati ifaayo ya kuimarisha umahiri wa Kiswahili katika wilaya ya Siaya na kwingineko nchini.

Mwisho, utafiti huu umenuia kutoa mwelekeo kwa washirika wote au washikadau wote katika kampeni za kutambua umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili sanifu, matatizo yanayoikumba lugha hii na kuzua mikakati mipya itakayoivezesha lugha hii kutumiwa kikamilifu katika mawasiliano miongoni mwa wakaazi wa Gem Wilayani Siaya.

### **1.5 Upeo wa Utafiti**

Katika tasnifu hii tulijihusisha na athari za kifonolojia za lugha ya Dholuo kwa wasemaji wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Kwanza, tulishughulikia makosa ya matamshi yanayotokana na athari za kifonolojia kwa wasemaji wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Kisha tulichunguza kama makosa haya hujitokeza katika maandishi. Tulihusisha wanafunzi wa darasa la tano na sita. Mgawanyo huu ulikusudiwa kuchunguza kama kuna tofauti zozote ambazo zinajitokeza hasa tukizingatia idadi ya makosa.

Wanafunzi wa darasa la tano na sita walichaguliwa kwa sababu, katika kiwango hiki, hawajaimarika sana katika umilisi wa lugha. Aidha, wao hufanya makosa mengi ya hijai na matamshi. Wanafunzi ambao hutoka jamii lugha ambayo hutumia lugha moja ya kwanza, hutumia lugha ya pili kwa nadra sana, labda wakiwa shuleni pekee.

Tulitumia hojaji ili kuhakikisha kuwa, wanafunzi walioshiriki walitoka katika jamii zilizo tumia Dholuo nyumbani na Kiswahili shuleni. Wanafunzi waliohusishwa

ni wale ambao wazazi wote wawili (Baba na Mama) walikuwa wazungumzaji wazawa wa Dholuo. (Taz. Kiambatisho A)

Maswala muhimu yaliyoshughulikiwa ni sauti za konsonanti, irabu, utiaji mkazo katika neno, usilibishaji na mifanyiko ya kifonojia kama vile uchopekaji, udondoshaji miongoni mwa mengine. Kutokana na upungufu wa kifedha na wakati, haikuwezakana kufanya utafiti katika kila sehemu ya Wilaya ya Siaya au mkoa wa Nyanza. Hata hivyo, kwa kutumia njia ya uteuzi huru ulioratibiwa katika kuteua shule tano kutoka tarafa ya Gem, Wilaya ya Siaya, utafiti huu ulijitokeza na picha kamili kuhusu athari za kifonolojia kwa wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

Kutokana na sababu ya kuwa eneo la utafiti ni pana, jumla ya wasailiwa mia moja waliteuliwa kwa kutumia sampuli ya uteuzi huru (Ishirini kutoka kila shule). Wasailiwa hawa walijumuisha wanafunzi wa darasa la tano na sita. Uteuzi huru wa sampuli ulizingatia kwa dhati mada na madhumuni ya utafiti huu. Wanafunzi wanaozungumza Dholuo kama LI pekee ndio walioteuliwa: wavulana hamsini na wasichana hamsini wenye umri kati ya miaka kumi na miwili na kumi na minne ndio waliohusishwa.

### **1.6 Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu ulichunguza athari za kifonolojia kwa wazungumzaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili. Ili kuweza kukusanya data, njia mbili za utafiti zilitumiwa:

- i. Utafiti maktabani
- ii. Utafiti wa nyanjani

#### **i. Utafiti wa Maktabani**

Utafiti huu ulifanywa kwa kuchunguza maandishi mbalimbali kuhusu athari za kifonolojia katika kujifunza lugha ya pili pamoja na tafiti zingine ambazo zimewahi kufanywa kuhusu lugha ya Dholuo. Kufanya hivyo kuituwezeshwa kupata msingi bora wa kuchunguza athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Aidha, mapitio ya

maandishi yalitusaidia kuelewa maoni ya wataalamu mbalimbali wa lugha kuhusu athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili.

## **ii. Utafiti wa Nyanjani**

Utafiti huu ulijikita katika Wilaya ya Siaya, tarafa ya Gem. Uteuzi wa Wilaya hii ulitokana na msingi kuwa wanafunzi wazawa wa sehemu hii hutumia Dholuo nyumbani na Kiswahili shuleni, jambo ambalo linafanya ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kuathiriwa na Dholuo. Katika kuchunguza athari za Dholuo katika Kiswahili utafiti huu ulikusanya data kutoka kwa wanafunzi mia moja kutoka shule tano ya Tarafa ya Gem. Shule hizi ziliteuliwa kwa kutumia sampuli ya uteuzi huru ulioratibiwa. Uchunguzi huu ulitumia data zilizopatikana kama kielelezo cha athari za kifonolojia za Dholuo katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

### **1.6.1 Ukusanyaji wa Data**

Utafiti huu ulihusu sauti za Kiswahili zinazotatiza wanafunzi wazawa wa Dholuo. Wanafunzi wa darasa la tano na sita katika shule tano za msingi wilayani Siaya tarafa ya Gem walihusishwa katika kukusanya data hii. Kwa kutumia madarasa mawili, watafiti walichunguza mabadiliko ambayo hutokea katika viwango mbalimbali vya elimu. Tuliamua kuwatumia wanafunzi wa darasa la tano na sita wa tarafa ya Gem ili kutimiza mahitaji maalumu yaliyopendekezwa na Ellis (1985:4) ambayo ni kutumia watafitiwa wenye viwango sawa kama vile:

- a) Elimu sawa
- b) Mazingira yanayofanana
- c) Umri sawa
- d) Wazungumzaji wa lugha ya kwanza inayofanana.

Ili kutimiza haya tulitumia hojaji ili kuteuwa watafitiwa ambao wazazi wote wawili walikuwa wazungumzaji wazawa wa Dholuo.

Shule hizi tano ziliteuliwa kwa njia ya bahati nasibu (uteuzi huru). Tulitumia jumuiya ya watafitiwa mia moja waliohusishwa katika utafiti. Ni imani yetu kwamba data iliyopatikana kutoka shule hizi tano imetosheleza mahitaji ya utafiti huu.

### 1.6.2 Mbinu za Kukusanya Data

Mbinu zilizotumika kuziteua fonimu zinazotatiza wanafunzi wazawa wa Dholuo kutamka na kuandika zilizingatia; hazina ya kifonemiki ya Kiswahili na Dholuo na vidadisi vya kutupatia data iliyostahiki utafiti huu. Tulitayarisha kidadisi ambacho sauti za maneno yake yalikuwa na mfumo wa nitoe – nikotoe yaani jozi mlinganuo finyu (Taz. Kiambatisho D)

Insha na masimulizi yalitumiwa kama utafiti mwanzo. Tulijihusisha na sauti ambazo hazipatikani katika hazina ya kifonemiki ya Dholuo (Okombo 1982 :19).

Selinger na Shohamy (1989) na Larse Freeman na Long (1994:5) wanatoa mapendekezo yafuatayo kuhusu mbinu za kukusanya data inayohusu makosa ya wanafunzi:

- a) Kuwaambia wanafunzi kusimulia hadithi fupi.
- b) Kuwaambia wanafunzi waandike insha.

Tulitumia njia ya masimulizi ya hadithi fupi. Masimulizi haya yalikuwa muhimu kwani ni kupitia kwa matukio au visa mbalimbali ambapo wanafunzi huweza kutoa mawazo yao yanavyofululizwa kwa uhalisia wao na hivyo, kubainisha uwezo wa lugha. Watafitiwa walipewa dakika tano kusimulia hadithi fupi kuhusu mada walizopewa (tazama kiambatisho D)

Tulinasa mazungumzo hayo katika kinasa sauti ili kutambua na kuchunguza vitamkwa vilivyotatiza wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Masimulizi ya wanafunzi yalitusaidia kubainisha makosa ya kimatamshi ya wanafunzi wazawa wa Dholuo yanayotokana na athari za kifonolojia za Dholuo kwa lugha ya Kiswahili. Mbali na masimulizi, watafitiwa walipewa mada ili kuandika insha juu yake (taz. Kiambatisho C) Insha hii ilinuiwa kuthibitisha ikiwa ni kweli kama wanafunzi wanapofululiza mawazo yao kwa uhalisia, basi



kwa kiwango fulani , huweza kuathiriwa na lugha yao ya kwanza. Data iliyopatikana ilimsaidia mtafiti kuthibitisha ikiwa ni kweli kuna uhusiano mkubwa baina ya hijai na matamshi katika Kiswahili, jambo linalomfanya mwanafunzi kuandika maneno ya Kiswahili jinsi anavyoyatamka hasa kwa misingi na kanuni za lugha ya Dholuo. Insha za wanafunzi zilisahihishwa kwa kurejelea tu fonimu teule(v, z, f x na x). Fonimu hizi zilizotajwa, ni zile ambazo hazipatikani katika hazina ya kifonemiki ya Dholuo kulingana na Okombo (1982 :19)

Watafitiwa, pia, walisoma kwa sauti. Sauti zao zilinaswa kwenye kinasa sauti kisha kufanyiwa uchanganuzi ili kubainisha ikiwa kuna makosa yoyote ya matamshi. Altenberg na Vago (1983:29) na Corder (1983:60) wanasema kuwa mtindo wa kusoma ni muhimu kwa vile hufanya wanafunzi wasikwepe kutamka sauti ambazo huwatatiza. Njia hii pia ilitumiwa na Beebe na Fledge (1980). Kwa hivyo watafitiwa walisoma kwa sauti mambo haya:

- a) Orodha ya maneno hamsini ya Kiswahili yenye sauti zinazotatiza wasemaji wazawa wa Dholuo (jozi mlinganuo finyu). Mtafiti alichagua maneno kwa kurejelea hazina ya kifonemiki ya lugha ya Dholuo. Sauti ambazo hazipatikani katika orodha ya fonimu za Dholuo (tazama kiambatisho A).
- b) Sentensi fupifupi zilizoandikwa kwa njia mahususi ili kuzua matamshi yanayotatiza.(tazama kiambatisho B)
- c) Taarifa fupi iliyoandikwa kwa njia mahususi ili kuzua matamshi yanayotatiza wanafunzi wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili. (Tazama kiambatisho C)

Watafitiwa walisomewa imla ili kubainisha makosa ya kihijai yanayosababishwa na athari za Dholuo kwa Kiswahili. Maneno yenye sauti zinazotatiza Waluo kutamka yalisomwa kwa sauti kisha wanafunzi wakaagizwa kuyaandika walisomewa maneno mawilimawili (Jozi mlinganuofinyu). Walisomewa maneno hayo mara tatu (kwanza walisikiliza, pili waliandika, tatu wahakikishe kama wameandika vizuri).Mtafiti alijinasa Kwenye chombo cha kunasia sauti ili kuhakikisha kuwa sauti zote zilitamkwa vizuri. Matokeo yalikusanywa kisha kufanyiwa uchanganuzi baadaye.

Tulifanya hivyo ili kujaribu kuthibitisha ikiwa ni kweli kuna uhusiano au ukuruba wowote baina ya hijai na matamshi katika Kiswahili jambo analomfanya mwanafunzi kuandika maneno ya Kiswahili jinsi alivyoyatamka hasa kwa misingi na kanuni za Dholuo. Matokeo yalimsaidia mtafiti kuthibitisha au kupinga kauli ya wataalam Sapir (1921), Bloomfield (1933: 21), Fillmore (1981) na Aronoff (1985) ambao wanashikilia kuwa kuna ukuruba baina ya matamshi na maandishi.

Sapir (1921) anasema kuwa maandishi ni ishara zinazohifadhi usemi au tamko. Bloomfield (1933:21) anasema maandishi si lugha bali ni njia ya kuhifadhi lugha kupitia kwa hati. Naye Fillmore (1981) anasema kuwa mawasiliano kupitia kwa maandishi huwa ni njia mojawapo ya mazungumzo ya ana kwa ana. Aronoff (1985:28) anataja kuwa lugha zungumzi ni ukweli lakini lugha andishi ni thibitisho au ushahidi wa ukweli huo. Mukuthuria (2004) anasema kuwa matamshi ya mtu kila mara huwa na athari za lugha ya kwanza. Athari hizi, pia kupitia matamshi, zinaweza kujitokeza katika maandishi. Aghalabu, namna tunavyozungumza ndivyo tunavyoandika. Maelezo ya wataalam hawa yanathibitisha kuwa kuna uhusiano kati ya matamshi na maandishi.

### **1.6.3 Uchanganuzi wa Data**

Katika uchanganuzi wa data tulitumia uchanganuzi thamano na wingiidadi ambapo tulitumia mbinu za msambao wa umaratokezi na kipimio cha ulemeokati cha wastani. Data iliyokusanywa iliwekwa pamoja katika utaratibu ili iweze kufanyiwa uchanganuzi.

Kisha ilihaririwa kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa ni sahihi, kamilifu na inayo kubalika. Baadaye, iliainishwa na kupangwa katika makundi pamoja na kutumia majedwali na tarakimu. Hatimaye, data ilijumulishwa pamoja kwa namna inayorahisisha utoaji wa matokeo kwa swala lililochochea utafiti huu

### 1.6.3.1 Hatua ya kwanza

Mtafiti alitambulisha na kuorodhesha vitamkwa ambavyo hutatiza Waluo kutamka katika lugha ya Kiswahili (kutokana na masimulizi pamoja na insha walizoziandika) Watafitiwa walisoma taarifa yenye maneno hamsini yenye matamshi/vitamkwa ambavyo hutatiza Waluo. Kisha akaorodhesha idadi ya makosa ya matamshi yaliyotokea. (Tazama kimbatisho C na D)

Mtafiti aliangalia kila kosa la matamshi lililojitokeza, mara ngapi. Jumla ya makosa ilitumiwa kupata wastani wa kihesabu. (Dulay na Burt 1974:44-45)

$$\frac{\text{Makosa yote}}{\text{Jumla ya majaribio (maneno)}} \times 100 = \text{asilimia ya makosa}$$

### 1.6.3.2 Hatua ya pili

Watafitiwa walisomewa orodha ya maneno hamsini yenye vitamkwa vinavyowatatiza wanafunzi wazawa wa Dholuo kutamka, ili kuchunguza kama kuna makosa yoyote ya hijai. Mtafiti alijinasa kwenye kanda ya kunasia sauti ili kuhakikisha kuwa maneno hayo yalitamkwa vizuri, yaani kuzuia uwezekano wa makosa hayo kuwa ni ya mtafiti mwenyewe. Tulitaka kubainisha kama kuna ukuruba wowote baina ya makosa ya matamshi na hijai. Kazi za wanafunzi zilisahihishwa ili kubainisha idadi kamili ya makosa ya hijai na kuzilinganisha na makosa ya matamshi. (Taz. Jedwali 4.1 na 4.2)

### 1.6.3.3 Hatua ya tatu

Tulichunguza uhusiano kati ya utamkaji mbaya na uendelezaji mbaya kwa kulinganisha kiasi cha makosa ya matamshi na hijai. Makosa ya matamshi yaliainishwa; kisha kuchunguzwa kwa kurejelea mazoezi ya imla, jinsi makosa hayo yalivyojitokeza katika maandishi.

Baada ya kubainisha na kuainisha makosa katika viwango , tulichanganua na kueleza jinsi makosa hayo yanatokana na athari za Dholuo kifonolojia na jinsi yanavyochangia kwa ujumla katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika wilaya ya Siaya (tarafa ya Gem).

### **1.7 Hitimisho**

Katika sura hii , tulishughulikia maswala ya kimsingi yaliyotuongoza katika utafiti huu. Mambo haya yalikuwa kama dira katika kazi hii, kwa vile, yalitupatia mwelekeo uliotusaidia kufanikisha kazi hii. Mambo yaliyoshughulikiwa ni kama : Usuli wa mada, mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, natija ya utafiti, upeo wa utafiti, mbinu za utafiti na maelezo ya istilahi zilizotumiwa katika utafiti.

## SURA YA PILI

### 2.1 MAPITIO YA MAANDIKO

Kuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusu ujifunzaji wa lugha za pili na matatizo yanayoambatana nazo. Baadhi ya wataalamu walioshughulikia swala hili ni pamoja na Lado (1957), Halliday (1964) Stamper na Stampe (1979) Corder (1978), Dulay, Burt na Krashen (1982) Mbaabu (1985), Wanyoike (1978) Beshu (1991), Musau (1993), Mudhune (1994). Massamba (1987), Vitale (1985), Bakari (1982), Fromkin na Rodman (1983), Mukuthuria (2004), Onyango (1997) na Mangwa (2005).

Lado (1957:2) anasema kwamba mwanafunzi anayekumbana na lugha ngeni atapata vipashio vyake fulani vikiwa rahisi na vingine vigumu sana. Zile sehemu zilizo sawa na zile za lugha yake asili zitakuwa rahisi kwake na zile ambazo ni tofauti zitakuwa ngumu. Iwapo sauti fulani katika lugha ya kwanza haipo katika lugha ya pili, mwanafunzi atajaribu kuiongeza kwa kutumia sauti ya lugha yake asili inayoonekana kukaribiana na iliyo katika muundo wa lugha yake ya kwanza. Tunakubaliana na Lado (1957); hata hivyo, tumesonga mbele zaidi kuchunguza na kueleza jinsi tofauti hizi huathiri msemaji wa Dholuo anapojifunza Kiswahili.

Halliday (1964) anasema kwamba ujifunzaji wa lugha ya pili, kwa kawaida, hufanyika baada ya kujifunza lugha ya kwanza kukamilika. Katika kiwango hiki, ajifunzaye lugha huwa tayari amejenga umilisi wa kutosha wa kimawasiliano katika lugha yake ya kwanza. Kwa hivyo, lugha ya kwanza ya mwanafunzi huathiri kwa kiasi lugha ya pili. Ingawa tafiti huyo ameshughulikia lugha tofauti, lakini maelezo haya yalitufaa sana katika utafiti huu kwani yalitusaidia kuthibitisha au kupinga kwa kuzingatia wanafunzi Waluo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Wanafunzi hao, mbali na kuwa na umilisi wa lugha yao ya kwanza ya Dholuo, wamejifunza Kiswahili huku wakiathiriwa na Dholuo.

Naye Corder (1978:132) aligundua kutokana utafiti wake kuwa, watu wanapojifunza lugha ya pili, huwa tayari wanayo l1 ya kwanza. Baadhi ya kanuni wanazozielewa katika lugha ya kwanza hutumivatika usemaji na uelewaji wa lugha ya pili. Kutokana na hali hii, kuna mazoaa kutumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili; hivyo, makosa hutokeMaoni haya ya wataalamu hawa wawili ni muhimu kwa utafiti huu kwani yametkeza kupambanua, kuelewa na kueleza athari za kifonolojia kwa wasemaji awa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili.

Wanyoike (1978) alishughulikia fonolojia ambapoonyesha mifano mbalimbali ya ukiukaji wa kaida za matamshi ya Kiswahili Saninaofanywa na wanafunzi kutoka jamii kadhaa za Kenya kama Wakikuyu, Wakan, Wakalenjin na Waluo. Mtafiti huyu hakufanya utafiti wa kina; ndipo akatoaoni kwamba kunahitajika sasa kufanywe uchunguzi unaohusiana na kujifunza kwahili ili kudhihirisha ni matatizo gani ya kipekee yanayowakabili watu kutokajamii mbalimbali wanapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

Massamba (1987) anasisitiza kwamba kila lughaa kanuni zake za kupanga sauti ili kuunda maneno. Katika hali hii, kuna mipangiliayoruhusiwa na ile isiyoruhusiwa. Hali hii kwa kiasi kikubwa hupelekea lughaa kwanza kuathiri lugha ya pili. Tunakubaliana na Massamba; hata hivyo, sisi tupiga hatua zaidi kwa kuchunguza, kuchambua na kueleza jinsi tofauti za mfumcauti wa lugha ya kwanza huathiri mfumo sauti wa lugha ya pili katika kiwango ch kifonolojia.

Fromkin na Rodman (1983) wanadokeza kwami tofauti za kimuundo baina ya L1 na L2 hupelekea msemaji wa L2 kuathirika na L1 Kwa kutumia Nadharia za Fonolojia Zalishi Asilia (FZA) Bakari (1982) anadhihiria kwamba mifanyiko ya kifonolojia husaidia mtu anayejifunza lugha ya pili kudbiti na kurahisisha usemaji wa hiyo lugha. Huku akiwanukuu Bakari (1982) na Hyman (1975) Aswani (1995) ameendeleza kauli hii katika muktadha wa lgha kuingiliana, ambapo L1 inaathiri L2. Maoni haya ya wataalamu wa awa ni muhimu kwa utafiti huu kwani yametuelekeza kuelewa na kueleza mchango wa mifanyiko ya kifonolojia.

Mbaabu (1985) alifanya utafiti ambapo hakuwalenga wanafunzi darasani. Alichunguza makosa ya kifonolojia, kisarufi na kisemantiki yanayofanywa na Wakenya mbalimbali wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Anadai kwamba baadhi ya makosa haya yanatokana na lugha ya kwanza. Pia, Mbaabu (1985) aliandika kuhusu makosa ya kawaida yanayotokea mara kwa mara wakati watu wanapojaribu kuzungumza na kuandika Kiswahili Sanifu. Alikusanya na kuyasahihisha makosa yanayotokana na athari za lugha ya kwanza ambayo yanajumuisha yale ya kimsamiati na kifonolojia. Kadhalika, aliyachunguza makosa ya kimatamshi na kisarufi ambapo kaida za matumizi ya viambishi hukiukwa. Ingawa utafiti wa Mbaabu umetaja baadhi ya athari zinazotokana na lugha ya Dholuo kwa wale wanaojifunza lugha ya Kiswahili, unaonekana kuwa wa kijuujuu na wa kijumla sana, hii ndiyo sababu tuliamua kushughulikia undani swala la athari za lugha ya kwanza katika kiwango cha kifonolojia na hijai ili kuthibitisha jinsi athari hizi zinavyochangia katika kudhoofisha ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili.

Besha (1991) alifanya utafiti uliowalenga watu wazima wa jamii ya Kimaasai wanaojifunza Kiswahili nchini Tanzania kwa upande wa matamshi, upangaji maneno, mfumo wa majina pamoja na miundo ya vitenzi vya Kiswahili, ameshughulikia ujifunzaji wa lugha ya pili. Ni muhimu kutaja hapa kwamba anayoyasema mtafiti yamechangia pakubwa katika kueleza uchunguzi wetu, ni bayana kuwa mtazamo wake ulilenga wasemaji wazawa wa lugha ya Kimasai, ilhali sisi tukijishughulisha na ujifunzaji huo unavyoathiriwa kifonolojia na lugha ya Dholuo.

Mangwa (2005), alifanya utafiti ambapo alichunguza athari za Ekegusii katika Kiswahili na zinavyochangia matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili kwa wanafunzi wa Kisii wilayani Kisii Kusini. Amedhihirisha jinsi lugha ya Ekegusii inavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili. Anasema kuwa matokeo ya mtihani wa Kiswahili katika kidato cha nne ni tatizo la kitaifa. Sehemu mbalimbali nchini zinaathiriwa na hali hii. Kazi hii ililenga kubainisha kiini hasa cha matokeo mabaya ya lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa Ekegusii wa kidato cha nne. Tofauti na kazi hii, utafiti huu ulijikita katika kuchunguza athari za kifonolijia kwa wasemaji wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili.

Musau (1993) alilinganisha fonolojia ya lugha saba; Kiluo, Kikuyu, Kimaasai, Kikamba Kibukusu, Kinandi, Kisomali na ya Kiswahili. Utafiti wake ulilenga watu wazima (wanafunzi wa vyo vya walimu wa shule za msingi). Alilinganisha lugha hizi na lugha ya Kiswahili katika kiwango cha matamshi pekee lakini hakuangalia jinsi tofauti hizi huathiri maandishi au hijai. Katika utafiti huu tulichunguza jinsi athari hizi huweza kujitokeza katika maandishi. Kazi hii ya Musau ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu ameshughulikia lugha saba Dholuo ikiwa miongoni mwao. Kwa hivyo matokeo ya kazi yake inaoana moja kwa moja na azma ya utafiti wetu.

Mudhune (1994) alilinganisha mofosintaksia ya Dholuo na Kiswahili na jinsi tofauti hizo zinavyowaathiri wanafunzi wanaojifunza Kiswahili Sanifu. Kutokana na kazi yake, imebainika wazi kwamba swala la lugha ya Dholuo kuathiri Kiswahili kama lugha ya pili lipo. Matokeo ya kazi yake imechangia pakubwa utafiti wetu ingawa mtafiti huyu alishughulikia maswala ya sarufi na wala si fonolojia.

Mukuthuria (2004) alichunguza jinsi lugha ya Kiswahili huathiriana na Kitigania katika ngazi ya mofolojia na chanzo cha athari hizo. Kutokana na utafiti wake ilibainika kwamba maingiliano ya lugha huibuka pale ambapo mifumo miwili tofauti ya lugha ikitumiwa kwa ajili ya mawasiliano. Anaendelea kusema kuwa lugha zote zinazotumika katika jamii-lugha ya Kenya zifanyiwe utafiti kama huo, ujikite katika viwango mbalimbali vya lugha kama vile fonolojia, sintaksia, semantiki na kadhalika.

Onyango (1977), ameshughulikia tofauti za kisarufi zilizopo kati ya Kinyala na Kiswahili sanifu ili kubainisha kama tofauti hizo ni kikwazo kwa Wanyala wanapojifunza Kiswahili sanifu. Katika utafiti huu amewalenga wanafunzi wa darasa la nane wilayani Busia. Alibainisha kwamba makosa ya kisarufi katika Kiswahili cha wanafunzi Wanyala hutokana na athari za lugha ya kwanza kwa Kiswahili. Hata hivyo, kazi yake haikushughulikia athari za kifonolojia bali ilijikita katika kuchunguza maswala ya kisarufi. Hili ndilo pengo linalofidiwa na utafiti huu ambao ulichunguza athari za kifonolojia kwa wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili.



Utafiti huu unanuiwa kuziba mwanya pamoja na kuchangia kitaalamu katika eneo hili pana la athari za lugha ya kwanza katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Kwa ujumla, maandishi haya yalitoa mwanga hasa kwa upande wa mbinu za kufanya utafiti na vigezo muhimu vya kuzingatia katika kuchunguza athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili.

## **2.2 Misingi ya Nadharia**

Kulingana na kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981), nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Kuna nadharia kadhaa ambazo zimewahi kutumiwa na watafiti katika utafiti wa athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji na utumiaji wa lugha ya pili. Nadharia zilizotuongoza katika kazi hii ni Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi (N.U.L) na Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia (NFZA).

### **2.2.1 Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi**

Nadharia ya uchanganuzi linganuzi hushikilia kuwa lugha ya kwanza huathiri kujifunza kwa lugha ya pili; kwa hivyo, ndicho kizuizi kikuu katika kujifunza lugha ya pili. Kulingana na waasisi wa nadharia hii, muundo wa lugha ya kwanza ( $L_1$ ) hutofautiana na muundo wa lugha ya pili ( $L_2$ ). Hali hii husababisha muundo wa lugha ya kwanza kuingizwa katika lugha ya pili. Hali hii hutokana na athari za kimazoea za lugha ya kwanza.

Nadharia ya uchanganuzi linganuzi ilitusaidia kubainisha sauti zinazowatatiza Waluo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Tuliweza kubashiri athari za kifonolojia kwa kuangalia fonimu katika lugha zote mbili na jinsi sauti hizo hutamkwa yaani ala za matamshi zinazohusishwa katika kuzitamka sauti hizo na pahali pa kuzitamkia sauti hizo. Lado (1957:Vii) ametoa mwongozo wa jinsi Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi inavyoweza kutumiwa kulinganisha lugha mbili. Katika dibaji ya kitabu chake anasema: "...tunaweza kubashiri na kueleza sauti ambazo zinaweza kutatiza na

zisizotatiza kwa kulinganisha lugha ambayo mwanafunzi anajifunza na lugha yake ya kwanza”.

Kulingana na Okombo (1982:19) tunaweza kubashiri kuwa wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili huweza kupata ugumu kutamka sauti zifuatazo [v, z, ], x, γ] kwa sababu sauti hizi hazipatikani katika abjadi ya Dholuo (Tazama 3:10 ). Tulilinganisha sauti/fonimu za lugha hizi mbili kifonolojia ili kubainisha kama kuna athari zozote zinazojitokeza (tazama kiambatisho D). James (1980:3-4) anasema kwamba uchanganuzi linganuzi huchunguza katika kiwango cha mtu binafsi jinsi mzungumzaji wa lugha ya kwanza anavyoendelea kuimudu lugha ya pili.

Lado (1957:2) anaeleza kwamba uchanganuzi linganuzi huchukulia kwamba watu hujaribu kuhamisha maumbo na maana kutoka lugha zao za kwanza hadi lugha ya pili. Kwa hivyo, uchanganuzi linganuzi unahusu namna lugha ya kwanza inavyomwathiri mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili kimatamshi, kisarufi na kisemantiki. Kulingana na Lado (1957), Makosa ya kimatamshi huweza kutokea ikiwa kuna vitamkwa katika lugha ya pili lakini haviko katika lugha ya kwanza ya mwanafunzi.

Wataalamu Van Els na wenzake (1984) wameeleza kuwa nadharia ya uchanganuzi linganuzi imejikita katika nguzo zifuatazo:

- a) Sababu kuu inayoleta matatizo na kuzua makosa katika kujifunza lugha ya pili ni zile athari za lugha ya kwanza.
- b) Kadiri lugha ya kwanza na ya pili zinavyotofautiana kimuundo ndivyo jitihada za kujifunza lugha ya pili zinavyotatizwa zaidi.
- c) Matokeo ya kuzilinganisha lugha hizo mbili hutumiwa kubashiri yale matatizo na makosa yatakayotokea wakati wa kujifunza lugha ya pili.
- d) Mwalimu wa lugha anahitaji kufunza zile tofauti zinazodhihirika kati ya lugha hizo mbili. Utaratibu unaofuatwa katika kuchanganua vipashio vya lugha ni kuzilinganisha na kuzitofautisha ili kudhihirisha zinavyofanana na kutofautiana. Hii ina maana kwamba tofauti kati ya lugha ya kwanza na lugha

ya pili ndiyo itatizayo ujifunzaji wa lugha ya pili, ilhali kufanana kwao hurahisisha ujifunzaji huo (Lado 1957:2)

Verma na Krishnaswamy (1989) katika kuelezea nadharia ya uchanganuzi linganuzi wanasema kuwa wakati mwanafunzi anajifunza lugha ya kwanza, fikira zake zote huelekezwa kwenye mfumo wa lugha ya kwanza kupitia kwa mazoea ya matumizi. Anapoanza kujifunza lugha ya pili ukinzano wa kimfumo hutokea. Kulingana na wataalam hawa makosa au athari hutokea kwa sababu zifuatazo:

- a) Matamshi ambayo hufuata hijai moja kwa moja.
- b) Mvuto kutoka lugha ya kwanza
- c) Kutokuelewa mifumo ya lugha ya pili.
- d) Usawazisho kwa misingi ya lugha ya kwanza.

Mwanafunzi mluo ambaye anajifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili huwa katika hali ya ukinzano kwa sababu fikra ya mwanafunzi huyu huwa imetawaliwa na miundo na matamshi ya lugha ya Dholuo.

Ellis (1985:25) amezitambua na kuziorodhesha daraja tatu za utaratibu wa uchanganuzi linganuzi. Daraja hizo ni:

- a) Maelezo mwafaka ya lugha mbili husika
- b) Uamuzi kuhusu vipengele hivyo katika lugha hizo mbili.
- c) Ubashiri wa sehemu fulani za lugha ambazo huenda zikasababisha makosa.

Nadharia ya uchanganuzi linganuzi huangalia au huzingatia mifumo miwili au zaidi ya lugha. Kwa hivyo, tulipochunguza miundo ya lugha hizi mbili (Dholuo na Kiswahili) tuliweza kubashiri sehemu fulani za lugha ambazo huenda zikasababisha makosa au ugumu katika kujifunza lugha ya pili.

Hata hivyo, kuna baadhi ya waandishi ambao wamepinga nadharia ya uchanganuzi linganuzi James (1980: 146) anasema kuwa nadharia ya uchanganuzi linganuzi inaweza kutumiwa kubashiri kutokea kwa kosa fulani la lugha lakini haiwezi

kutumiwa kubashiri umbo halisi la kosa hilo litakavyokuwa (kama ni la kimatamshi, kisarufu au kimuundo).

James (1980:152) na wasomi wengine wanapinga kwamba si vizuri uchanganuzi linganuzi kudai kwamba wanafunzi wafunzwe tu tofauti zilizopo baina ya lugha ya kwanza na ya pili bali wafunzwe kufanana kwa lugha hizi mbili ili waweze kujigundulia ni wapi uhamishaji wao wa vipengele vya lugha ya kwanza hadi lugha ya pili hukubalika na ni wapi havikubaliki. Wataalamu hao wanasema kwamba si rahisi kukadiria kikweli viwango vya ugumu katika kujifunza vipengele mbalimbali vya lugha. Ugumu huo hauwezi kukadiriwa kwa kuzirejelea tu zile tofauti za kiisimu zinazojitokeza

### **2.2.2 Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia**

Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ina misingi yake katika kauli kwamba kuna jambo la kijumla na lenye uasilia katika miundo ya kifonolojia ya lugha. Kwa mujibu wa Anderson (1985), misingi hii ya Fonolojia Zalishi Asilia imejikita katika uwezo wa kifonolojia wa mwanadamu wa kutamka sauti kwa kutumia ala za kutamkia na kuzipanga sauti hizo kwa kuongozwa na ubongo wake. Anasema kwamba kuna mambo ya kijumla na asilia yanayohusiana na mifumo yote ya kifonolojia inayotokana na hali kwamba uzungumzi hupangwa na kuongozwa na ubongo na viungo au ala zinazotumika katika utamkaji.

Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ni mojawapo ya nadharia zilizozuka kupinga nadharia ya Fonolojia Zalishi Geuzaumbo. Nadharia hii iliendelezwa sana na Theovenemann na kufafanuliwa na Hooper (1976) inarejelea mambo matatu muhimu;

- a) Hali ya uasilia yenye nguvu
- b) Hakuna hali ya upangaji
- c) Hali halisi ya makisio ya kijumla.

Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia imekashifiwa na baadhi ya wataalamu kwamba haijitoshelezi. Hata hivyo, hakuna nadharia yoyote ambayo inajitosheleza bila kuchangiwa hapa na pale. Kwa kuzingatia nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia, tulichanganua jinsi mwanafunzi wa Dholuo anapozungumza Kiswahili huwa amepanga fikira yake kwa mpangilio wa lugha yake ya kwanza.

Donegan na Stampe (1979) wanasema kuwa mifanyiko ya kifonetiki na kifonolojia hutawaliwa na ile hali ya kuweko kwa hali ya uhalisia yenye nguvu au mvuto. Ni nguvu hizi ambazo hutawala sauti au foni zinazotolewa. Wataalam Donegan na Stampe (1979) wameeleza kuwa Nadharia ya Fonolojia Asilia imejikita katika nguzo zifuatazo:

- a) Ni nadharia asilia
- b) Hakuna ushahidi kuwa mabadiliko ya kifonolojia na matamshi ya watoto hufunzwa, bali ni swala la kiasilia.
- c) Mifanyiko huwa ni ya kiasilia kutokana na mvuto wa nguvu za kifonolojia. Wanafunzi wazawa wa Dholuo hawana uzoefu wa sauti hizi kwa vile sauti hizi hazipatikani katika fonolojia ya lugha ya Dholuo.
- d) Makosa ya matamshi hutokana na ile hali ya watoto kushindwa kuzuia mfumo asilia.

Tuliongozwa na Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia kuchunguza chanzo cha makosa ya kifonolojia katika lugha ya pili. Nadharia hii ilitusaidia kubainisha kiisimu sababu za wanafunzi Waluo wanaojifunza lugha ya Kiswahili kufanya makosa fulani au kuwa na ugumu kutamka sauti fulani. Tulirejelea ala za matamshi na sehemu za kutamkia sauti ili kubainisha kama sauti zinazowatatiza wasemaji wazawa wa Dholuo hutamkwa kutoka mahali maalumu. Tulirejelea orodha ya sauti za Dholuo (Okoth 1982: 12) na kubainisha ni sauti zipi ambazo hazipatikani humo na zinapatikana katika orodha ya sauti za Kiswahili. Fonimu ambazo hazipatikani katika orodha ya fonimu ya Dholuo ni (v, z,  $\int$ , x,  $\gamma$ ). Kwa hivyo nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ilitusaidia kubainisha iwapo sauti hizi, ambazo ni za vikwamiza huweza kuwatatiza wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili.

### 2.3: Hitimisho

Katika sura hii, tulipitia hoja za wataalamu mbalimbali kuhusu swala la athari ya L1 kwa L2. Ilidhihirika wazi kwamba athari ya L1 kwa L2 ni jambo linalohusu wote wanaojifunza lugha ya pili (L2). Mapitio ya maandishi ya wataalamu mbalimbali katika sura hii yalionyesha kuwako kwa pengo la tafiti zinazolenga kuibua athari za kifonolojia kwa wasemaji wa L1 wanaojifunza L2. Aidha tulijaribu kuthibitisha kuwa pana haja ya kufanya utafiti wa namna hii miongoni mwa lugha zote ambazo zinahusiana na Kiswahili au lugha ambazo zinapatikana katika mazingira ambamo lugha ya Kiswahili inatumika. Hii ni kwa sababu takriban zote zimeathiri lugha ya Kiswahili katika ngazi mbalimbali.

Pia tulitumia nadharia zote mbili kwa sababu hakuna inayojitosheleza yenyewe kwa vile kila mojawapo ina faida na upungufu wake. Hata hivyo, zote zina lengo moja la kimsingi ambalo ni kufanikisha ufunzaji wa lugha lengwa kwa kuchunguza swala la makosa katika misingi ya kisayansi inayokubalika na nadharia ya kiisimu na ile ya ujifunzaji wa lugha ya pili.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

## SURA YA TATU

### 3.0 MUUNDO WA KIFONOLOJIA WA LUGHA YA KISWAHILI SANIFU NA DHOLUO

#### 3.1 Utangulizi

Sura hii imegawanywa katika sehemu mbili kuu. Inachunguza na kulenga kubainisha miundo ya kifonolojia ya lugha ya Kiswahili na Dholuo. Katika kufanya hivi imezingatiwa kwamba tofauti za mifumo sauti kati ya lugha ya Kiswahili na Dholuo ndiyo husababisha athari za L1 katika L2. Ufahamu mzuri wa muundo wa kifonolojia wa lugha ya Kiswahili na Dholuo ulituwezesha kuyabaini mabadiliko ya kifonolojia yanayotokea pindi mzungumzaji wa Dholuo anayejifunza Kiswahili anapoathiriwa na lugha yake ya kwanza (mfumo lugha ya Dholuo). Hivyo ni kusema kuwa msingi wa athari za L1 na L2 kifonolojia hutokana na tofauti za kimuundo baina ya lugha zinazohusika.

Katika sehemu hii tumezitalii fonimu za lugha ya Dholuo na Kiswahili, kanuni za mfuatano wa fonimu hizo katika ujenzi wa vipashio vikubwa kama silabi na maneno, na mabadiliko ya sauti za lugha hizi mbili kwa mujibu wa mazingira mbalimbali ya kifonolojia. Kisha tulichunguza miundo ya silabi za Dholuo na Kiswahili na uwekaji wa mipaka katika silabi hizo. Hatimaye, tulichunguza swala la mkazo katika lugha hizi mbili. Tumelinganisha muundo wa Kiswahili na ule wa Dholuo ili kuafiki lengo kuu la utafiti huu.

Sridhar (1981:207) amependekeza kuwa, anayefanya uchunguzi au utafiti kwa mintirafu ya uchanganuzi linganuzi, sharti awe na data kamili kuhusu miundo na mifumo sauti ya lugha zote mbili. Ndipo sura hii imelenga kubainisha miundo ya kifonolojia ya Kiswahili sanifu na Dholuo.

Tumefuata njia iliyopendekezwa na Ellis (1983:26) ambaye amezitambua na kuziorodhesha daraja tatu za utaratibu wa uchanganuzi linganuzi. Daraja hizo ni:

- (a) Maelezo mwafaka ya lugha mbili husika.
- (b) Uamuzi kuhusu vipengele hivyo katika lugha hizo mbili.
- (c) Ubashiri wa sehemu fulani za lugha ambazo huenda zikisababisha makosa.

Lugha huundwa kwa sauti. Ili kuelewa asili ya lugha, ni lazima tuanze kwa kuangalia sauti zake.

### **3.2 Fonimu za Kiswahili na Dholuo.**

Katika tasnifu hii, neno fonimu limetumika kwa maana ya kipandesauti ambacho huleta tofauti katika maana ya neno kikipachikwa katika neno hilo. Fonimu ni kipashio kidogo kabisa cha kifonolojia kinachobadili maana ya neno (Aswani 2001). Fonolojia kwa hivyo, ni tawi la isimu ambalo hujishughulisha na uchunguzi wa mifumo ya sauti za lugha mahsusi kama vile Dholuo na Kiswahili. Nia kuu ya sehemu hii ni kudhihirisha nafasi inayochukuliwa na fonimu katika hijai ya Kiswahili na Dholuo, ikiwa na msingi wake katika herufi za alfabeti. Alfabeti ni kundi la ishara zilizoandikwa na kuelezwa kama konsonanti na vokali, kila mojawapo ikiwakilisha aina moja ya sauti. Sauti au vipande sauti ambavyo husababisha tofauti kimaana katika maneno ya lugha mahsusi hujulikana, kiisimu kama fonimu.

Dhana ya fonimu ndiyo chanzo cha maandishi ya kifabeti. Kila fonimu inawakilishwa na ishara yake mahsusi; na hivyo, fonimu za vokali, kwa mfano, huwakilishwa na ishara zinazojulikana, kiothografia kama vokali na konsonanti. Katika kila lugha, alfabeti inayotumika katika othografia huzingatia ukubaliano au mshabaha kati ya alama moja na fonimu ambayo ni aina ya sauti moja. Katika Dholuo na Kiswahili kuna mshabaha mkubwa kati ya maandishi na mfumo wa utamkaji. Ingawa kila lugha ina ruwaza ya kipekee ya mpangilio wa sauti, sauti za lugha zote hugawanywa katika makundi mawili, ambayo ni konsonanti na vokali.

### **3.3 Fonimu za Kiswahili**

Wataalamu mbalimbali wamewahi kufanya utafiti juu ya fonimu za Kiswahili. Hawa ni pamoja na Ashton (1944), Whiteley (1974), Polome (1967), Mfaume (1984),



Nchimbi (1992) na Mgullu (1999). Wataalam hawa wanatofautiana katika idadi ya fonimu-konsonanti walizoziorodhesha. Wote wanaafikiana juu ya idadi ya fonimu-irabu.

Nimefuata orodha ya Nchimbi (1992) kwa vile ameorodhesha pia fonimu ambazo kimaandishi huwakilishwa kwa mfungamano wa nazali [m] pamoja na konsonanti[b] yaani [m̄b], pia konsonanti nazali [n] na konsonanti [d], [ʃ] na [ɟ] yaani [n̄d], [n̄ʃ] na [n̄ɟ]. Mfungamano mwambatano unapotamkwa katika lugha ya Kiswahili, husikika kama ni sauti moja, na kisaikolojia hokusudiwa na mtamkaji kuwa sauti moja.

Wakati mwingine, ikiwa kuna mfungamano mwambatano wa fonimu za nazali na fonimu zingine, sauti hizi huungana na kuwa fonimu moja na wakati mwingine haziungani (Mgullu 1999:69). Sauti hizi haziungani kila mara lakini huungana katika mazingira maalumu ambapo Konsonanti nazali si silabi.

Ingawa jambo hili ni tata, kazi hii imetumia kigezo cha matamshi na wala si cha maandishi kwa hivyo tunaamini ya kuwa, katika mazingira hayo maalumu sauti hizi huungana na kuwa fonimu moja. ( taz. 3.6.2.4)

Data ifuatayo ni dhihirisho la madai hayo:

- |                         |  |
|-------------------------|--|
| (i) [m̄b] kama katika   | [kam̄ba] - kamba<br>[pam̄ba] - pamba<br>[m̄boga] - mboga               |
| (ii) [n̄d] kama katika  | [pund̄a] - punda<br>[nd̄ovu] - ndovu                                   |
| (iii) [n̄ʃ] kama katika | [kun̄ʃa] - kunja<br>[n̄ʃia] - njia                                     |
| (iv) [n̄ɟ] kama katika  | [un̄ga] - unga<br>[an̄ga] - anga<br>[fun̄ga] - funga<br>[an̄ga] - anga |

Nchimbi (1992) anadai kwamba miambatano hii huwakilisha sauti moja katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, orodha ya fonimu za Kiswahili zilizotumika katika tasnifu hii ni:

### Vokali

#### Foni Unukuzi

[a] [ala]	-	a - ala
[e] [e le za]	-	e - eleza
[i] [inama]	-	i - inama
[o] [o ta]	-	o - ota
[u] [umiza]	-	u - umiza

#### Otografia

#### Konsonanti

[p] [paka] [panda]	p - paka panda
[t] [taka] [ta ma]	t - taka tema
[č] [čai] [čimba]	ch - chai chimba
[k] [kata] [keti]	k - kato keti
[b] [baba] [baraka]	b - baba baraka
[d] [dada] [daka]	d - dada daka
[ŋ] [ŋ ombe] [ŋ ambo]	ng' - ng'ombe - ng'ambo

#### Otografia

[f] [faa]	f - faa
[j] [jani]	j - jani
[g] [gawa]	g - gawa
[m] [mate]	m - mate
[mb̄] [mbaja]	mb - mbaya
[nd̄] [ndoa]	nd - ndoa
[nj̄] [njama]	nj - njama
[nḡ] [ngumu]	ng - ngumu
[θ] [θeluji]	th - theluji

[s] [siri]	s – siri
[ʃ] [ʃati]	sh – shati
[h] [hati]	h – hati
[v] [vaa]	v – vaa
[ð] [ð ambi]	dh – dhambi
[z] [zaraa]	z – zaraa
[r] [roho]	r – roho
[l] [lia]	l – lia
[j] [jai]	y – yai
[ɣ] [ɣali]	gh – ghali
[w] [lewa]	w – lewa
[x] [xeri]	kh – kheri

### 3.4.0 Konsonanti za Kiswahili

Sauti za konsonanti huainishwa kwa kuzingatia jinsi ya kutamka na mahala pa kutamka. Sauti hizi za konsonanti huelezwa kwa kuzingatia sifa tatu kuu ambazo ni: upumuaji, mahali pa kutamkia na jinsi ya kutamka.

#### 3.4.1 Hali ya glota

Pumzi zinazotoka mapafuni husukumwa nje kupitia mkondo-hewa kuelekea nyuzi za sauti na kupitia kinywani, puani au viungo vyote viwili. Katika sehemu ya nyuzi za sauti, kuna misuli miembamba ambavyo hujenga nyuzi hizo. Viungo hivyo huweza kuchukua hali mbili. Vinaweza kupanuka au vinaweza kubana. Ikiwa nyuzi za sauti zimepanuka, mwanya huachwa katikati, na ikiwa zimebanwa huwa, zimefungwa. Hali hii husababisha glota kutoa sauti zinazotofautiana.

Glota inaweza ; inapofunguka, pumzi husukumwa kutoka kwa mapafu kupitia mkondo hewa uliobanwa. Sauti zote, ambazo hutolewa wakati ambapo glota imefunguka, huitwa sauti hafifu (sighuna). Ikiwa nyuzi za sauti zimevutwa pamoja, glota hufungika na pumzi kutoka mapafuni, husukuma nyuzi hizo ili kuzitenganisha na kusababisha mrindimo. Sauti zitolewazo katika hali hii huelezwa kuwa ghuna.

Katika lugha ya Kiswahili sauti au fonimu ambazo sikhuna ni: [p] [t] [ɕ] [k] [ʃ] [θ] [s]  
[h]

Nazo sauti ghuna ni hizi: [b] [d] [ʒ] [g] [v] [ð] [z] [ʒ] [m] [n] [ɲ] [ŋ] [l] [w] [r] [j]  
[mb] [nd] [ng] [nj]

Data ifuatayo ni ithibati ya maelezo hayo.

Sauti hafifu (sikhuna)	Sauti ghuna
[p] – [paa] – paa	[b] – [baba] – baba
[t] – [taa] – taa	[d] – [dada] – dada
[ɕ] – [ɕ aka] – chaka	[ʒ] – [ʒuma] – juma
[k] – [kata] – kata	[g] – [gogo] – gogo
[f] – [fika] – fika	[v] – [vaa] – vaa
[θ] – [θe luji] – theluji	[ð] – [ð ana] – dhana
[s] – [sasa] – sasa	[z] – [zana] – zana
[ʃ] – [ʃuka] – shuka	[ʒ] – [ʒ ali] – ghali
[h] – [hama] – hama	[m] – [mama] – mama
	[n] – [nena] – nena
	[ɲ] – [ɲ ama] – nyama
	[ŋ] – [ŋ ombe] – ng'ombe
	[l] – [lala] – lala
	[r] – [ruka] – ruka
	[w] – [watu] – watu
	[j] – [jetu] – yetu
	[mb] – [mbao] – mbao
	[nd] – [ndovu] – ndovu
	[ng] – [nguo] – nguo
	[nj] – [njeo] – njeo

Jedwali 3.1: Jinsi ya kutamka Konsonanti za Kiswahili [ghuna- sikhuna]

### 3.4.3.2 Mahali pa Kutamkia

Katika utamkaji wa konsonanti, pumzi au mkondo wa hewa kutoka mapafuni hupitia pango la kinywa ambapo, kwa kiasi fulani, huzuiliwazuiliwa kinywani. Mahali ambapo hewa huzuiliwa, wakati sauti hutamkwa, huitwa mahali pa kutamkia. Mahali pa kutamkia ni muhimu sana katika uelezaji wa sauti, hususan, konsonanti. Katika kutamka sauti [p], mdomo wa chini na ule wa juu hugusana, na hewa kutoka mapafuni huzuiliwa na midomo kwa muda. Kwa hivyo, fonimu [p] ni sauti ya midomo. Isitoshe, [b] hutamkiwa pale pale. Sauti hizi mbili ni za midomo. Tukiangalia [f], tunaona kuwa mdomo wa chini hukaribia meno ya juu. Pumzi kutoka mapafuni huzuiliwa kati ya mdomo wa chini na meno ya juu. Kwa mintarafu hii, [f] inakuwa mdomo meno. Fonimu [v] hutamkwa mahali palepale. Katika kutamka fonimu [t] na [d], tunaona kuwa ncha ya ulimi hukaribia ufizi. Pumzi kutoka mapafuni huzuiliwa kati ya ala hizi mbili kwa muda. Kwa msingi huu basi, fonimu [t] na [d] ni sauti za ufizi.

Ukizingatia hali ya glota na mahali pa kutamkia, tunaweza, kueleza jozi hizi za sauti ifuatavyo:

- [p] – Sauti sikhuna ya midomo
- [b] – Sauti ghuna ya midomo
- [f] – Sauti si guna ya mdomo – meno.
- [t] – Sauti sikhuna ya ufizi
- [d] – Sauti ghuna ya ufizi

Tunapotamka sauti [č] na [ʃ], ala mbili hushirikiana, ambazo ni ncha ya ulimi, ambayo hukaribia kaaka gumu, ilhali sehemu ya mbele ya ulimi hujipinda kwenye ukuta wa kinywa. Sauti hii hutokea katika maneno kama:

- [č] – [cama] – chama
- [ʃ] – [Jambo] – jambo
- [č] – [če. ma] – chema
- [ʃ] – [Jitu] – jitu

Sauti nyingine zipatikanazo kwenye kaakaa gumu ni kama vile [ɲ] na [j] kama vile zinavyodhihirika katika maneno yafuatayo:

[ɲ] – [ɲ ama] – nyama

[ɲ] – [ɲ ani] – nyani

[j] – [jai] – yai

[j] – [jaja] – yaya

Kuhusu sauti za kaakaa laini, sehemu ya nyuma ya ulimi hukaribia kaakaa laini. Sauti zitamkiwazo kwenye kaakaa laini ni: [k] [g] [ɣ] [ŋ] [x]. (Mgullu 1999: 27)

[ɣ] – kama vile katika [ɣ ali] – ghali

[k] – kama vile katika [kândo] – kando

[g] – kama vile katika [gâmba] – gamba

[ŋ] – kama vile katika – [ŋ omb e] – ng'ombe

[x] – kama vile katika – [xeri] - kheri

Kwa upande wake, sauti ya koromeo ni moja tu, ambayo ni [h], kama vile katika

[h] – [hapa] – hapa

[h] – [hali] – hali

[h] – [hapo] – hapo

Sehemu	Fonimu	Neno
Mdomo wa juu na chini	[p]	[pãnda]
	[b]	[bãnda]
	[m̃b]	[m̃bao]
	[m]	[mama]
Mdomo wa chini na meno ya juu	[f]	[faa]
	[v]	[vaa]
Meno	[θ]	[θ elufi]
	[ð]	[ð am̃bi]
Ufizi	[t]	[taa]
	[d]	[dada]
	[s]	[saa]
	[z]	[zaa]
	[l]	[lala]
	[r]	[ruka]
	[nd̃]	[nd̃oa]
Kaakaa laini	[k]	[kaa]
	[ñg̃]	[ñg̃ao]
	[ɣ]	[ɣ ali]
	[x]	[xeri]
	[ŋ]	[ŋ am̃bo]
Kaakaa gumu	[ç]	[ç ama]
	[n]	[n ama]
	[ɲ]	[ɲ uki]
	[j]	[jule]
Midomo na kaakaa laini	[w]	[watu]
Koromeo	[h]	[hapa]
Kati ya kaakaa gumu na ufizi	[ʃ]	[ʃ ule]

Jedwali 3. 2: Mahali pa kutamkia konsonanti za Kiswahili

## Maelezo

- a) **Mdomo wa juu na chini** Baadhi ya sauti hutamkwa kwa kuikutanisha midomo yote miwili, kwa mfano [m] [b] na [p] [m̄b]
- b) **Mdomo na meno:** mahali pengine ambapo foni mbalimbali hutamkiwa in kwenye mdomo na meno. Kwa kawaida sauti hizi hutamkwa wakati mdomo wa chini unapokuwa umeyagusa meno ya juu. Mifano mizuri ya sauti hizi in pamoja na [ f ] na [v].
- c) **Meno:** mahali pengine ambapo foni hutamkiwa ni pale kwenye meno. Vitamkwa vinavyotamkiwa kwenye meno huitwa foni za meno. Wakati wa kuzitamka foni hizi ulimi huwekwa katikati ya meno ya juu na ya chini na hususan huwa umeyagusa meno ya juu. Mifano mizuri ya foni za meno in pamoja na [ θ ] na [ð].
- d) **Ufizi:** Ufizi ni mahali pengine ambapo foni za lugha hutamkiwa. Kwa kawaida wakati wa kuzitamka foni za ufizi ncha ya ulimi huwa imeugusa ufizi. Imebainika kuwa katika lugha ya Kiswahili, ufizi ndipo mahali ambapo fonimu nyingi zaidi hutamkiwa kuliko mahali pengine popote, mifano mizuri ya foni za ufizi ni pamoja na: [t] [d] [s] [z] [l] [r] [n] [n̄d]
- e) **Kati ya Kaakaa gumu na ufizi:** Sehemu nyingine ambayo hutumiwa wakati wa kutamka foni ni ile iliyopo kati ya ufizi na kaakaa gumu. Wakati wa kuzitamka foni hizi sehemu ya kati ya ulimi huinuliwa na kugusa sehemu iliyoko kati ya kaakaa gumu na ufizi. Mfano mzuri wa foni unaopatikana katika sehemu hii ni [ɕ] [ɟ] [ʃ] [ʒ] [nɟ]
- f) **Kaakaa laini.** Mahali pengine panapotumiwa kutamkia fonimu mbalimbali za lugha ya Kiswahili ni kwenye kaakaa laini. Aghalabu wakati wa kuzitamka foni hizo sehemu ya kati au nyuma ya ulimi huinuliwa hadi kukaribia au kugusa sehemu hiyo laini iliyo nyuma ya kinywa. Sehemu hizi hushirikiana na ulimi kutamka foni zifuatazo: [k] [g] [x] [x̄] [ŋ] [ŋ̄g]
- g) **Midomo na kaakaa laini:** Foni chache tu katika lugha ya Kiswahili ndizo hutamkiwa katika sehemu mbili tofauti na ambazo hazipo karibu. Sehemu hizo ni midomo, ambayo ipo mbele ya kinywa, na kaakaa laini iliyo nyuma ya kinywa. Sehemu hizi hushirikiana wakati wa kutamka fonimu fulani. Mfano mzuri wa fonimu za midomo na kaakaa laini ni nusu-irabu [w]



- h) **Koromeo.** Wakati mwingine baadhi ya fonimu katika lugha ya Kiswahili hutamkiwa kwenye koromeo. Wakati wa kuzitamka fonimu hizi, koromeo hubanwa kiasi fulani ili kuruhusu sauti kutoka. Mfano mzuri wa fonimu za koromeo ni: [h]

### 3.4.4 Jinsi ya Kutamka

Sauti zote hupangwa katika makundi kutegemea jinsi zinavyotamkwa. Konsonanti hutamkwa wakati hewa kutoka mapafuni huzuiliwazuiliwa au hutatizwa kinywani kwa namna fulani. Wakati mwingine hewa huzuiliwa kabisa na wakati mwingine hutatizwa kiasi. Kwa kuzingatia jinsi ya utamkaji wa konsonanti, kuna jinsi sita.

Aina	Idadi
a) Vizuiwa/vipasuo	06
b) Vikwamizwa	10
c) Vizuiwa – Kwamiza	02
d) Kitambaza	01
e) Kimadende	01
f) Nazali	08

#### 3.4.4.1 Vizuiwa/Vipasuo:

Hizi ni sauti zinazotamkwa wakati hewa kutoka mapafuni husukumwa nje kwa nguvu na huzuiwa kabisa kabla ya kuachiliwa kwa ghafla na kutoa sauti ambayo hufanana na sauti isikikayo wakati kitu kinapolipuka. Tunaweza kuzigawa sauti za vizuiwa kutegemea na mahali pa kutamkia kama ifuatavyo;

##### (i) Vipasuo vya Midomo.

Hizi ni fonimu [p] na [b] ambazo hutamkwa kwa kukutanisha midomo yote miwili

Mifano	[p] – [papa]	- papa
	[b] – [baba]	- baba

##### (ii) Vipasuo vya ufizi:

Fonimu hizi ni [t] na [d] zinatamkwa wakati ncha ya ulimi inagusana na ufizi wa juu.

Mifano:

[t] – [tamaa] - tamaa

[d] – [dada] - dada

**(iii) Vipasuo vya kaakaa gumu**

Hizi ni fonimu [ɕ] - [ɕ ama] - Chama

[ʃ] - [ʃ ambazi] - jambazi

**(iv) Vipasuo vya kaakaa laini.**

Fonimu [k] na [g] hutamkwa wakati kiwiliwi cha ulimi kwa nyuma inapogusana na kaakaa laini.

Mifano

[k] - [kaa] - kaa

[g] - [gunia] - gunia

**3.4.4.2 Vikwamizwa**

Vikwamizwa ni sauti ambazo hutamkwa wakati ambapo hewa kutoka mapafuni haizuiliwi moja kwa moja, kunakuwapo na mwanya kidogo wa kupitia hewa. Ni sawasawa na inayovuja au mpira wenye pancha. Vikwamizwa pia vimepangwa katika makundi kutegemea mahali pa kutamkia:

**(i) Vikwamizwa vya mdomo/meno:**

Sauti hizi hutamkwa wakati mdomo wa chini unapogusana na meno ya juu. Fonimu za vikwamilizwa vya mdumo/meno ni: [f] na [v]

Mifano

[f] - [fulana] - fulana

[v] - [vamia] - vama

**(ii) Vikwamizwa vya meno/ Sauti za Kimeno:**

Hizi hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapogusana na meno ya juu. Vitamkwa hivyo ni

[θ] na [ð].

Mifano:

[θ] - [θ amani] - thamani

[ð] - [ð amana] - dhamana

**(iii) Vikwamizwa vya ufizi:**

Fonimu hizi ni [s] na [z] ambazo hutamkwa ncha ya ulimi inapogusana na ufizi wa juu.

Mifano

[s] - [simba] - simba

[z] - [ziba] - ziba

**(iv) Vikwamizwa vya kaakaa gumu**

Sehemu ya mbele ya ulimi ikigusana na kaakaa gumu, fonimu [ʃ] hutamkwa.

Hutokea katika maneno kama

[ʃ] - [ʃ ime]- shime

[ʃ] - [ʃ ida] - Shida

**(v) Vikwamizwa vya kaakaa laini:**

Kiwiliwili cha ulimi cha nyuma kikigusana na kaakaa laini, foni [ɣ] hutolewa.

Mifano

[ɣ] - [ɣ ali] - ghali

[ɣ] - [ɣ ulamu] - ghulamu

**3.4.4.3 Nazali:**

Hizi ni konsonanti ambazo hutamkwa kwa kukishusha kimio kwa namna ambayo kiasi kikubwa cha hewa kutoka mapafuni huelekezwa kupitia kwenye chemba cha pua. Katika lugha ya Kiswahili, kuna nazali zipatazo nne: [n] [m] [ŋ] na [ɲ]. [mb̄] [nd̄] [nɳ̄] [nɠ̄]. Fonimu [m] hutamkwa wakati mdomo wa juu na mdomo wa chini hukutanishwa pamoja, [n] hutamkwa wakati ncha ya ulimi inagusana na ufizi wa juu; [ŋ] hutamkwa wakati bapa la ulimi kinagusana na kaakaa gumu na foni [ɲ] ambayo hutamkwa wakati kiwiliwili cha ulimi kinagusana na kaakaa laini. Mfano wa Nazali katika maneno ni kama zifuatazo:

[m] - [mama] - mama  
 [n] - [nani] - nani  
 [ŋ] - [ŋama] - nyama  
 [ɲ] - [ɲambo] - ng'ambo.  
 [m̄b] - [m̄buzi] - mbuzi  
 [n̄d] - [n̄doo] - ndoo  
 [nɟ] - [nɟaa] - njaa  
 [n̄ɡ] - [n̄ɡozi] - ngozi

#### 3.4.4.4 Vimadende

Hutamkwa wakati ncha ya ulimi inagusana na ufizi. Kutokana na nguvu ya hewa inayopita kati ya ncha hiyo na ufizi, ncha ya ulimi hugotagota ufizi kwa harakaharaka. Katika Kiswahili, kuna kimadende kimoja tu, [r]. Sauti hii hutokea katika maneno kama.

[r] - [rarua] - -rarua  
 [r] - [rafiki] - rafiki  
 [r] - [ruka] - ruka

#### 3.4.4.5 Viyeyusho

Hizi ni fonimu ambazo wakati wa kuzitamka hewa haizuiliwizuiwi kinywani. Sauti hizi ni [w] na [j]. Sauti hizi hutokea katika maneno kama:

[w] - [watu] - watu  
 [j] - [jai] - yai

Kwa hivyo, sauti zote huelezwa kulingana na vigezo vitatu ambavyo ni hali ya glota, mahali pa kutamkia na jinsi ya kutamka (Nchimbi 1992). Tazama chati ifuatiayo

## Konsonanti za Kiswahili

Namna ya kutamka	Midomo	Midomo meno	Meno	Ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaa laini	Koromeo
(i) Sighuna Vipasuo	p			t	č	k	
	b			d	ʃ	g	
(ii) Ghuna							
(i) Sighuna Vikwamizwa Ghuna		f	θ	s	ʃ	χ	h
		v	ð	z		ʒ	
Nazali	m			n		ng	
	m̄b			nd	ɲ ɲ̄	ŋ	
Vitambaza				l		n	
Vimadende				r			
Viyeyusho	w				j		

Jedwali la 3:3

Asili Nchimbi 1992 :14

### 3.1 Vokali za Kiswahili

Kiswahili kina irabu au vokali tano (Ashton, 1944:3; Polome (1967:46-47). Irabu hizo tano ni [i], [e] [a] [o] na [u]

[a] – katika – [kaa],	[baba], [ama]
[e] – katika – [pekee ],	[debe], [em̄be ]
[ i ] – katika – [bidii],	[bibi], [wifii]
[o] – katika – [ʃogoo],	[gogo], [zogo]
[u] – katika- [mfukuu],	[ʃufu], [sumu]

Katika Kiswahili Sanifu, hakuna tofauti ya maana baina ya irabu [e] na [ɛ], [o] na [ɔ], [i] na [ɪ], [ u ] na [ʊ]. Kwa sababu irabu za Kiswahili hazina sifa ya urefu (Mutahi, 1987:40).

Katika utamkaji wa irabu, hakuna ala zikurubianazo ili kupunguza upana wa mkondo hewa ili kuzuia pumzi. Kwa hivyo hakuna mkwaruzano au msugurano katika uwazi wa kuenuka au kooni, kama vile ilivyo na konsonanti. Vokali huelezwa kwa kuzingatia kwenda juu au kuwa chini kwa ulimi, nafasi ya ulimi kinywani na mkao wa mdomo. Kwa hivyo irabu hubainishwa kwa kuzingatia sifa kuu tatu yaan:

- (a) Mahali pa kutamkia irabu
- (b) Mwinuko wa ulimi
- (c) Mkao wa mdomo

### 3.5.1 Mahali pa kutamkia Irabu

Kuhusu mahali pa kutamkiwa irabu, sehemu tatu hutumiwa kuzitofautisha irabu. Sehemu hizo tatu ni:

(i) Sehemu ya mbele ya ulimi kama vile:

- [i] - [kiti] - kiti
- [e] - [čeza] - che za


(ii) Sehemu ya kati ya ulimi kama vile

- [a] - [alama]
- [kalamu]
- [kamati]

(iii) Sehemu ya nyuma ya ulimi kama vile:

- [u] - [ugonjwa]
- [o] - [ombi]

### Kielelezo 3:1 Mahali pa Kutamkia Irabu



Asili: Nchimbi 1992:14

### 3.5.2 Mwinuko wa Ulimi.

Mwinuko wa ulimi ni wa aina nne:

- (i) Mwinuko-chini kama vile [a] – ulimi huwa umeinuka kidogo sana; ulimi huwa umelala chini kwenye upande wa chini wa kinywa.

[a] – [alama]

[a] – [ahadi]

- (ii) Mwinuko-kati kama vile [e ] na [o ].

**Mifano**

[e] – elewa]

[o] – [oa]

- iv) Mwinuko-juu kama vile [ i ] na [u]. Ulimi huwa upande wa juu wa kinywa.

[i]- [inama]

[u]- [ulimi]

### 3.5.3 Mkao wa Midomo

Wakati wa kuzitamka irabu, mdomo huweza kukaa kwa namna mbili (Mgullu, 1999:31):

- (i) Mkao wa mviringo

- (ii) Mkao wa mtandazo (wazi)

Irabu zote za mbele hutamkwa midomo ikiwa imetandazwa.

[i] na [e]

Lakini irabu zote za nyuma hutamkwa midomo ikiwa mviringo

[u] na [o]

Kwa kuzingatia vigezo hivyo, tunaweza kueleza vokali au irabu za Kiswahili kama ifuatavyo:

## Irabu za Kiswahili.

Kwenda juu au chini kwa ulimi	Sehemu ya ulimi	Muundo wa midomo
[ i ] – Juu	Mbele	Mtandazo
[ e ] – Kati	Mbele	Mtandazo
[ a ] – Chini	Kati	Mtandazo
[ o ] –Kati	Nyuma	Mviringo
[ u ] – Juu	Nyuma	Mviringo

**Jedwali: 3:4**

### 3.6 Mfuatano wa Sauti katika kuunda Maneno ya Kiswahili (fonotaktiki)

Kila lugha ina kanuni inazofuata katika kuzipanga sauti za irabu na konsonanti ili kuunda maneno ya lugha hiyo (Mbaabu, 1985:10). Lugha ya Kiswahili, sawa na lugha zingine za Kibantu hutumia mwambatano wa konsonanti na irabu kwa wingi sana katika kuunda maneno. Kwa hivyo silabi nyingi za maneno mengi ya Kiswahili ni mwambatano huo wa konsonanti na irabu (kv). Neno laweza kuanzia ama kwa konsonanti au kwa irabu, lakini, kila mara neno lenye asili ya Kibantu ni sharti liishie kwa irabu. Ifuatayo ni mifano michache ya mpangilio wa fonimu kujenga maneno ya Kiswahili.

#### 3.6.1 Irabu

Irabu zote za Kiswahili zinaweza kutokea mwanzo wa neno, mwisho, na katikati ya neno.

##### 3.6.1.1. Mwanzo wa Neno

Maneno ya Kiswahili yanaweza kuwa na mianzo ya irabu. Kwa mfano:

[ a ] – [ andaa ] – andaa - vkvv

[ e ] – [ eleza ] – eleza – vkvkv

[ i ] – [ imba ] – imba - vkv

[ o ] – [ omba ] – omba – vkv

[ u ] – [ utambi ] – utambi – vkvkv



### 3.6.1.2 Mwisho wa Neno

Maneno mengi ya Kiswahili yanaishia na irabu. Kwa mfano:

[a] – [uliza] – vkvkv

[e] – [pete] – kvkv

[i] – [mvuvi] – kkvkv

[o] – [msemu] – kkvkv

[u] – [karibu] – kvkvkv

### 3.6.1.3 Katikati ya Neno

Irabu pia hutokea katikati ya neno ikitanguliwa au kufuatwa na konsonanti. Mfano:

[a] – [tano] – kvkv

[e] – [meno] – kvkv

[i] – [kima] – kvkv

[o] – [boma] – kvkv

[u] – [kuta] – kvkv

### 3.6.1.4 Mwambatano wa Irabu

Irabu mbili, tatu au zaidi zinaweza kupangiliwa katika kujenga maneno ya Kiswahili. Mpangilio huu unaweza kutokea mwanzo, katikati au mwisho wa neno. Data ifuatayo ni dhihirisho la mwambatano wa irabu.

[aa] – [baada] – kvkv

[ai] – [tai] – kvv

[e] – [akae] – kvv

[ua] – [barua] – kvkvv

[oa] – [bao] – kvv

[aua] – [maua] – kvvv

[oea] – [zoea] – kvvv

[uaua] – [kuaua] – kvvvv

[aocua] – [wanaocua] – kvkvvvv

[aoio] – [wanaoiongoza] – kvkvvvvkvkv

### 3.6.2 Konsonanti

Neno la Kiswahili linaweza kuanzia kwa konsonanti ikifuatiwa na irabu au konsonanti nyingine. Konsonanti hutokea pia katikati ya irabu au ikitanguliwa au kufuatwa na konsonanti nyingine.

#### 3.6.2.1 Konsonanti Mwanzo wa Neno

Maneno mengi ya Kiswahili huanzia na konsonanti ikifuatiwa na irabu yoyote. Kwa mfano

[kitabu] – kvkvkv

[nanasi] –kvkvkv

[katikati] – kvkvkvkv

[kula] – kvkv

Konsonanti huweza kufuatwa na konsonanti nyingine mwanzoni mwa neno. Kwa mfano

/mb/ - [mbali] – kvkv

/nd/ – [ndugu] – kvkv

#### 3.6.2.2 Konsonanti katikati ya Irabu

Katika lugha ya Kiswahili, konsonanti inaweza kutokea katikati ya irabu yoyote. Kwa mfano

[ɛ ] – [u ɛ afu] – uchafu – vkkvkv

[ ʒ ] - ʒ aḏabu] – ghadhabu – kkvkkvkv

[t] – [kitabu] – kitabu – kvkvkv

Konsonanti inaweza pia kutokea katikati ya neno lakini ikifuatiwa au kutanguliwa na konsonanti nyingine. Kwa mfano

[rt] – [maʃ arti] – masharti – kvkkvkkv

/mp/ - [atampiga]- atampiga– kvkkvkv

/bd/ - [labda] – labda – kvkkv

### 3.6.2.3 Konsonanti Mwisho wa Neno

Katika lugha ya Kiswahili, ni maneno machache, hususan yenye asili ya kigeni, hasa Kiarabu, kuishia na Konsonanti mwisho. Kwa mfano

[m] – [maaium] – maalum – kvkvk

[n] – [ma ealan] – mathalan – kvkkvkvk

[n] – [hususan] – hususan – kvkvkvk

### 3.6.2.4 Mwambatano wa Konsonanti

Konsonanti za msingi zinaweza kuambatana na kuunda sauti moja; kwa mfano, [m] inaweza kufuatwa na fonimu [b] na kujenga sauti moja [mb]. Fonimu za aina hii ni nyingi katika Kiswahili na zinaambatana kwa utaratibu maalum, nazo zipo za aina mbili: mwambatano wa fonimu mbili na mwambatano wa fonimu tatu.

#### (a) Mwambatano wa Fonimu Mbili (kk)

Mwambatano huu ni wa aina tatu:

- (i) Fonimu za aina ya nazali kama vile [m] [n] huweza kufuatwa na fonimu za aina ya vipasuo vyenye mghuno kama vile [ b ] [d] [g] [j]. Utaratibu wa kuambatana
- (ii) Unafuata kanuni ya mahali pa kutamkia: sauti zinazoambatana hutamkwa mahali pamoja ili kujenga sauti au fonimu zifuatazo

m + b – [mb̄] – [mbili] – kvkv  
– [mbuzi] – kvkv

[amba] – kvkkv

n + d – [nd̄] – [ndazi] – kvkv  
– [ndimi] – kvkv  
– [ndovu] – kvkv

n + j – [nj̄] – [njama] – kvkv  
– [njiwa] – kvkzv  
– [njugu] – njungu- kvkv

n + ġ - [nġ] - [nġao] – ngao- kvv  
 - [nġuvu] – nguvu- kvkv  
 - [munġu] – mungu- kvkv

(iii) Fonimu [j] huweza kutanguliwa na konsonanti [p], [f] na [v] kujenga miolongo wa konsonanti hizi:

p + j - [pj] - [upja] – upya - vkk/2v  
 f + j - [fj] - [ɸifja] – jitya – kvkk/2v  
 v + j - [vj] - [vjatu] – vyatu – kk/2vkv  
 v + j - [vj] - [vjom̄bo] – vyombo – kk/2kv  
 f + j - [fj] - [fjeka] – fyeka – kk/2vkv

(iv) Fonimu [w] huweza kutanguliwa na fonimu zote za kiswahili isipokuwa [v] [e]

[ð] [ʒ]

[h] [j] kujenga fonimu ambatano zifuatazo.

P + w - [pw] - [pwani] – pwani - kk/2kv  
 - [pwaja] – pwaya - kk/2vkv  
 g + w - [gw] - [gwaride] – gwaride- kk/2vkvkv  
 - [gwanda] – gwanda- kk/2vkv  
 f + w - [fw] - [ɸufwa] – shufwa- kvk/2v  
 ŋ + w - [w] - [ŋwafua] – ng'wafua – kk/2vkvv  
 ʃ + w - [w] - [nywele] – nywele – kk/2vkv  
 b + w - [bw] - [bwana] – bwana - kk/2vkv  
 t + w - [tw] - [kutwa] – kutwa - kvkk/2v  
 d + w - [dw] - [tendwa] – tendwa - kvk/2v  
 k + w - [kw] - [kwetu] – kwetu - k/2vkv  
 s + w - [sw] - [swali] –swali - kk/2vkv  
 z + w - [zw] - [kazwa] – kazwa - kvkk/2v  
 l + w - [lw] - [kulwa] – kulwa - kvkk/2v  
 m + w - [mw] - [mwalimu] – mwalimu - k/2vkvkv

### 3.6.2.5. Mpangilio wa Konsonanti ya Nazali [m]

Konsonanti zote za Kiswahili zinaweza kutanguliwa na fonimu [m] mwanzo au katikati mwa neno. Lakini katika neno linaloundwa, fonimu [m] inakuwa silabi

- [mp] – [mpaka]-mpaka – kkvkv  
[alimpa]-alimpa– vkvkkv  
[walimtukana]-walimtukana – kvkvkkvkvkv
- [mb] – [alimbaka]-alimbaka – vkvkkvkv  
[mbebe]-mbebe– kkvkv
- [mt] – [mtama]-mtama– kkvkv  
[mtulivu]-mtulivu – kkvkvkv
- [md] – [atamdunda]-atamdunda – vkvkkvkvkv  
[mdaku]-mdaku – kkvkv
- [mč] | – [mčana]-mchana –kkkvkv  
[mčiča] | -mchicha – kkkvkvkv
- [mʃ] | – [mʃukuu]-mʃukuu – kkvkvv  
[tumʃuze]-tumʃuze – kvkvkvkv
- [mk] – [mkuki] – mkuki - kkvkv
- [mwanamke] – mwanamke- kkvkvkvkv
- [mg] – [mgumu] – mgumu - kkvkv
- [mɡ] – [usimɡombeze] – usimɡombeze - vkvkkvkvkvkv
- [mf] – [mfano] –mfano - kkvkv
- [mv] – [mvulana] – mvulana - kkvkvkv
- [mɛ] – [tamɛilia] – tamthilia – kvkkkvkvkv
- [ms] – [hamsini] – hamsini - kvkvkvkv
- [mz] – [mzembe] – mzembe - kkvkvkv
- [mʃ] | – [mʃale] -mshale– kkkvkv
- [ml] – [mlevi] – mlevi - kkvkv

[mr]	- [mrama] – mrama - kkvkv
[mn]	- [mnene] – mnene - kkvkv
[mh]	- [mhuni] – mhuni- kkvkv
[mɲ]	- [mɲaɲaɲi] – mnyang'anyi – kkkvkvkv
[mm]	- [umma] – umma - vkv
[mj]	- [kimja] – kimya –kvkv

### 3.6.2.6 Mpangilio wa Konsonanti Nazali [n]

Katika Kiswahili Konsonanti Nazali [n] inaweza kufuatwa na Konsonanti zifuatazo: [t] [ç] [s] [z] [r] [n], kama katika maneno yafuatayo:

[nt]	- [nta] – nta – kv
[nç]	- [nçi]
[ns]	- [jinsi] – jinsi - kvkv
[nz]	- [nzige] nzige - kkvkv
[nn]	- [nne] – nne - kv
[ŋg]	- [ŋguvu] – nguvu – kvkv

### 3.6.2.7 Mpangilio wa Konsonanti zisizo za Nazali

Katika lugha ya Kiswahili mpangilio ufuatao ni wa kawaida hasa kwa maneno yenye asili ya kigeni:

[bd]	- [labda] – kvkv
[kt]	- [maktaba] – kvkvkv
[ɟ]	- [dalji] – kvkv
[sk]	- [skuli] – kvkv
[lt]	- [sultani] – kvkvkv
[ft]	- [mufti] – kvkv
[rt]	- [maʃarti] – kvkvkv
[tl]	- [matlai] – kvkvvv
[dr]	- [nadra] – kvkv
[fr]	- [tafrija] – kvkvkv
[ht]	- [muhtasari] – kvkvkvkv
[ks]	- [nuksi] – kvkv

- [rs] – [fursa] – kvkkv
- [lf] – [elfu] – vkkv
- [lh] – [alhamisi] – vkkvkvkv
- [st] – [stadi] – kkvkv
- [ʃt] – [maʃtaka] – kvkkkvkv
- [skr] – [skrubu] – kkkvkv
- [bl] – [blanketi] – kvkkkvkv
- [mst] – [mstari] – kkkvkv

Jedwali lifuatalo limetoa mfuatano wa sauti katika kuunda maneno ya Kiswahili. Sauti ambazo zimepangwa kwenda chini ndizo zinatangulia katika mfuatano kisha zile za juu zinafuata.

**Mfuatano wa Sauti za konsonanti katika Kuunda Maneno ya Kiswahili**

	p	t	d	k	g	f	v	s	z	ʃ	č	ʒ	n	ɲ	ŋ	l	r	w	j
p	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	+	+	+
b	-	+	+	-	-	-	-	-	-	+	-	+	-	-	-	+	+	+	+
t	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	+	+	-
d	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	+	-
k	-	+	-	-	-	+	-	+	-	-	-	-	-	-	-	+	+	+	-
g	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	+	+	-
r	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
f	-	+	-	-	-	-	-	+	-	-	-	-	-	-	-	+	+	-	+
v	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+
o	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+
ö	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
s	+	+	-	+	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	+	+	-
z	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-
ʃ	-	+	-	-	+	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-	-	-
h	-	-	+	-	-	-	-	-	+	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
č	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-
ʒ	-	-	+	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-
m	+	+	+	+	+	+	+	+	+	+	+	+	+	+	+	+	+	+	+
n	-	+	+	-	-	-	+	+	+	+	+	+	+	-	-	-	-	+	-
ɲ	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-
ŋ	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
l	-	+	+	-	+	+	-	+	-	+	-	-	-	-	-	-	-	+	-
r	-	+	+	+	+	-	+	+	+	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-
w	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
j	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-

**Jedwali la 3:5**

**Asili: Musau (1993 : 53)**

Nimeikubali orodha ya Musau (1993:53) ya mfuatano wa konsonanti za Kiswahili ila tu nimeongezea mifuatano fulani ya konsonanti ambayo hakutaja katika orodha yake au chati hii.



### 3.7 Silabi katika Kiswahili


Silabi ni tamko linalojengwa na fonimu moja au zaidi (Aswani, 2001:75). Silabi ni sauti inayoweza kutamkika. Muundo wa silabi ya lugha yoyote ile hutawaliwa na muundo wa kifonolojia wa lugha hiyo. Uwezo wa kutambua mfuatano unaoruhusiwa na lugha fulani ni sehemu ya umilisi wa kifonolojia wa lugha hiyo. Silabi kwa hivyo, ni tamko la kimsingi kabisa katika neno inayoweza kutamkwa mara moja na kwa pamoja kama fungu moja la sauti. Maneno ya lugha yeyote kikiwemo Kiswahili hutamkwa kwa kufuata silabi. Kwa mintarafu hii, tutaeleza silabi kama tamko kamili katika neno, ambalo laweza kuwa ni Konsonanti pekee, vokali tu, konsonanti na vokali au konsonanti zaidi ya moja.

#### 3.7.1 Silabi iliyoungwa kwa Irabu/Vokali Pekee [i]

Irabu zote za Kiswahili Sanifu ni silabi katika mazingira yafuatayo:

##### a) Mwanzo wa neno:


- oa - [o \$ a] - v \$ v  
 ombi - [ om̄bi] - [ o\$ m̄bi] - v\$kv kkv  
 anacheza - [a \$ na \$ če \$ za]- v \$ kv \$ kv \$ kv  
 adabu - [a \$ da \$ bu] - v\$kv\$kv.



b) Mwisho wa maneno, ambapo irabu au vokali hiyo ya mwisho imetanguliwa na irabu nyingine. Data ifuatayo ni dhihirisho la silabi ya aina hiyo.


- Chezea - [č e \$ ze \$ a] - kv \$ kv v

Pigilia - [pi \$ gi \$ li \$ a] - kv \$ kv\$ kv \$ v  
 Pitishia - [pi \$ ti \$ ŋi \$ a] - kv \$ kv \$ kv \$ v



c) Silabi ya vokali tu, katika Kiswahili hutokea kama kuna mwandamano wa vokali mbili bila konsonanti. Data ifuatayo ni dhihirisho la silabi ya aina hiyo:

Maana - [ma \$ a \$ na] - [kv \$ v \$ kv]  
 Pooza - [po \$ o \$ za] - [kv \$ v\$ kv]  
 Laana - [la\$ a \$ na] - [kv \$ v \$ kv]  
 Maadam - [ma \$ a \$ da \$ m] - [kv \$ v \$ kv\$ k]  
 Maasi - [ma \$a \$si] - [kv \$ k \$ kv]  
 Kuoana - [ku \$o\$a\$na] - kv \$ v \$ v \$ kv]




### 3.7.2 Silabi ya Konsonanti na Vokali (kv)

Silabi ya aina hii huundwa wakati fonimu - konsonanti inapoungana na fonimu - irabu ili kufanyiza tamko au silabi moja. Konsonanti moja hufuatwa na vokali na kuzua mwandamano [kv]. Kama inavyoelezwa na data ifuatayo:

- [k] + [v]            -- [ku \$ la] – kula - kv\$kv  
                           -- [pa \$ ta] – pata – kv\$kv  
                           -- [ta \$ fu \$ ta] - tafuta - kv\$kv\$kv

Neno - tafuta



### 3.7.3 Konsonanti Ambatano ikifuatwa na Irabu [kkv]

Silabi hii hutokea pale ambapo kuna mwandamano wa konsonanti zaidi ya moja zikifuatwa na vokali. Kwanza, kunaweza kuwa vokali, pale ambapo tunahusisha baadhi ya nasali na sauti nyingine za mghuno.

Mifano:

- Mbuzi                    -- [mbu\$zi] – k<sup>1</sup>/<sub>2</sub>v\$kv  
 Mjomba                 -- [m̄jo\$mb̄ba] – k\$kv\$kv

Pia tunaweza kuwa na mfuatano wa nasali na nusu vokali kama ifuatavyo: [k<sup>1</sup>/<sub>2</sub> kv]


Kunywa – [ku\$ŋ wa] – kv\$ k<sup>1</sup>/<sub>2</sub> v

Wakati mwingine vipasuo [p] [t] [k] [b], vikwaruzo [s] na kitambaza [l] huja kabla ya [k<sup>1</sup>/<sub>2</sub>].

mifano:

- Pwagu - [pwa\$gu] - [kk<sup>1/2</sup> v\$kv]
- Pwani - [pwa\$ni] - [kk<sup>1/2</sup> v\$kv]
- patwa - [pa\$twā] - [kv\$ k<sup>1/2</sup> v]
- swali - [swa\$li] - [kk<sup>1/2</sup> vkv]
- kubwa - [ku\$bwa] - [kv\$kk<sup>1/2</sup> v]

mjomba




### 3.7.4 Silabi iliyoundwa kwa Konsonanti Pekee [k]

Kiswahili vilevile kinazo silabi chache ambazo huishia na konsonanti; yaani silabi funge (Mgullu 1999:77). Konsonanti hujisimamia kama silabi bila msaada wa irabu Silabi funge hupatikana sana katika maneno mkopo hasa, zikipatikana katikati mwa neno.

#### (i) Silabi iliyoundwa kwa konsonanti endelevi – ng’ongo [k]

- [m] - [m \$ vu \$ vi] - mvuvi - k \$ kv\$ kv  
[m \$ si \$ča\$na] - msichana - k \$ kv\$ kkv\$ kv
- [n] - [n \$ zi] - nzi - k \$ kv  
[n \$ ta] - nta - k \$ kv  
[n \$ je] - nje - k \$ kv



(ii) Silabi iliyoungwa kama konsonanti imefuatwa na konsonanti nyingine hasa katika maneno yenye asili ya Kigeni .

mifano:

labda – [lab\$ da] –kvk\$kv

alhamisi - [al\$ha\$mi\$si] – vk\$kv\$kv\$kv

daftari [daf\$ta\$ri] – kvk\$kv\$kv

ilhali – [il\$ha\$li] – vk\$kv\$kv

### 3.8 Mkazo

Mkazo ni kipengele muhimu sana katika matamshi ya lugha ya Kiswahili. Sifa hii hushughulikia jinsi watu wanavyotamka maneno kwa nguvu zaidi katika sehemu fulani fulani. Kuna aina mbili za mikazo: mkazo wa sentensi na mkazo wa neno. Kazi hii imejikita katika aina ya pili (mikazo katika neno).

Mikazo huwekwa katika silabi fulani kwenye neno. Kila lugha huwa na utaratibu wake wa kuweka mikazo katika maneno ya lugha hiyo. Katika lugha zingine mahali pa mikazo hapabadiliki (mikazo - fungwa) lakini katika lugha zingine mahali pa mikazo hubadilika badilika. Mikazo katika lugha ya Kiswahili huwekwa kwenye silabi ya pili kutoka ile ya mwisho katika neno. Ni muhimu kuelewa kuwa yapo maneno machache ambayo yamekopwa kutoka lugha zingine ambayo yanawekwa mkazo mahali pengine (Mgullu, 1999: 78) , (Vitale 1985: 106) na Polome (1967:50).

[wakulima]

[mf̄oto]

[p̄iga]

[j̄iko]

Haya ni baadhi ya maneno ambayo yanawekwa mkazo mahali pengine. Maneno haya yamekopwa kutoka kwa lugha ya Kiarabu.

[k̄adiri] - [kadiri]

[ka ð̄ alika] - [ka ð̄ alika]

[n̄usura] - [nusura]

[m̄uʃkili] - [muʃkili]

[h̄eʃima] - [heʃima]

[bar̄abara] - [bara bara]

### 3.9 Mifanyiko ya Kifonolojia inayoiathiri Silabi ya Kiswahili.

Kuna sheria kadhaa za kifonolojia ambazo huathiri silabi. Tungependa sasa kuzichunguza baadhi ya taratibu na kanuni za kifonolojia na jinsi zinavyoihusisha silabi na vijenzi vyake

#### 3.9.1 Udondoshaji

Udondoshaji ni hali ya kundondosha kipashio cha neno; irabu, konsonati au silabi. Vipashio hivi vya maneno hutoweka kabisa katika mazingira maalum ya kifonolojia. Udondoshaji hutokea kwa sauti ambazo ni hafifu.

##### 3.9.1.1 Udondoshaji wa Irabu

Irabu hudondoshwa zaidi pale ambapo irabu mbili au zaidi zinazofanana huwa zimefuatana. Sababu moja kubwa ya kudondoshwa kwa irabu ni kusahilisha matamshi. Kwa mfano:-

[wa + alimu] - [walimu]

[wa + anafunzi] - [wanafunzi]

[mu + tu] - [mtu]

[muhindi]            - [mhindi]  
 [ha + a + tak + i]    - [hataki]  
 [ha + a + ku + fu + a] - [hakufua]  
 [wa + em̄bam̄ba]    - [wem̄bam̄ba]

### 3.9.1.2 Udondoshaji wa Konsonanti

Konsonanti hudondoshwa wakati neno fulani katika hali ya wingi huendelezwa katika hali ya umoja. Kwa mfano:

[wana ě eza] > [ana ě eza]  
 [wanapika] > [anapika]  
 [tunalima] > [unalima]

### 3.9.2 Uchopekaji

Ni utaratibu wa kifonolojia unaoathiri muundo wa silabi kwa kuingizwa au kutia konsonanti au irabu. Uchopekaji, kwa hivyo, ni mfanyiko wa kifonolojia ambapo sauti huongezwa kwa zile zilizoko katika neno. Katika lugha ya Kiswahili, pindi pakitokea mkururo wa vokali, sauti huweza kuchopekwa ili kuuvunja mkururo huo, hasa katika mnyambuliko wa baadhi ya vitenzi.

Uchopekaji pia hutokea wakati maneno ya mkopo hupachikwa irabu ikiwa neno hilo linaishia konsonanti.

mifano

[maalum]            - [maalumu]  
 [kitab]              - [kitabu]

### 3.10 Sauti za Dholuo

Dholuo ni mojawapo ya lugha ya kinailoti ambayo inazungumzwa katika mkoa wa Nyanza, magharibi mwa Kenya kwenye ufuo wa ziwa Victoria (Omondi, 1982:1). Lugha yoyote ile huwa na mpangilio maalum wa sauti, ambao huitwa mfumo sauti. Sawa na lugha nyingine za Kiafrika, Dholuo hudhihirisha mshabaha mkubwa kati ya lugha andishi na ile ya kuzungumza. Sauti zote za Dholuo zimeorodheshwa katika makundi mawili, ambayo ni konsonanti na vokali. Kwa vile kazi hii imejikita katika

athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili, data kuhusu mifumo sauti ya Dholuo ambayo ni lugha ya kwanza imetusaidia kubashiri sehemu ambazo huweza kuwatatiza wazungumzaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

### 3.10.1 Konsonanti za Dholuo

Lugha ya Dholuo ina fonimu ishirini na tano za Konsonanti (Omondi: 1982 : 19, Okombo 1982:19 na Adhiambo Oduol 1990 :48). Sauti hizi za Konsonanti zimeelezwa kwa kuzingatia sifa tatu kuu: ambazo ni upumuaji, mahali pa kutamkia na jinsi ya kutamka

#### 3.10.1.1 Hali ya Glota

Kama tulivyotaja hapo awali, glota inaweza kufunguka na inapofunguka, pumzi husukumwa kupitia mkondohewa uliobanwa. Sauti zote ambazo hutolewa wakati ambapo glota imefunguka, huitwa sauti hafifu (sighuna) kwa sababu hakuna mtikisiko wa nyuzi za sauti. Ikiwa nyuzi za sauti zimeshikana pamoja, glota hufungika na pumzi kutoka mapafuni husababisha mrindimo wa nyuzi za sauti, kisha hutoa sauti zenye mghuno. Katika lugha ya Dholuo sauti ambazo sighuna ni:

[p][t][ɕ][k][f][θ][s][h]

Nazo sauti za konsonanti ambazo ni ghuna ni hizi:

[b][mb][d][ɟ][g][ð]

[m][n][ŋ][ɲ][l][r][w][j][nɟ][n̂d][n̂ð][n̂g]

Data ifuatayo imetoa mwangaza kwa maelezo hayo.



**Jinsi ya kutamka konsonanti za Dholuo (sighuna- ghuna)**

Sauti hafifu (Sighuna)	Sauti ghuna
[p] - [p u rɔ] - puro - kulima	[b] - [b u ra] - bura -kesi
[t] - [tadɔ] - tado - paa la nyumba	[mb̄]- [m̄baka] - gumzo
[ɕ] - [ɕ ako] - chako - anza	[d] - [dala] - dala - nyumbani
[k] - [kanɔ] - kano - weka	[ʃ] - [ʃ uɔk] - juok - uchawi
[f] - [f u lɔ] - fulo - sema	[g] - [gɔmbɔ] - gombo - tamaa
[θ]- [θ unɔ]- thuno - titi	[ð ] - [ð anɔ] - dhano - binadamu
[s] - [s u ja] - suya - harufu	[m] - [ma ðɔ ] - madho - kunywa
[h] - [hawi] - hawi - Bahati	[n] - [nenɔ] - kuona
	[ŋ ] - [ŋ akɔ] - nyako - msichana
	[ŋ ] - [ŋ ato] - ngato - mtu
	[l] - [law] - nguo
	[r] - [riekɔ] - rieko - akili
	[w] - [we č ε] - weche - mambo
	[j] - [jwe č ] - ywech - ufagio
	[nj] - [ nɲaga] - njaga - bangi
	[ n ð ] - [n ð an ð u] - ladha
	[nd̄] - [nd̄ara] - njia
	[n̄ g] - [n̄ g ima] - maisha

**Jedwali la 3:6**

**3.10.1.2 Mahali pa Kutamkia**

Kama tulivyotaja hapo awali, (tazama 3.4.3.2) mahali ambapo pumzi huzuiliwa, wakati sauti hutamkwa huitwa mahali pa kutamkia. Mahali pa kutamkia ni muhimu sana katika uelezaji wa sauti, hasa konsonanti.

Data ifuatayo ni kielezo kuhusu konsonanti za Dholuo na mahali zinapotamkwa.

## Mahali pa kutamkia Konsonanti za Dholuo

Sehemu	Fonimu	Neno/Maana
Midomo	[p]	[puko] – puko-mwaga
	[b]	[baṅdo] –bando – mahindi
	[m]	[mɔs] –mos- pole
	[ṁb]	[ɔṁbi č ]-ombich
Mdomo wa chini na meno ya juu	[f]	[fweɣ] – fweny – ufunuo
Meno	[θ]	[θum] –thum- mziki
	[ð]	[ðɔk] – dhok – ng'ombe [nð anð u] – ndhandhu - ladha
Ufizi	[t]	[tem] – tem – jaribu
	[d]	[d u tɔ] – duto – yote
	[s]	[se čε ] – seche – wakati
	[l]	[law] – law – nguo
	[r]	[remḅ] – remḅ – damu
	[n]	[nera] – nera – mjomba
	[ṁd]	[ṁdawa] – ndawa - sigara
Kaakaa laini	[k]	[kɔŋɔ] – kong'o – pombe
	[g]	[gɔṁbɔ] – gombo – tamani
	[ṅ]	[ṅgima] – ngima - maisha
	[ŋ]	[ŋwɔnɔ] – ng'wono - huruma
Kaakaa gumu	[t]	[tʋ θ] -chuth – kabisa
	[ʃ]	[ʃa rɔ]- jaro – dharau
	[ṁʃ]	[ṁʃaga] – njaga - bangi
	[ʃ]	[ʃaθi ] - nyathi – mtoto [jweɣɔ]-yweyo – pumuzika
Midomo na kaakaa laini	[ w ]	[weče] - maneno
Koromeo	[ h ]	[hera] – mapenzi

Jedwali la 3:7

### Maelezo:

- i. **Midomo miwili:** - Sauti [ p ], [ b ], [mb] na [ m ] hutamkwa kwa kukutanisha midomo yote miwili.
- ii. **Mdomo na meno.** Fonimu [ f ] hutamkwa wakati mdomo wa chini umegusa meno ya juu.
- iii. **Meno:** wakati wa kuzitamka fonimu [ θ ] [ð] na [nð], ulimi huwekwa katikati ya meno ya juu na ya chini na hususan huwa umeyagusa meno ya juu.
- iv. **Ufizi:** Wakati wa kuzitamka foni [ t ] [ d ] [nd] [ s ], [ n ], [ r ] na [ l ], ncha ya ulimi huwa imegusa ufizi.
- v. **Kaaka laini:** Fonimu [ k ] [g] [ng] na [ŋ] hutamkwa wakati sehemu ya kati au nyuma ya ulimi huinuliwa hadi kukaribia au kugusa sehemu hiyo laini lililo nyuma ya kinywa.
- vi. **Kaaka gumu:** wakati wa kuzitamka foni [č], [ʃ] [nʃ] [ɲ] na [j] sehemu ya kati ya ulimi huinuliwa na kugusa kaaka gumu.
- vii. **Midomo na kaaka laini:** wakati wa kutamka foni [ w ] hewa hubanwa kwa kuiviringisha midomo yote miwili.
- viii. **Koromeo:** foni [ h ] hutamkwa kama koromeo imebanwa kiasi fulani ili kuruhusu sauti kutoka.

### 3.10.1.3 Jinsi ya Kutamka

#### 3.10.1.3.1 Vipasuo:

Lugha ya Dholuo ina vipasuo kumi na viwili. Hivi vipasuo ni sauti zinazotokea wakati mkondo wa hewa unapozuiliwa au kukwamizwa kinywani kwa muda: Ukatizwaji huu ni wa muda mfupi tu. Katika Dholuo, sauti hizi ni. [ p ] [ b ] [mb] [ t ] [ d ] [č] [ʃ] [k] [g] [nd] [ŋ] [ng]. Data ifuatayo ni kilelezo cha maelezo hayo.

- [p] – [pap] – pap – uwanja  
[b] – [bura] – bura – kesi  
[mb] – [mbaka] – mbaka – gumzo

- [t] – [tedɔ] – tedo – upishi  
 [d] – [dum]– dum – kuruka  
 [č] – [č ak] – chak – maziwa  
 [ʈ] – [ʈuok ] – juok – uchawi  
 [k] – [kwan ] – kwano – hesabu  
 [g] – [gweno] – kuku  
 [nd̄] – [nd̄iga] - ndiga – baiskeli  
 [n̄] – [n̄aga] – njaga – bangi  
 [ŋg] – [ŋgudi] – ngudi – shingo

### 3.10.3.2 Vikwamizwa:

Lugha ya Dholuo ina vikwamizo vitano. Sauti za vikwamizo hutamkwa wakati mkondo hewa unapitishwa kwenye bomba la sauti, ambapo ala za matamshi zinagusana na kuacha mwanya mdogo. Katika Dholuo, sauti hizi ni [ f ] [ θ ] [ ð ] [ s ] [ h ]. Mifano ya sauti inajitokeza katika maneno yafuatayo:

- [f] – [fulɔ] – fulo – shtaki.  
 [θ] - [ θ u m]- thum – kinanda  
 [s] – [s u ja] – suya – harufu  
 [h] – [huso ]– huso – kunywa

### 3.10.1.3.3 Sauti za Nazali:

Kuna nazali nne katika lugha ya Dholuo. Sauti za nazali hutamkwa wakati ambapo baadhi ya hewa hupitia puani. Katika Dholuo, hizi ni sauti [m n,ŋ]. Data ifuatayo imetoa mwangaza kwa maelezo hayo.

- [m] – [mo n] – mon – wanawake  
 [n ] – [nindɔ] – nindo – usingizi  
 [ŋ] – [ŋ iri ] – nyiri – wasichana  
 [ŋ ] – [ŋ aŋ ] – ng'ang' – kujigamba

### 3.10.1.3.4 Vitambaza

Sauti hizi hutamkwa ncha ya ulimi ikigusishwa ufizi, huku baadhi ya hewa ikiachiliwa itoke kwenye pande za ulimi. Vitambaza katika Dholuo ni [ l ] kama kinavyojitokeza katika maneno haya yafuatayo:

- [ l ] – [l u m]- lum- nyasi.
- [law] - law - nguo.

### 3.10.1.3.5 Vimadende

Hutamkwa wakati ncha ya ulimi ikiwa imegusa ufizi lakini kutokana na nguvu ya hewa inayopita kati ya ncha hiyo na ufizi, ncha ya ulimi hupigapiga kwa harakaharaka kwenye ufizi. Katika lugha ya Dholuo, kuna kimadende kimoja tu, nacho ni [r]. Sauti hii hutokea katika maneno kama:

- [r] - [rem] - remo – damu
- [riŋ] - ring'o – nyama

### 3.10.3.6 Viyeyusho

Katika kutamka sauti za viyeyusho ,mkondo hewa hauzuiliwi mahali popote. Sawa na Kiswahili, Dholuo ina viyeyusho viwili ambavyo ni [w] na [ j ]. Sauti hizi hutokea katika maneno kama ifuatayo:

- [w] – [we ɕ e] – weche – mambo
- [wel] – welo - wageni
- [w θ] – wuoth- safari
- [ j ] - wʌjʌ - waya - shangazi

Chati ifuatayo ni kielezo cha vitamkwa vya Dholuo ambavyo vimeelezwa kwa vigezo vya mkao wa Glota, kutamkia na jinsi ya kutamkia. Chati hii imekopwa kutokana na Okombo (1982)

## Konsonanti za Dholuo

Namna kutamka	ya	Midomo	Midomo meno	Meno	Ufizi	Kaakaa gumu	Kaakaa laini	koromeo
Vipasuo		p b mb		n ð	t d, nd	č f n̄f	k g ng	
Vikwamizo			f	θ, ð	s		ŋ	h
Nazali		m			n			
Vitambaza					l			
Vimadende					r			
Viyesho		w				j		

Jedwali la 3:8 Asili (Okombo 1982 : 19)

Kutokana na chati hiyo, tunaona kuwa Dholuo ina sauti ishirini na tano (25) za konsonanti, ambazo hudhihirika katika kielelezo cha (Okombo, 1982) kama ifuatayo ♣

### Unukuzi wa sauti na maneno

Kiotografia	Unukuzi sauti na maneno		Neno kimaandishi	Tafsiri kwa Kiswahili
p	/p/	[pap]	pap	Uwanja
b	/b/	[buk]	buk	Kitabu
w	/w/	[mo]	mo	mafuta
f	/f/	[fulu]	fulu	Samaki
th	/θ/	[θum]	thum	Kinanda
dh	/ð/	[ðako]	dhako	mke
t	/t/	[tado]	tado	tado
d	/d/	[dum]	dum	kuruka
r	/r/	[rao]	rao	kiboko
l	/l/	[lum]	lum	nyasi
s	/s/	[san]	san	sahani
n	/n/	[nam]	nam	ziwa
ch	/ç/	[çak]	chak	maziwa
j	/ʃ/	[ʃowi]	jowi	kifaru
y	/j/	[jamo]	yamo	upepo
ny	/ɲ/	[ɲako]	nyako	msichana
k	/k/	[kom]	kom	kiti
g	/g/	[guok]	guok	mbwa
ng'	/ŋ/	[ŋato]	ng'ato	mtu
h	/h/	[hawi]	hai	bahati
mb	/m̄b/	[m̄baka]	mbaka	gumzo
ndh	/ð/	[nð anð u]	ndhandhu	utamu
nd	/n̄d/	[n̄diga]	ndiga	baiskeli
nj	/nʃ/	[nʃaga]	njaga	bangi
ng	/n̄g/	[n̄gudi]	ngudi	shingo

Jedwali la 3:9

### 3.11 Vokali za Dholuo

Kama lugha nyinginezo za Nailotiki, Dholuo ina irabu kumi (Omondi, 1982:11, Okombo, 1982:19). Irabu hizo ni: [ a ] [ e ] [ i ] [ o ] [ u ] [ʌ] [ɛ] [ɪ] [ɔ] [ʊ]. Kwa mujibu wa wataalam hawa wawili, lugha ya Dholuo ina irabu fupi na irabu ndefu. Tunakubaliana na maoni yao kuhusu idadi au orodha ya irabu hizo.

Kuna vigezo vitatu muhimu vinavyotumiwa na wanaisimu katika kuzieleza irabu za lugha yoyote ile. Vigezo hivi ni: sehemu ya ulimi inayotumika katika kuitamkia sauti hiyo ya irabu; hali ya mwinuko wa alasogezi ulimi, ambayo ndiyo inayohusika katika kutamkia sauti husika ya irabu, na tatu ni hali ya midomo wakati aina fulani ya irabu inapotamkwa.

#### 3.11.1 Irabu Fupi

Irabu fupi za lugha ya Dholuo ni [a] [e] [i] [o] na [u].

/a/ hutamkwa kama katika maneno haya:

[č ak] – chak – maziwa

[par] – par – jamvi

/e/ hutamkwa kama katika maneno haya:

[penʃo] – penjo – swali

[be č o] – becho – nzuri

[beto] – beto – kufyeka

[tedo] – tedo – kupika

/i/ hutamkwa kama katika maneno haya:

[i č] – ich – tumbo

[it] – it sikio

[lit] – lit- uchungu

/o/ hutamkwa kama katika maneno:



/o/ hutamkwa kama katika maneno:

[j <sup>o</sup> tedo]	– mpishi
[onego]	– inafaa
[kumo]	– kuadhibu

/u/ hutamkwa kama katika maneno:

[puko]	– puko – kumwaga
[kuḏo]	– kudho – puliza

### 3.11.2 Irabu Ndefu

Ni irabu ambazo hudhihirika kuwa ndefu zaidi ya zile fupi katika muktadha sawa. Urefu wa irabu za Dholuo hutegemea vigezo mbalimbali vya kimuktadha kama vile mkazo na toni. Zifuatazo ni irabu ndefu za Dholuo:

/ʌ/ kama katika:

[j <sup>ʌ</sup> tedo]	– jatedo – mpishi
[k <sup>ʌ</sup> ɲɔ]	– kanyo – hapo
[tedor <sup>ʌ</sup> ]	– tedora – kujipikia
[kam <sup>ʌ</sup> nɔ]	– kamano –ndivyo

/ɛ/ kama katika:

[pɛ]	– pe
[lɛ]	– le – shoka
[lɛm]	– omba
[ʌlɛm]	– alem – niombe

/I/ kama katika


[lIt]	– lit – majonzi
[mIt]	– mit – utamu
[ɔmit]	– omit –tamu
[Ite]	– ite – sikio lake

/ɔ/	kama katika	
[kanɔ]	– kano – kuweka	
[kumɔ]	– kumo – kuadhibu	
[negɔ]	– nego – kuua	
[dijɔ]	– diyo – finya	
[ɔnegɔ]	– onego – ameva	

/u/	kama katika	
[bul]	– bul –choma	
[bʊ]	– bu- halafu	
[bʊt]	– but – karibu	

Zinaweza kuwasilishwa katika chati kama ifuatavyo:

### Kielezo 3.2 Irabu za Dholuo



(Okombo 1982:19)

### 3.11.3 Mahali pa Kutamkia Irabu

Kama tulivyotaja hapo awali, sehemu tatu hutumiwa kuzitofautisha irabu. Sehemu hizo tatu ni: mbele, kati na nyuma

(i) Sehemu ya mbele ya ulimi inayotamkiwa vitamkwa vifuatavyo:

[ I ]	kama katika [mit]	– mit – tamu
[ e ]	kama katika [tinde]	– tinde – siku hizi
[ ɛ ]	kama katika [l ɛ ]	– le – shoka

(ii) Sehemu ya kati ya ulimi inayotamkiwa vitamkwa kama vile:

[ a ] kama katika [č ak] – chak – maziwa

[ʌ] kama katika [kʌ re] – kare – sawa

(iii) Sehemu ya nyuma ya ulimi inayotamkiwa vitamkwa kama vile:

[ u ] kama katika [puko] – puko – mwaga

[ʊ] kama katika [bʊ] – bu – halafu

[ o ] kama katika [pogo] – pogo – gawa

[ɔ] kama katika [ɔmijɔ] – omiyo - anampatia

### 3.11.4 Mwinuko wa Ulimi

Katika kutamka irabu za Dholuo, aina nne ya miinuko ya ulimi hudhihirika:

(a) Mwinuko wa chini [a] na [ʌ].

Ulimi huwa umeinuka kidogo sana; ulimi huwa umelala chini ya kinywa. Irabu zifuatazo hutamkwa katika hali hii.

[ a ] kama katika [ kari ] – kari – pako

[ʌ] kama katika [ k ʌ ] – ka – hapa

(b) Nusu – chini kama vile [ε] na [ɔ]. Ulimi huwa haupo chini lakini upo karibu sana na chini.

[ε] – [tekrε] - tekre – nguvu zake

[ɔ] – [to ŋɔ] – tong'o – kata

(c) Nusu –juu kama vile [ e ] na [ o ] ulimi huwa karibu na upande wa juu lakini haupo juu kabisa

#### Mifano

[e] – [tedo] - kupika

[o] – [ɟowi] - kifaru.

(d) Juu – vokali za juu hutamkwa wakati ulimi huwa umefikia kilele chake. Ulimi hukaribiana na paa la kinywa. Vokali hizi katika Dholuo ni [ I ] na [ u ]

### Mifano

[ I ] kama katika [pijo] -piyo - haraka  
[ u ] kama katika [puk] -puk -mwaga

### 3.11.5 Mkao wa Midomo

Mkao wa midomo ni jinsi nyingine ya kuelezea fonimu za irabu. Katika hali hii, jinsi mbili za mkao wa midomo hujitokeza nazo ni: mvingo ambao hutokea pale ambapo midomo huvutwa nyuma na kushumburiwa.

Irabu zote za mbele hutamkwa midomo ikiwa imetandazwa.

[ i ] kama katika -[kiro] -kiro- mwaga  
[ e ] kama katika [kej] -keyo-kuvuna  
[ ε ] kama katika [t ε k] -tek- ngumu  
[ a ] kama katika [abiro] -abiro -naja  
[ o ] kama katika [omit] -omit -tamu

lakini irabu zote za nyuma hutamkwa midomo ikiwa mvingo kwa mfano:

[ u ] kama katika-[ubiro]-ubiro-mnakuja  
[ʊ] kama katika [kʊmo]-kuno-kule  
[o] kama katika [puko]-puko-mwaga  
[ɔ] kama katika [kɔmbe]-kombe-viti  
[ʌ] kama katika [ʌmosi]-amosi-nimekusalimu

Kutokana na data hiyo, tunaona kuwa Dholuo ina irabu kumi (10). Kuna vokali ndefu tano katika lugha ya Dholuo ambazo hutegemea vigezo mbalimbali vya kimuktadha kama vile mkazo na toni.

### 3.12 Mfuatano wa Sauti za Dholuo

Lugha hujengwa kwa ishara na sauti, lakini sauti zinazotumika ni za konsonanti na vokali. Lugha huundwa kwa sauti ndogo kabisa ziiwazo fonimu. Fonimu zikisimama pekee huwa hazina maana. Zinaungana kuunda silabi ambapo silabi huunda neno na maneno huunda vifungu ambavyo huunda sentensi. Lugha ya Dholuo sawa na lugha zingine za Kinailotiki hutumia mwambatano wa konsonanti na irabu (KV), Irabu na Konsonanti (VK), Konsonanti pekee (kk) na irabu pekee (vv). Neno laweza kuanzia kwa Konsonanti au Irabu na pia kuishia kwa konsonanti ama kwa irabu. Ifuatayo ni mifano michache ya mpangilio wa fonimu zinazojenga maneno ya Dholuo.

#### 3.12.1 Irabu

Irabu zote za Dholuo zinaweza kutokea mwanzo wa neno, mwisho na katikati ya neno.

##### 3.12.1.1 Mwanzo wa Neno:

Maneno ya Dholuo yanaweza kuwa na mianzo ya irabu. Mdokezo huu unaweza kufafanuliwa kwa data ifuatayo:

- [ a ] kama katika [ a biro ] – abiro – naja
- [ ^ ] kama katika [ ^ mosi ] – amosi – nakusalimu
- [ e ] kama katika – [ entie ] – entie – yuko
- [ ε ] kama katika [ ε n ] – en – ni yeye
- [ i ] kama katika [ it ] – it – sikio
- [ I ] kama katika – [ In ] – in – wewe
- [ o ] kama katika [ obiro ] – obiro – anakuja
- [ ɔ ] kama katika [ ɔ nge ] – onge – hamna
- [ u ] kama katika – [ ubiro ] – ubiro- mnakuja
- [ ʊ ] kama katika [ ʊ bi ] – ubi – mje

##### 3.12.1.2 Mwisho wa Neno

Maneno mengi ya Dholuo yanaweza kuishia kwa irabu kama inavyofafanuliwa na data ifuatayo:

- [ a ] kama katika [ č ira ] –chira - mwiko

- [ʌ] kama katika [tedorʌ] - tedora – kujipikia
- [e] kama katika [pile] – pile – kila siku
- [ɛ] kama katika [lɛ] – le - shoka
- [i] kama katika [gini] – gini – kitu hiki
- [I] kama katika [ɟ Iri] – nyiri - wasichana
- [o] kama katika [kumo] – kumo - adhibu
- [ɔ] kama katika [di jɔ] – diyo - finya
- [u] kama katika [kuɔ] – kudho - miba
- [ʊ] kama katika [kʊnɔ] – kuno – kule/huku

### 3.12.1.3 Katikati ya Neno

Irabu pia hutokea katikati ya neno ikitanguliwa au kufuatwa na konsonanti. Mdokezo huu unaweza kufafanuliwa na deta ifuatayo:

- [a] kama katika [kanɔ] - kano – weka
- [ʌ] kama katika [ɟʌ tede]-jatedo - mpishi
- [e] kama katika [tedo] –tedo- pika
- [ɛ] kama katika [tɛk] -tek - ngumu
- [i] kama katika [lit] -lit- majonzi
- [I] kama katika [d I jɔ] -diyo- finya
- [o] kama katika [tedorʌ] -tedora – tedora - kujipikia
- [ʌ] kama katika [kʌɔ] -kanyo- huko
- [u] kama katika [kumo] -kumo– adhibu
- [ʊ] kama katika [k u ɔ] – kudh – puliza

### 3.12.1.4 Mwambatano wa Irabu

Irabu mbili zinaweza kupangiliwa katika kujenga maneno ya Dholuo. Mpangilio huu kama wa Kiswahili, unaweza kutokea mwanzo, katikati au mwisho wa neno. Data ifuatayo ni dhihirisho la mwambatano wa irabu katika Dholuo.

- [ao] kama katika [ɟaot] -jaot-mke-kvkv
- [oo] kama katika [ɟoote] – joote – wanaotumwa - kvkv
- [uo] kama katika [ɟuok] – juok – uchawi- kvkv

- [ua ] kama katika – [juak] -yuak– kilio - kvvk  
 [ie] kama katika – [gotieno]- gotieno – usiku - kvkvkv  
 [au] kama katika – [ʌuka] – auka – upepo - vkv  
 [ei] kama katika – [eič] – eich – tumboni - vvk  
 [ia] kama katika – [go ðiambo] – godhiambo – jioni - kvkkvkv  
 [au] kama katika [ aučiel] – auchiel – sita - vvkkvkv  
 [ie] kama katika – [parie] – parie – fikiria - kvkv

### 3.12.2.0 Konsonanti

Neno la Dholuo linaweza pia kuanza kwa konsonanti ikifuatwa na irabu au konsonanti nyingine. Konsonanti hutokea katikati ya neno, katikati ya irabu au ikitanguliwa au kufuatwa na konsonanti nyingine.

#### 3.12.2.1 Konsonanti Mwanzo wa Neno

Maneno mengi ya Dholuo huanza kwa konsonanti ikifuatwa na irabu yoyote. Utaratibu huu unaweza kufafanuliwa na data ifuatayo.

- [puro] – puro – kulima – kvkv  
 [baro] – baro – pasua – kvkv  
 [ʃopuro] – jopuro – wakulima – kvkvkv  
 [kano] – kano – weka – kvkv

Konsonanti huweza kufuatwa na nusu irabu mwanzoni mwa neno . Utaratibu huu unaweza kufafanuliwa na data ifuatayo.

- /lw/ – [lwedo] – lwedo – mkono – kk½ vkv  
 /tw/ – [tweng'o] – tweng'o – kushona – kk½vkkv  
 /mw/ – [mwodo] – mwodo – kula – kk½vkv  
 /rw/ – [rwako] – rwako – vaa – kk½vkv

### 3.12.2.2 Konsonanti katikati ya Irabu

Katika lugha ya Dholuo, konsonanti inaweza kutokea katikati mwa irabu yoyote.

- [č] – [oč ido] – ochido – mchawi – vkvkv
- [b] – [osebiro] – osebiro – amekuja – vkvkvkv
- [r] – [čaro] – charo – dharau – kvkv

Konsonanti inaweza pia kutokea katikati ya neno lakini ikifuatwa au kutanguliwa na konsonanti nyingine kama inavyodhihirishwa na data ifuatayo:

- /ms/ – [mosna] – nisalimie – kvkkv
- / ð r/ – [baðruok] – badhruok- kuwa mjanja – kvkkvkv
- /n ð / – [nðanð u] – ndhandhu – ladha/tamu – kvkv

### 3.12.2.3 Konsonanti Mwisho wa Neno

Tofauti na Kiswahili, maneno mengi ya Dholuo huishia au humalizika na konsonanti mwisho. Utaratibu huu unaweza kufafanuliwa na data ifuatayo:

- [t] – [lit] – lit – chungu – kvk
- [č] – [č u] – chung' – simama – kvk
- [m] – [θim] – thim – msitu – kvk
- [n] – [č n] – chan – panga – kvk
- [p] – [pap] – pap – uwanja – kvk
- [r] – [ger] – ger – kali – kvk

### 3.12.2.4 Mwambatano wa Konsonanti

Konsonanti za msingi zinaweza kuambatana na kujenga sauti moja, kama vile [ n ] inaweza kufuatwa na fonimu [ d ] na kujenga sauti moja [nd]. Fonimu za aina hii ni nyingi katika lugha ya Dholuo konsonanti mbili au zaidi zinaweza na huambatana kwa utaratibu maalum,; mwambatano wa fonimu mbili na mwambatano wa fonimu tatu.

(a) **Mwambatano wa fonimu mbili (kk)** – kama katika data ifuatayo

- m+ b – [m̄b] – [m̄baka] – hadithi –kkvkv



n + d - [ndiga] – ndiga – baiskeli – kkvk

n + ʃ - [nʃaga] – njaga – bangi – kkvk

**(b) Fonimu [w] huweza kutanguliwa na fonimu zote za Dholuo na kujenga fonimu ambatano zifuatazo:**

/pw/ - [apwojo] – apwoyo – sungura – vkk½vk

/bw/ - [bwo ðo] – bwodho – kujinasua – kk½vk

/fw/ - [fwolo ] – fwolo – kukohoa- kk½vk

/ðw/ - [rwa ðwa] – rwadhwa – fahali wetu – kk½vk

/tw/ - [twango] – twang'o – kushona – kk½vkk

/dw/ - [dwaro] – dwaro – hitaji – kk½vk

/rw/ - [rwako] – rwako- vaa – kk½kvk

/lw/ - [lwoko] – lwoko – kuosha – kk½vk

/sw/ - [swajo] – swayo – chochea – kk½vk

/nw/ - [nwo ɕ] – nwocho – kurudia – kk½vkk

/čw/ - [čwojo] – chwoyo – choma – kk½vk

/ʃw/ - [ʃwala] – jwala -jwala - kkvk

/jw/ - [jwe č ] – ywech – ufagio – kk½vk

/gw/ - [gweno] – gwen – kuku – kk½vk

/m̄bw/ - [hum̄bwa] – humbwa – sifa zetu – kvkk½v

/n ðw] - [hunðwe] – hundhwe – ndege – kvkk½kv

/n̄ʃw/ - [win̄ʃwa] – winjwa – ndege wetu – kvkk½v

/n̄gw/ - [ran̄gwa] – rangwa – tutafute – kvkk½v

/ŋw/ - [ŋwon o ] – ng'wono – huruma – kk½vk

/n̄dw/ - [wendwa] – wendwa – wageni wetu – kvkk½v

/ɲw/ - [ɲwol] – nywol – kuzaa – kk½vk

/hw/ - [hwano] – anua - kk½vk

**Mwambatano wa fonimu tatu (kkk½)**

Fonimu ambatano mbili [m̄b] [n̄d] [n̄ʃ], [n̄g] [n ð] zinaweza kufuatwa na nusu irabu [w] kujenga fonimu zifuatazo.

m + b + w	- [m̄bw] – [hum̄bwa] – humbwa – sifa zetu-kvkkk½v
n + d + w	- [nd̄w] – [wend̄wa] – wendwa – wageni- wetu-kvkkk½v
n + <b>ɟ</b> + w	- [n̄ɟw] – [win̄ɟwa] – winjwa – ndege wetu-kvkkk½v
n + g + w	- [nḡw] – [ranḡwa] – rangwa – tutafute- kvkkk½v

Konsonanti chache sana za Dholuo zinaweza kufuatwa na nazali [m] mwanzo au katikati ya neno. katika neno linalojengwa kwa fonimu ya nazali [m] huwa silabi. Kuna mifano ya maneno yaliyokopwa ambayo kila mara huchopekwa irabu [i], [u] na [o] ili kuvunja mkururo huo wa konsonanti. Madai haya yanaweza kufafanuliwa na data ifuatayo:

[komno]	– komno – kiti hicho – kvkkv
[kampeñ]	– kampen – kampeni – kvkkvk
[kampani]	– kampani – kampuni – kvkkvkv

(c) **Mpangilio wa konsonanti za nazali [n].**

Katika lugha ya Dholuo konsonanti nazali inaweza kufuatwa na konsonanti zifuatazo: [t],[k],[r],[d],[s]

[nt]	– [antie]	– niko - vkkv
[nk]	– [ankano]	– ankanyo – niko hapo – vkkvkkv
[nr]	– [hanruok]	– hanruok – nkujiweka – kvkkvkv
[nd̄]	– [ohand̄e]	– ohande – faida yake – vkkvkkv
[ns]	– [usna]	– niuzie – vkkv

Jedwali lifuatalo limetoa mfuatano wa sauti za konsonanti katika kuunda maneno ya Dholuo (Musau 1993: ) Sauti ambazo zimepangwa kwenda chini ndizo zinatangulia kisha zile za juu zinafuata. Pia inaonyesha mfuatano wa fonimu konsonanti za lugha ya Dholuo.

**Mfuatano wa sauti za Konsonanti katika kuunda maneno ya Dholuo**

	p	b	t	d	k	g	f	θ	ð	s	ʃ	h	t	m	n	ɲ	ŋ	l	r	w	j		
p	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-	
b	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-
t	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-	-	+	-	-	-	+	-	-
d	-	-	-	-	+	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-	-	-	-	+	+	-	-
k	-	-	+	-	-	+	+	-	-	+	-	-	-	+	-	-	-	+	+	+	+	-	-
g	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	+	+	-	+	-	+	-	-	
f	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-	
θ	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	+	+	-	-	-	-	+	-	
ð	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-	
s	-	-	-	-	+	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-	-	-	-	-	+	-	
ʃ	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-	
h	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-	
t	-	+	-	-	+	-	-	-	-	-	-	-	+	-	-	-	-	-	-	-	+	-	
m	+	+	-	-	+	-	-	-	+	-	-	-	-	-	+	+	-	-	-	-	+	-	
n	-	-	-	-	-	-	+	-	+	+	-	-	+	+	-	+	-	-	-	-	+	-	
ɲ	-	-	-	-	-	+	-	-	-	-	-	-	-	+	+	-	-	-	-	+	+	-	
ŋ	-	-	-	-	+	-	+	-	-	-	-	-	+	-	+	-	-	-	-	-	+	-	
l	+	-	+	-	-	+	+	-	-	-	-	-	-	+	-	+	-	-	-	-	+	-	
r	-	-	-	-	+	+	-	-	-	-	-	-	-	+	+	+	-	-	-	-	+	-	
w	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	
j	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	+	-	

**Jedwali la 3:10 Asili Musau (1993:53)**

**3.13 Silabi Katika Dholuo**

Lugha ya Dholuo ina aina mbili za silabi; silabi funge na silabi huru. Maneno mengi ya Dholuo yana silabi huru na funge kwa vile yanaishia kwa irabu na konsonanti. Katika Dholuo silabi inaweza kuwakilishwa kwa sauti moja mbili au zaidi.


**3.13.1 Silabi za Vokali pekee [v]**

Irabu zote za Dholuo ni silabi katika mazingira yafuatayo.

- (a) Mwanzo wa maneno kama inavyojitokeza katika data ifuatayo:

- /a/ - [a čiemo] – achiemo – a \$ č \$e \$ mo – v \$ kv\$kv\$ kv
- /o/ - [obiro] – obiro - o\$bi\$ro – v\$kv\$kv
- /I/ - [Itijo] – itiyo – I\$ti \$jo – ninafanya kazi v\$kv\$kv
- /Λ/ - [Λbi] - Λ\$bi – nije v\$kv
- /u/ - [utedona] - - utedona – u\$te\$do\$na – mnanipikia v\$kv\$kv\$kv


Silabi za maneno haya yanajitokeza hivi:



Mwisho wa maneno, ambapo irabu au vokali hiyo ya mwisho imetanguliwa na irabu nyingine. Deta ifuatayo ni dhihirisho ya silabi ya aina hiyo:

- /e/ - [nitie] – nitie - napatikana ni\$ti\$e – kv\$kv\$v
- /e/ - [jie] – yie – yi\$e mitumbwi – kv\$v

silabi hizi hujitokeza hivi katika mchoro



(b) Silabi ya vokali tu, katika Dholuo, hutokea kama kuna mwandamano wa vokali mbili bila konsonanti. Data ifuatayo ni dhihirisho la silabi ya aina hiyo.

/oo/ - [joote] – joote – jo\$o\$te – wanaotumwa - kv\$v\$kv


/uo/ - [juok] – ju\$o\$sk – Uchawi - kv\$v\$sk

/au/ - [auka] – auka – a\$u\$ka – Kimbunga - v\$v\$skv

/ao/ - [jaot] – jaot – ja\$o\$st – mke - kv\$v\$sk

/ia/ - [go<sup>ɔ̃</sup>iambo] – godhiambo – jioni go\$<sup>ɔ̃</sup>i\$a\$ambo – kv\$kv\$v\$skv

Mwandamano wa vokali: [go<sup>ɔ̃</sup>iambo]



### 3.13.2 Silabi ya Konsonanti na Irabu (kv).


Aina hii ya silabi hutokea pale ambapo konsonanti moja hufuatwa na vokali, na kuzua mwandamano (KV). Utaratibu huu unaweza kufafanuliwa na data ifuatayo.

tedo – [te\$do] – upishi kv\$kv

kelona – [ke\$lo\$na] – niletee kv\$kv\$kv

jatedo – [j^A\$te\$do] – mpishi kv\$kv\$kv

Silabi hizi hujitokeza hivi katika mchoro [j^A tedo] – jatedo.



### 3.13.3 Silabi ya Konsonanti moja pamoja na nusu Irabu

Silabi hii hutokea pale ambapo kuna mwandamano wa konsonanti moja pamoja na nusu Irabu [w]. Data ifuatayo ni kielelezo cha maelezo hayo.

/pw/ - [apwojo] – apwoyo] – sungura-[a\$pw\$jo] – v\$kk½v\$


/nw/ - [nwo čo] – nwocho –marudio-[nwo\$ č o ] – kk½v\$kv

/ñdw/ - [wendwa] – wendwa –wageni wetu-[we\$ñdw] –kv\$kk½v

/ñjw/ - [winjwa] – winjwa –ndege wetu-[wi\$ñjwa] – kv\$kk½v

/nðw/ - [hun ðwe] – hundhwe –aina ya ndege-[hu\$ñðwe] – kv \$kk½v

Silabi hizi hujitokeza hivi katika mchoro: [wendwa ]



### 3.14 Mkazo

Mkazo kama tulivyodokeza awali ni jinsi watu wanavyotamka maneno kwa nguvu zaidi katika sehemu fulanifulani. Katika lugha ya Dholuo mahali pa mikazo katika maneno hubadilibadilika.

Kulingana na Omondi (1982:21), mkazo katika Dholuo hubakia katika kiini cha silabi cha neno hata baada ya kupachikwa kwa viambishi awali au tamati. Data ifuatayo ni dhihirisho la madai kuwa mahali pa mikazo katika maneno ya Dholuo hubadilikadilika:

[t <sup>é</sup> do]	– kupika
[ʃ <sup>ʌ</sup> t <sup>é</sup> do]	– mpishi
[it <sup>é</sup> do]	– unapika
[iset <sup>é</sup> dona]	– umenipikia?

Lugha ya Dholuo ina matumizi huru ya mikazo. Si lazima mkazo uwekwe mahali maalum kila mara katika lugha hii.

(i) Maneno yafuatayo yanachukua mkazo katika silabi ya pili

[ʃ <sup>ʌ</sup> at <sup>é</sup> do]	– jatedo – mpishi
[i <sup>é</sup> t <sup>é</sup> dona]	– itedona - unapika
[ʃ <sup>ʌ</sup> imat <sup>é</sup> donwa]	– jimatedonwa – wanaotupikia

(ii) Haya mengine nayo yanachukua mkazo katika silabi ya kwanza

[t <sup>é</sup> dnigi]	– tednigi – wapikie
[t <sup>é</sup> dnwa]	– tednwa – tupikie
[t <sup>é</sup> druok]	– tedruok – kujipikia

(iii) Maneno haya yanachukua mkazo katika silabi ya tatu.

[ʃ <sup>ʌ</sup> omat <sup>é</sup> do]	– jomatedo – wapishi
[moset <sup>é</sup> di]	– mosetedi – kimepikwa
[iset <sup>é</sup> dona]	– isetedona - umenipikia

Lugha ya Dholuo, kwa hivyo, haina mahali maalum pa kuwekewa mikazo kwenye maneno. Mahali pa kuweka mkazo katika maneno hubadilikabadilika. Kwa njia hii, lugha ya Dholuo ni tofauti na Kiswahili, ambacho maneno yake huchukua mkazo kwenye silabi ya pili kutoka mwisho.



### 3.15 Udondoshaji

Kama tulivyotaja hapo awali (Tazama 3:9:1) Mfanyiko wa udondoshaji hutokea wakati ambapo kipashio fulani cha neno husika kinatoweka kabisa katika mazingira maalum ya kifonetiki au kifonolojia (Aswani 2001: 98). Udondoshaji, kwa hivyo unahusu irabu, konsonanti na hata silabi.

#### 3.15.1 Kudondoshwa kwa Vokali

Katika Dholuo, vokali hudondoshwa ikiwa neno husika limeendelezwa katika hali ya wingi (Mudhune 1994: 65). Tazama mifano ifuatayo.

Umoja	Wingi	Kiswahili
[gweno] – gweno	[gwen] – gwen	kuku
[wiŋo] – winyo	[wiŋ] – winy	ndege
[gwoŋo] – gwonyo	[gwoŋ] – gwony	upele

Udondoshaji wa vokali pia hutokea wakati maneno fulani katika hali ya wingi huendelezwa katika hali ya umoja (Mudhune 1994:64). Tazama mifano ifuatayo.

Wingi	Umoja	Kiswahili	Wingi
[jawuoji] – yawuoyi	[wuoji] – wuoyi	mvulana	- Wavulana
[agulni] – agulu	[agulu] – agulu	mtungi	- Mitungi
[higni] – higni	[higa] – higa	mwaka	- Miaka
[agwetni] – agwetni	[agwata] – agwata	kata	- Kata zaidi
[ndigni] – ndigni	[ndiga] – ndiga	baiskeli	- baiskeli

#### 3.15.2 Udondoshaji wa konsonati:

Kuna udondoshaji wa konsonanti kama katika maneno yafuatayo:

[maber] > [aber]	- zuri-mzuri
[matin] > [atin]	- dogo- mdogo
[m biro] > [ biro]	- yaja-kuja
[mara č ] > [ara č]	- baya- mbaya
[watijɔ] > [atijɔ]	- kufanya kazi

### 3.15.3 Udondoshaji wa Silabi

Kuna udondoshaji wa silabi kama katika mifano ifuatayo.

[matin] > [tin]	- chache	- ndogo
[maber] > [ber]	- mara	- uzuri
[ɟapuonɟ] > [puonɟ]	- mwalimu	- funzo
[puonɟri] > [puonɟ]	- jifunze	- funza

### 3.16 Uchopekaji

Mfanyiko huu ni moja kati ya njia za kifonolojia ambazo hutumika kudhibiti muundo wa kifonolojia unaopendelewa na lugha husika (tazama schane 1972).

#### 3.16.1 Uchopekaji wa Irabu

Katika mfanyiko huu wa kifonolojia, irabu hupachikwa mwazoni mwa neno pale ambapo haikuwemo awali. Tazama mifano ifuatayo:

[ber] – ber > [aber]	– aber – uzuri-mzuri
[tin] – tin > [atin]	– atin – ndogo-mdogo
[biro] – biro > [ubiro]	– ubiro – kuja
[pek] – pek > [ipek]	– ipek - uzito

#### 3.16.2 Uchopekaji wa Konsonant

Katika mfanyiko huu wa kifonolojia, Konsonanti hupachikwa pale ambapo haikuwepo awali. Tazama mifano ifuatayo:

[atin] > [matin]	– mdogo-ndogo
[aber] > [maber]	– mzuri-nzuri
[abiro] > [wabiro]	– naja-twaja

#### 3.16.3 Uchopekaji wa Silabi

Kuna uchopekeji wa silabi nzima kama maneno yafuatayo yanavyoonyesha.

[o čiemo] > [očiemoga]	- anakula	- hula
[oti ] > [otijɔni]	- afanye	- anakufanyia
[ti č ] > [joti č ]	- kazi	- wafanyakazi

### 3.17 Ubashiri wa Makosa kwa Mujibu wa Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi (N.U.L) na Fonolojia Zalishi Asilia (Fza)

(i) Katika kujifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili, wanafunzi wazawa wa Dholuo hupata shida kutamka fonimu [v, z, ʃ, ʒ, x]. Jambo hili hutokea kwa sababu ya kutokuwa kwa vitamkwa hivi katika mfumo wa kifonolojia wa Dholuo. (Tazama 2.2.1). Ala zao za matamshi huwa hazijazoea kutamka sauti hizi hasa wanapotumia lugha ya Dholuo kila mara wakiwa nyumbani na Kiswahili shuleni pekee.

Utaratibu huu unaweza kufafanuliwa na data ifuatayo:

#### Kiswahili

[x]	- Kheri	- [xeri]
[ʒ]	- lugha	- [luʒ a]
[k]	- kuku	- [kuku]
[g]	- gamba	- [gamba]
[ŋ]	- ng'ombe	- [ŋ ombe]

#### Dholuo

_____	(hakuna)
_____	(hakuna)
kado - [kado]	- mchuzi
gwen- [gwen]	- kuku
ng'ato - [ŋ ato]	- mtu

#### Kiswahili

[j]	- [jambo]- jambo
[č]	- [č ama] - chama
[ʃ]	- [ʃ amba]- shamba
[j]	- [jule] - yule

#### Dholuo

juko- [juko]	- pata
chiemo- [čiemo]	- chakula
_____	(hakuna)
yamo- [jamo]	- upepo

#### Kiswahili

[t]	- [tawi] - tawi
[d]	- [dada] - dada

#### Dholuo

toko- [tɔko]	- pakua
dala- [dala]	- nyumbani

[s] - [sura] - sura  
 [z] - [zua] - zua  
 [l] - [lala] - lala  
 [r] - [ruka] - ruka  
 [n] - [nenō] - neno

**Kiswahili**

[n] - [nani] - nani  
 [t] - [tume] - tume  
 [l] - [lala] - lala

**Kiswahili**

[ʃ] - [ʃamba] - amba  
 [ɲ] - [ɲanya] - nyanya  
 [z] - [zima] - zima  
 [ʒ] - [ʒambo] - jambo  
 [č] - [čafu] - chafu

**Kiswahili**

[k] - [kaka] - kaka  
 [ɣ] - [luɣa] - lugha  
 [g] - [gamba] - gamba  
 [x] - [masalxeri]

**Kiswahili**

[p] - [papa] - papa  
 [b] - [baba] - baba  
 [m] - [mama] - mama

sembe- [sembe] - mkia

law- [law] - nguo

rombo - [rombo] - kondoo

nam- [nam] - ziwa

**Dholuo**

nenō- [nenō] - ushuhuda

tero- [tero] - kupeleka

lemo- [lemo] - maombi

**Dholuo**

nyasi- [ɲasi] - sherehe

jut- [ʃut] - inama

chamo- [čamo] - kula

**Dholuo**

kano- [kano] - weka

gwedho- [gweðo] - gwedho - bariki

**Dholuo**

paro- [paro] - fikira

bat- [bat] - mkono

mako- [mako] - shika

**Kiswahili**

[f] – [faa] – faa

[v] – [vaa] – vaa

[θ] – [θelufi] – theluji

[ð] – [ðambi] – dhambi

[ʃ] – [ʃamba] – shamba

[s] – [sima] – sima

[z] – [zika] – zika

**Dholuo**

fulo- [fulo] – sema

thum- [θum] – kinanda

dhum - [ðum] – kuongea

sando - [sando] – kutesa

**Kiswahili**

[h] – [huru] – huru

- [hati] – hati

**Dholuo**

hawi- [hawi] – bahati

hera- [hera] – mapenzi

(ii) Wanafunzi wazawa wa Dholuo huingiza irabu za Dholuo katika mfumo sauti wa Kiswahili. Kuna irabu tano pekee katika lugha ya Kiswahili, lakini Dholuo ina irabu kumi. (Tazama kielelezo 3.1 na 3.6).

(iii) Dholuo ni lugha ya kiimbo. Wanafunzi wazawa wa Dholuo huingiza viimbo vya Dholuo katika utamkaji wa sauti za Kiswahili

(iv) Lugha ya Dholuo ina mfumo huru wa mkazo kwa vile mkazo huweza kuwekwa kwenye silabi yoyote. Kwa njia hii, lugha ya Dholuo ni tofauti na Kiswahili, ambacho maneno yake huchukua mkazo kwenye silabi ya pili kutoka mwisho. Wanafunzi wa Dholuo huingiza matumizi huru ya mikazo katika maneno ya Kiswahili. (tazama 4.4.)

(v) Irabu za Kiswahili hurefushwa, sifa ambayo hupatikana katika irabu au vokali za Dholuo pekee.

(vi) Wanafunzi wazawa wa Dholuo katika kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili huweza kuchopeka au kudondosha sauti za irabu, konsonanti na hata silabi za maneno ya Kiswahili ili kurahisisha matamshi (tazama 4.5.1, 4.6 na 4.7)

Ubashiri huu, ulituongoza kuangalia sehemu za lugha au fonimu ambazo huenda zikasababisha makosa wakati wanafunzi wazawa wa Dholuo

wanapojifunza kiswahili

### **3:18 Hitimisho**

Katika sura hii,tulichunguza na kujadili miundo ya kifonolojia ya lugha ya Kiswahili na Dholuo.Tumezirejelea orodha za fonimu za Kiswahili kutokana na kazi za wanaisimu Nchimbi(1992),Mgullu(1999) na Aswani (2001) na zile za Dholuo kutokana na wanaisimu Okombo(1982) na Omondi (1982). Aidha tulichunguza silabi za lugha hizi mbili ,huku tukizingatia vijenzi vyake, muundo wake na umuhimu wake katika fonolojia ya lugha hizi mbili.Hatimaye tulichunguza kanuni za uwekaji wa mikazo katika maneno ya Kiswahili na Dholuo.

## SURA YA NNE

### 4.0 UCHANGANUZI WA MAKOSA YA MATAMSHI NA HIJAI.

#### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, athari za kifonolojia za Dholuo katika Kiswahili (L2) zimeelezewa kwa kuchambua data iliyopatikana nyanjani. Data hii ilipatikana kwa njia ya uchunguzi shiriki katika mazungumzo ya kawaida, kurekodiwa matamshi kwenye kanda na uandishi wa imla. Kwa hivyo, tulichunguza athari za kifonolojia zinazodhihirika wakati msemaji mzawa wa Dholuo anapojifunza Kiswahili sanifu.

#### 4.2 Athari za utamkaji wa Sauti za Konsonanti.

Hatua ya kwanza ya uchanganuzi wa data ambayo vidadisi vyake tulikwisha kurekodi kwenye kanda za kunasia sauti na pia nakala za wanafunzi za kazi ya imla na insha ilikuwa ni ; kuhesabu makosa ya kila mtafitiwa katika kuzitamka na kuziandika vile vitamkwa teule (v, z, j, y na x). Fonimu hizi zilipangwa kwenye maneno ambayo yalikuwa na mfumo wa nitowe – nikutowe (tazama kiambatisho D).

Makosa ya matamshi na hijai yaliorodheshwa hivi:

Vitamkwa	Makosa ya matamshi	Makosa ya hijai
[ʃ] - [s]	49	37
[z] - [s]	30	24
[v] - [f]	14	07
[ʒ] - [ʒ]	83	63
[ʒ] - [k]	23	14
[x] - [h]	66	22
[x] - [k]	31	14

Makosa haya yalitumiwa kupata wastani wa kihesabu

$$\left[ \frac{\sum X}{n} \times 100 \right]$$

Utafiti huu umeonyesha kuwa, wanafunzi wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili sanifu aghalabu hukumbwa na shida ya kuzitamka baadhi ya fonimu za Kiswahili Sanifu hasa zile ambazo hazipatikani katika orodha ya fonimu za Dholuo (tazama 3:1:4 hadi 3:1:11). Data ifuatayo imeonyesha tofauti zilizopo baina ya mfumo wa fonimu wa Dholuo (L1) na ule wa Kiswahili sanifu (L2): na athari za tofauti hizi kwa matamshi na maandishi ya Kiswahili Sanifu yanayofanywa na wazawa wa (L1), kama chati ifuatayo inavyodhihirisha

#### Makosa yanayotokana na athari za kifonolojia za Dholuo katika Kiswahili

FONIMU ZA KISWAHILI	MATAMSHI KWA MISINGI YA L1	MAKOSA YA MATAMSHI %	MAKOSA KATIKA MAANDISHI (IMLA)
[ʃ]	[s]	6.13%	4.62%
[z]	[s]	4.62%	1.84%
[v]	[f]	5.73%	4.25%
[ɣ]	[g]	41.56%	31.52%
[ʎ]	[k]	0.32%	0.20%
[x]	[h]	33%	11%
[x]	[k]	15.5%	0.7%

Jedwali 4:1

Athari za tofauti hizi kwa matamshi na maandishi ya Kiswahili Sanifu yanayofanywa na wazawa wa Dholuo yalijitokeza hivi katika maneno yafuatayo.

[ʃ] – [ʃ uka] > [s] - [suka]

[ʃ] – [maʃ izi] > [s] - [masisi]

[z] – [zima] > [s] - [sima]

[z] – [hizi] > [s] - [hisi]

[v] – [vaa] > [f] - [faa]

[v] – [jivu] > [f] - [jifu]

[ɣ] – [ɣ ali] > [g] - [gali]

[ʎ] – [lu ʎa] > [g] - [luga]



- [ɣ] – [lu ɣa].>[g]-[luga]
- [k] – [kali].>[k]-[kali]
- [k] – [kasia].>[k]-[kasia]
- [x] – [masalxeri].>[h]-[masalheri]
- [x] – [ixlasi].>[h]-[ihlasi]
- [x] – [ixlasi].>[k]-[iklasi]

Kutokana na data tulizopata, ilibainika wazi kuwa lugha ya kwanza huathiri lugha ya pili kifonolojia. Vitamkwa [ɣ] na [x] vilitatiza wanafunzi wengi kutamka labda kwa sababu sauti hizi ni geni. Pia ilibainika kuwa matamshi mabaya huweza kuendelezwa kwa kiasi fulani katika maandishi. Hata hivyo, makosa ya hijai yalikuwa machache kuliko makosa ya matamshi.

#### 4.1 Usahihishaji Mno

Hii ni hali ya utamkaji mbaya wa vitamkwa au sauti mbalimbali katika jitihada za kujaribu kuepuka athari za lugha ya kwanza.

Kutokana na data ya utafiti huu, baadhi ya wanafunzi wazawa wa Dholuo, katika kuzitamka fonimu za Kiswahili, walitumia fonimu tofauti ambazo hazipatikani katika Dholuo (L1) lakini ziko katika orodha ya Kiswahili Sanifu. Aidha, fonimu fulani ambazo hazipatikani katika orodha ya sauti za Dholuo (L1) pia ziliingizwa kuchukua nafasi ya zile zinazopatikana katika orodha ya fonimu za Dholuo, hivyo, kusababisha athari za matamshi kwa wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili Sanifu. Data ifuatayo ni dhihirisho ya usahihishaji mno wa fonimu ambazo huathiri matamshi: tazama jadwali 4.2

Makosa yanayotokana na usahihishaji mno

FONIMU ZA KISWAHILI	USAHIHISHAJI MNO	MAKOSA YA MATAMSHI	MAKOSA YA MAANDISHI
[z]	[ʒ]	0.15%	0.46%
[s]	[z]	1.71%	2.36%
[s]	[ʒ]	2.64%	1.7%
[ʒ]	[z]	1.75%	0.8%
[x]	[g]	0.03%	0%

Jedwali 4:2

Athari za usahihishaji mno kwa matamshi na maandishi ya Kiswahili sanifu yanayofanywa na wanafunzi wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili yalijitokeza hivi, katika maneno yafuatayo.

[z] > [ʒ]	- [hizi]	- [hiʃi]
[z] > [ʒ]	- [huzuni]	- [huʃuni]
[s] > [z]	- [sima]	- [zima]
[s] > [z]	- [masika]	- [mazika]
[s] > [ʒ]	- [kisa]	- [kiʃa]
[ʒ] > [z]	- [ma izi]	- [mazizi]
[ʒ] > [z]	- [ʃule]	- [zule]
[x] > [g]	- [ixlasi]	- [iglasi]

### 4.3 Athari za Utamkaji wa Sauti za Irabu

Uchanganuzi wa data iliyokusanywa kwa ajili ya utafiti huu umeonyesha kwamba baadhi ya wazungumzaji wazawa wa Dholuo huendeleza sifa ya irabu ndefu ambayo hupatikana katika lugha ya Dholuo na wala hazipatikani katika Kiswahili sanifu ambayo ina irabu fupi au irabu za kawaida pekee. Irabu hizo zenye sifa ya urefu, huhifadhiwa kupitia kwa uwekaji mkazo kwenye silabi fulani. Katika lugha ya Dholuo ambayo ni lugha ya kiimbo. Sifa ya urefu wa irabu ni bainifu kwa sababu husababisha tofauti ya maana katika jozi ya maneno. Sauti za Dholuo zilizopaazwa huingizwa katika Kiswahili lugha ambayo haipazi sauti.

Athari za tofauti hizi, yaani irabu ndefu na irabu za kawaida, kwa matamshi na maandishi ya Kiswahili sanifu yanayofanywa na wazawa wa Dholuo yalijitokeza hivi katika maneno yafuatayo.

<b>Kiswahili Sanifu</b>		<b>Athari</b>
[atafika]	>	[ataf:ika]
[mimi]	>	[mi:mi]
[fahamu]	>	[faha:mu]
[maziwa]	>	[masi:wa]

#### 4.4 Mkazo

Lugha ya Dholuo inatofautiana na ile ya Kiswahili kwa jinsi ambavyo muundo asili wa lugha ya Dholuo unadhihirisha uwekaji mkazo ulio huru; yaani, mkazo huwekwa katika silabi mbalimbali kutegemea neno; katika silabi ya mwanzo ya neno, ya pili, ya tatu na hata ya mwisho. Lakini lugha ya Kiswahili Sanifu inahimiza uwekaji mkazo katika silabi ya pili kutoka mwisho wa neno (rejelea sura ya tatu: 3:8 na 3:14).

Utafiti tulioufanya umeonyesha kuwa, baadhi ya wanafunzi wazawa wa Dholuo, wanapojifunza Kiswahili huhifadhi kanuni za uwekaji mkazo wa lugha ya Dholuo. Data ifuatayo imeonyesha kwamba baadhi ya wanafunzi walifuata kanuni za lugha ya Dholuo kuweka mkazo katika silabi ya kwanza.

<b>Mkazo katika Kiswahili sanifu</b>		<b>Mkazo kwa misingi ya Dholuo</b>
[daíma]	>	[dáima]
[guníia]	>	[ḡunia]
[kula]	>	[Kulá]
[fungúua]	>	[ḡungua]
[píga]	>	[píga]

Kuna pia maneno mengine ambayo kwa kiasi kikubwa, yalitamkwa kwa kuwekewa mkazo katika silabi ya pili au ya tatu. Tazama mifano.

### Mkazo katika Kiswahili Sanifu

[uǵali]

[hamsini]

[iǵapokuwa]

[anaǵeza]

### Mkazo kwa misingi ya L1

[ugali]

[hamusini]

[iǵapokuwa]

[anaǵeza]

Baadhi ya wanafunzi pia waliweka mkazo katika silabi ya mwisho wa neno, kama inavyodhihirika katika data ifuatayo.

### Mkazo katika Kiswahili sanifu

[dunia]

[ǵumuija]

[gawana]

[kamata]

### Mkazo kwa misingi ya L1

[dunija]

[ǵumuija]

[gawana]

[kamata]

#### 4.5.0 Mifanyiko ya Kifonolojia.

Mifanyiko ya kifonolojia ni mabadiliko mbalimbali ambayo hutokea baada ya fonimu mbalimbali kuwekwa pamoja wakati wa kuunda vipashio vilivyo vikubwa zaidi kuliko hizo fonimu zenyewe. (Mgullu 1999:81). Mabadiliko ambayo hutokea aghalabu hutegemea muktadha wa kifonetiki. Kwa mfano, kuna kudondoshwa kwa baadhi ya sauti, kuungana kwa sauti na hata kurefushwa kwa baadhi ya sauti. Utafiti tulioufanya umeshughulikia mifanyiko ya kifonolojia ifuatayo:

#### 4.5.1 Uchopekaji

Uchopekaji ni mfanyiko wa kifonolojia ambao hupelekea kuchopekwa kwa kipashio pale ambapo hakikuwepo. Mfanyiko huu ni moja kati ya njia za kifonolojia ambazo hutumika ili kudhibiti muundo wa kifonolojia unaopendelewa na lugha husika (tazama, Mgullu 1999:85 -94). Mwanafunzi mzawa wa Dholuo anayejiifunza Kiswahili kama lugha ya pili, mara nyingi huhifadhi muundo asilia wa lugha ya Dholuo ambao kama tulivyodokeza hapo awali katika sura ya tatu, hutofautiana na lugha ya Kiswahili kifonolojia Jambo hili humfanya mwanafunzi mzawa wa Dholuo kuchopeka fonimu fulani kwenye neno ili kuleta ruwaza

inayopendelewa. Katika lugha ya Kiswahili, nazali [m] na [n] huweza kujisimamia kama silabi, mwanzoni mwa neno au katikati mwa neno. Mfumo huu wa sauti haupatikani katika lugha ya Dholuo; basi husababisha wanafunzi wazawa wa Dholuo kuchopeka fonimu [u] na [i] kati ya konsonanti hizi nazali ili kuleta ruwaza inayokubalika (tazama 4.5.1.1)

#### 4:5:1.1 Uchopekaji wa Irabu

Utafiti tulioufanya umedhihirisha kuwa, wanafunzi wazawa wa Dholuo huchopeka irabu au sauti za irabu fulani mwanzo wa neno au kati ya konsonanti fulani hasa za nasali ili kuvunja mkururo wa konsonanti na kurahisisha matamshi. Katika lugha ya Dholuo ni nadra sana kwa sauti za nasali [m] na [n] kujisimamia kama silabi. Wanafunzi; wazawa wa Dholuo wanapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili huendeleza muundo huo katika lugha ya Kiswahili.


#### Kiswahili Sanifu

#### Athari za L1

[mtoto]	-	kkvkv	-	[mutoto] - kvkvkv
[mtu]	-	kkv	-	[mutu] - kvkv
[mkora]	-	kkvkvkv	-	[makora] - kvkvkv, [mukora]-kvkvkv
[nne]	-	kkv	-	[ine] - vkv
[mlazo]	-	kkvkv	-	[milaso]- kvkvkv, [mulaso]-kvkvkv
[mkorofi]	-	kkvkv kv	-	[mikorofi]- kvkvkvkv, [mukorofi]
[mmoja]	-	kkvkv	-	[mumoja]- kvkvkv

Maneno haya licha ya kwamba katika hali asilia ya Kiswahili yana konsonanti ambatano, huchopekwa irabu [u], [i] au [a] ili kuvunja mkururo wa konsonanti na pia kuondoa hali ya sauti ng'ong'o [m] na [n] kujisimamia kama silabi

### Kielelezo 4.1



### 4:5:1:2 Uchopekaji wa Konsonanti

Kutokana na data tuliyokusanya, kuna mifano michache ya maneno yanayodhihirisha hali ya uchopekaji wa konsonanti. Wanafunzi wazawa wa Dholuo wanapojifunza Kiswahili huchopeka konsonanti katika maneno fulani ili kuvunja mfululizo au mkururo wa irabu. Wanafunzi wengi wamechopeka viyevusho. [ j ] na [ w ] ili kutenga irabu [ i ] , [ a ] na [ e ].

#### Kiswahili sanifu

#### Athari

[ gasia ] -	kvkvv	>	[ gasija ] - kvkvkv
[ dunia ] -	kvkvv	>	[ dunija ] - kvkvkv
[ kazia ] -	kvkvv	>	[ kazija ] - kvkvkv
[ majai ] -	kvkvv	>	[ majaji ] - kvkvkv
[ maembe ] -	kvkvv	>	[ mawembe ] - kvkvkv


Athari hii inaonyesha kuchopekwa kwa konsonanti viyevusho [ j ] na [ w ]. Ni dhahiri kwamba konsonanti [ j ] na [ w ] zimenuiwa kuvunja mkururo wa irabu [ i ], [ a ] na [ e ] miundo ambayo haipatikani katika fonolojia ya Dholuo.

**Kielelezo 4.2**

[majai] – kvkv

>

[majaji] - kvkvk<sup>1/2</sup>v



**4.5.1.3 Uchopekaji wa Silabi**

Katika kujifunza Kiswahili, wasemaji wazawa wa Dholuo huweza kuchopeka silabi nzima katika neno ili kuafiki ruwaza au muundo unaokubalika katika lugha ya Dholuo. Uchopekaji wa silabi nzima hutokea ili kurahisisha matamshi. Kutokana na data niliyokusanya, uchopekaji wa silabi nzima umejitokeza hivi; konsonanti + konsonanti + irabu [KKKI] katika maneno yafuatayo.

**(i) Silabi liyoundwa kwa konsonanti+ Konsonanti + Konsonanti + irabu**

- [skru \$ bu] - kkkv \$ kv > [si\$ku \$ru \$ bu]-kv \$kv \$ kv \$ kv
- [stru \$ n̄gi ] - kkkv \$ kkv > si \$ tu \$ ru \$ n̄gi]- kvkvkvkvkv
- [spri1 \$ ŋi] - kkkv \$ kv > si \$ pi \$ ri \$ ŋi –kv \$ kv \$ kv \$ kv

Data hii inatuelekeza kuibua kauli kuwa wanafunzi wazawa wa Dholuo huchopeka silabi fulani katika maneno, hasa konsonanti mbili au tatu zikifuatana ili kuvunja mkururo wa konsonanti.

**(ii) Silabi iliyojengwa kwa Konsonanti + Konsonanti + Irabu+ Konsonanti [ Kkik]**

Silabi yenye umbo hili ina mwanzo uliojengwa kutokana na mkururo wa konsonanti. Utamkaji wa silabi hii ni wa mpumuo mmoja wenye kilele cha irabu. Wanafunzi wazawa wa Dholuo huchopeka irabu ili kutenganisha konsonanti. Uchopekaji wa silabi hufanywa ili kurahisisha matamshi kwa kuzingatia muundo wa lugha ya Dholuo. Data ya utafiti huu imenipa mifano ya maneno yafuatayo.

**Kiswahili Sanifu**


[tra \$ kta] - kkv\$skv  
 [bla\$nske\$ti] - kkv\$skv\$skv

**- Uchopekaji wa Silabi.**

> [ti\$ra\$sk\$ta] - kv\$skv\$sk\$skv.  
 > [bu\$la\$sn\$ke\$st]- kv\$skv\$sk\$skv\$sk

**Kielelezo 4.4**

[trak\$ta] - kkvk\$skv > [ti\$ra\$sk\$ta] - kv\$skv\$sk\$skv.



**4.6 Udondoshaji**

Mfanyiko wa udondoshaji hutokea wakati ambapo kipashio fulani cha neno husika kinaondolewa kabisa katika mazingira maalum ya kifonotaktiki au kifonolojia. Udondoshaji, kwa hivyo unahusu irabu, konsonanti na hata silabi.

Katika fonolojia ya Kiswahili na Dholuo, inasemekana kuwa silabi yenye muundo wa konsonanti moja na vokali moja (k.v) ndio muundo wa kimsingi kabisa .



Mfanyiko wowote, ambao hupungunza muundo wa silabi changamano na kuzua ruwaza ( kv), huelekeza kwa kile kinachoitwa muundo wa silabi unaopendelewa zaidi. Lengo kuu la mfanyiko huu wa udondoshaji, ni kuvunja mkururo wa konsonanti au mwandamamo wa vokali.

#### 4:6:1 Udondoshaji wa Konsonanti

Silabi ya Dholuo na Kiswahili, aghalabu huwa na muundo unaopendelewa zaidi, yaani yenye mfuatano wa konsonanti na irabu. Uchaganuzi wa data iliyoikusanywa kwa ajili ya utafiti huu umeonyesha kwamba konsonanti ya koromeo [h] pia hudondoshwa iwapo inajitokeza mwanzo wa neno la Kiswahili. Kama vile katika:

Kiswahili Sanifu		- udondoshaji wa konsonanti	
[hizi]	- hizi-kvkv➤	[izi]	- izi- vkv.
[hisi]	- hisi-kvkv>	[isi]	- isi- vkv.
[hana]	- hana-kvkv>	[ ana]	- ana-vkv
[huzuni]	- huzuni-kvkvkv>	[ uzuni]	- uzuni-vkvkv
[husuni]	- husuni- kvkvkv>	[usuni]	- usuni-vkvkv.

Konsonanti ya koromeo [h] pia hudondoshwa itokeapo katikati mwa neno. Data ifuatayo ni dhihirisho la kauli hii.

Kiswahili Sanifu	Udondoshaji Wa Konsonanti
[mhuni] - mhuni-kkvkv	> [muuni] -muuni-kvvkv
[mhaṅḅdisi] - mhaṅḅdisi [kkukkvkv]	>[muāṅḅdisi] -muandisi-kvvkkvku
[mhaḍiri] - mhadhiri [kkvkvkv]	>[muaḍiri] -muadhiri-kvvkvkv

Tumegundua pia hali ya kiyeyusho [w] kudondoshwa mwanafunzi mzawa wa Dholuo anapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Mahali pa kiyeyusho [w] huchukuliwa na irabu [ u ]. Data ifuatayo ni dhihirisho la kauli hii.

**Kiswahili Sanifu****-Udondoshaji wa Kiyeyusho [w]**

[mwalimu]	-kkvkvkv	>	[mualimu]	-kvvkvkv.
[mwaka]	-kkvkv	>	muaka]	-kvvkv.
[mwana]	-kkvkv	>	[muana]	-kvvkv.
[mwizi]	-kkvkv	>	[muizi]	-kvvkv.
[anwani]	-vkkvkv	>	[anwani]	-kvvkv.

**4.6.2 Kudondoshwa kwa Vokali**

Kutokana na data tuliyoipata baadhi ya wanafunzi wazawa wa Dholuo walidondosha baadhi ya sauti za vokali wanapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Udondoshaji wa vokali hutokea katika mazingira ya mwanzo wa neno, kati ya vokali na mwisho wa neno.

**4.6.2.1 Udondoshaji wa vokali katika mazingira ya mwanzo wa neno.**

Fonolojia ya Dholuo hairuhusu mkururo wa vokali kujitokeza mwanzoni mwa neno. Mwanafunzi mzawa wa Dholuo katika kujifunza Kiswahili kama lugha ya pili hudondoa vokali moja au huchopeka konsonanti ili kuvunja mkururo wa vokali.

**Kiswahili Sanifu****Udondoshaji wa Vokali**

[uundaji]	-vvkkvkv	>	[Øundaji]	-vkkvkv.
[uopoe]	-vvkvv	>	[Øopoe]	-vkvv.

**4.6.2.2. Katika mazingira ya kati vokali****Kiswahili Sanifu****Udondoshaji wa Vokali**

[maandamano]	-kvvkkvkvkv	>	[ma Ødamano]	-kvkkvkvkv
[waafrika]	-kvvkkvkv	>	[wa Øfrika]	-kvkkvkv
[waandalizi]	-kvvkvkvkv	>	[wa Ødalizi]	-kvkkvkvkv
[maalum]	kvvkvk	>	[ma Ølum]	-kvkvk
[Maadili]	-kvvkvkv	>	[ma Ødili]	-kvkvkv
[maadam]	-kvvkvk	>	[ma Ødam]	-kvkvk
[pooza]	-kvvkv	>	[po Øza]	-kvkv
[laana]	-kvvkv	>	[la Øna]	-kvkv

[muundo]                      -kvvkkv                      >                      [m Øundo]                      -kvkkv

#### 4.6.2.3 Katitka mazingira ya mwisho wa neno

<b>Kiswahili Sanifu</b>			<b>Udondoshaji wa Vokali.</b>	
[sanaa]	-kvkvv	>	[sanaØ]	- kvkv
[mzee]	-kkvv	>	[museØ]	- kvkv
[zaraa]	-kvkvv	>	[saraØ]	- kvkv
[jamaa]	-kvkvv	>	[jamaØ]	- kvkv
[zaa]	-kvv	>	[saØ]	- kv
[kaa]	-kvv	>	[kaØ]	- kv
[twaa]	- kkkvv	>	[twaØ]	- kvv

Data hii inatuelekeza kuibua kauli kuwa wanafunzi wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili hudondoa baadhi ya vokali katikati mwa neno na mwisho wa neno ili kuvunja mkururo wa vokali [a], [e],[o] na [u] ili kurahisisha matamshi. Katika muundo wa Dholuo, ni nadra kwa vokali hizi kuendelezwa katika mkururo. Jambo hili hutokea ili kuzuia muundo wa kimsingi au muundo wa silabi unaopendelewa zaidi, ambao katika Dholuo na Kiswahili ni ule wenye ruwaza [kv] (konsonanti na vokali). Uchanganuzi wa data iliyokusanya kwa ajili ya utafiti huu umeonyesha kwamba vokali ya mwisho hudondoshwa hasa katika maneno ya mkopo na hata maneno mengine ya Kiswahili. Dholuo kama lugha nyinginezo za kanailoti, inaruhusu muundo wa maneno kuishia kwa konsonanti. Kwa hivyo, irabu au vokali za mwisho hudondoshwa ili kurahisisha matamshi kwa kufupisha neno.

Mifano

<b>Kiswahili Sanifu</b>			<b>Udondoshaji wa Vokali ya mwisho</b>	
[hospitali]	-kvkkvkvkv	>	[ospital Ø]	-vkkvkvk
[ofisi]	-kvkvv	>	[ofis Ø]	-kvkv
[polisi]	-kvkvkv	>	[polis Ø]	- kvkvk
[mwalimu]	-kkvkvkv	>	[mualim Ø]	-kvkvv


### 4.6.3 Udondoshaji Wa Silabi Nzima

Kutokana na data tuliyoipata, baadhi ya wanafunzi wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili, walidondoa silabi nzima ili kurahisisha matamshi. Ilibainika kwamba sauti ya koromeo/h/ pamoja na irabu [a] na [u] hudondoshwa mwanzoni, katikati, na mwisho wa neno ili kufupisha neno. Kwa hivyo, hali hii inarahisisha matamshi kwa mzungumzaji mzawa wa Dholuo.

#### Mifano.

Kiswahili Sanifu	-	Udondoshaji wa silabi
[m ahara]-kkvkvkv	>	[msara] - kkvkv
[ʃerehe]-kvkvkv	>	[seree] - kvkvv
[uʃuhuda]-vkvkvkv	>	[usuda] -vkvkv
[maharamia]-kvkvkv	>	[maramia] - kvkvkv

#### Kielelzo 4.5



### 4.7 Usilibishwaji

Silabi ni tamko linalojengwa na fonimu moja au zaidi. Muundo wa silabi ya lugha yoyote ile hutawaliwa na muundo wa kifonolojia wa lugha hiyo. Hyman (1975: 14-163) anadokeza kwamba mfuatano asilia wa sauti katika silabi za lugha nyingi ni wa

[KV]. Katika mkabala huu, kanuni za usilibishwaji hulenga kuuhifadhi muundo huu. Uchanganuzi wa data iliyokusanywa kwa ajili ya utafiti huu umeonyesha kuwa, wanafunzi wazawa wa Dholuo wanapojifunza Kiswahili huweza kubadilisha muundo wa silabi katika maneno ya Kiswahili ili kurahisisha matarshi. Jambo hili hutokea wakati silabi fulani hudondoshwa na huchopekwa ili kuhifadhi muundo asilia wa [KV], yaani muundo unaopendelewa wa konsonanti na irabu.

**4.7.1 Silabi ya vokali pekee katikati mwa Maneno**

Silabi ya vokali pekee, katikati mwa neno hupatikana katika lugha ya Dholuo na Kiswahili. Hata hivyo, lugha ya Dholuo haina mkururo wa vokali [a] katikati mwa maneno; hivyo, kupelekea wanafunzi wazawa wa Dholuo kupitia kwa mazoea ya lugha ya kwanza kudondoa vokali moja au kuchopeka konsonanti ili kuvunja mkururo wa vokali [a].

**Mifano:**



**Kiswahili Sanifu**

**Usilibishwaji**

[ma\$ a \$ na] KV \$ V \$ KV	>	[ ma \$ Ø \$ na ] KV \$ KV
[ma\$ a\$ da\$ mu] – KV \$ V \$ KV\$KV	>	[ma \$ da \$ m] – KV \$ KV\$ K
[ la \$ a \$ na] – KV\$ V \$ KV	>	[ la \$ Ø \$ na] – KV\$ KV
[ ma \$ a\$ si] – KV\$ V\$ KV	>	[ ma \$ Ø \$ si] – KV \$ KV

**Kielezo cha 4.6**

[ la \$ a\$ na] > [la \$ na]



**4.7.2 Silabi iliyoundwa Kwa Konsonanti Endelezi- Ng'ong'o [K]**


Uchanganuzi wa data iliyokusanywa kwa ajili ya utafiti huu, inatuelekeza kuibua kauli kuwa wanafunzi wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili huchopeka silabi fulani, mwanzoni mwa maneno, ikiwa maneno hayo yanaanza kwa konsonanti ng'ong'o [n] na [m] ili kuvunja mkururo wa konsonanti. Katika muundo wa Dholuo, konsonanti ng'ong'o [n] na [m] haziwezi kijisimamia kipekee kama silabi. Vokali [i] hupachikwa ili kuvunja mkururo wa konsonanti na pia kurahisisha matamshi

**Mifano:**

<b>Kiswahili Sanifu</b>		<b>Usilibishaji</b>
[ n \$ č i ]	— K \$ KKV	> [ in \$ č i ] VK \$ KKV
[ n \$ ne ]	— K \$ KV	> [ i \$ ne ] V \$ KV.
[ n \$ zi ]	— K \$ KV	> [ i \$ nzi ] V \$ KKV.

## Kielelzo cha 4.7

[ n \$ zi ] > [ i \$ nsi ]



## 4.8 Athari zinazotokana na Kanuni za Kifonotaktiki

Uchunguzi wa kanuni za kifonotaktiki za lugha ya Kiswahili na Dholuo unaonyesha kwamba lugha hizi mbili hazina tofauti kubwa sana katika mfuatano wa sauti. Hata hivyo, uchanganuzi wa data iliyokusanywa kwa ajili ya utafiti huu umeonyesha kwamba, wanafunzi wazawa wa Dholuo waliweza kuchopeka au kudondoa sauti fulani, hasa maumbo ambayo hayapatikani katika kanuni za kifonotaktiki za Dholuo. Walifanya hivi ili kurahisisha matamshi huku wakiongozwa na hali ya mazoea ya lugha yao ya kwanza. Mifuatano ya sauti isiyopatikana katika muundo wa Dholou hubadilishwa kupitia kwa udondoshaji na uchopekaji. Data ifuatayo ni dhihirisho la kauli hii.

### Kiswahili Sanifu

gh – [lu a] – lugha  
 kh – [ xeri ] – kheri  
 gh – [ɣasia] – ghasia  
 kh – [ixlasi] – ikhlasi  
 nn – [nne] - nne  
 mm – [umma] – umma

### Athari kutokana wa kauli za Kifonotaktiki.

> [luga] - luga  
 > [ heri ] - heri  
 > [gasia] – gasia  
 > [ iklasi] – iklasi  
 > [ine] - ine  
 > [uma] - uma

mp	- [mpaka] - mpaka	>	[ mupaka] –mupaka
fw	- [fwari] – shwari	>	[swari] – swari
nz	- [ mwanafunzi] – mwanafunzi	>	[ muanafunsi] - mwanafunsi

Data hii inabainisha kuwa ,wanafunzi wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili huweza kuongozwa kwa kiasi fulani na muundo wa Dholuo (L1) katika kujifunza Kiswahili.

#### 4: 9 Hitimisho

Sura hii imechunguza matokeo ya athari za kifonolojia ya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Utafiti huu umechunguza na kuonyesha tofauti zilizopo baina ya mfumo sauti wa Dholuo (L1) na ule wa Kiswahili Sanifu (L2); na athari za tofauti hizi kwa matamshi na maandishi ya Kiswahili Sanifu yanayofanywa na wazawa wa Dholuo. Mifanyiko ya aina mbalimbali imeainishwa na kuchunguzwa. Kisha mifanyiko hii imechanganuliwa na kuelezwa kinagaubaga.

Hii ni pamoja na:

- i. Uchopekaji
- ii. Udondoshaji
- iii. Uwekaji mkazo
- iv. Usilibishaji

Mifanyiko hii yote imeonyesha kuwa mwanafunzi mzawa wa Dholuo anayejifunza Kiswahili huhifadhi muundo asilia wa lugha yake ya kwanza jambo ambalo huelekea kumfanya kuhamisha muundo wake wa Dholuo katika Kiswahili.

Ilibainika wazi kuwa, wanafunzi wazawa wa Dholuo walifanya makosa ya matamshi na pia hijai(tazama jedwali 4.1 na 4.2 Uk. 87 na 89 ). Makosa haya yalitokana na tofauti zilizoko katika mifumo sauti ya lugha ya Dholuo na Kiswahili.



## SURA YA TANO

### 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii ya tano, mambo muhimu yaliyoibuka na kubainika kutokana na utafiti huu yameelezwa. Kisha, matatizo na mafanikio yaliyopatikana katika utafiti huu yameelezwa. Halafu, hitimisho likapatikana kwa kutoa mapendekezo kuhusu sehemu zinazohitajika kufanyiwa utafiti zaidi.

#### 5.2 Utafiti kwa Ujumla

Tasnifu hii imechunguza kwa kina athari za kifonolojia kwa wasemaji wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Lengo kuu la utafiti uliopelekea kukamilika kwa tasnifu hii lilikuwa ni kuweka bayana jinsi ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili huathirika na Dholuo. Utafiti huu kwa hivyo ulijikita katika kuchunguza athari zinazosababisha matamshi mabaya ya baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili. Tatizo kubwa la matumizi mwafaka ya lugha ya Kiswahili katika ngazi ya fonolojia ndilo lililokuwa kiini cha utafiti.

Katika sura ya kwanza, tulishughulikia maswala ya kimsingi katika utafiti kama vile; usuli wa mada, mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, natija ya utafiti, upeo wa utafiti, mbinu za utafiti na maelezo ya istilahi zilizotumika katika utafiti

Katika sura ya pili, ya utafiti huu tumeorodhesha hoja za wataalamu mbalimbali kuhusu athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Mapitio ya maandishi ya wataalamu mbalimbali katika sura hii yameonyesha kuweco kwa pengo za utafiti zinazolenga kuibua athari za kifonolojia kwa wasemaji wa lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Pia katika sehemu hii, tulishughulikia kwa kina nadharia

zilizotuongoza katika utafiti wetu, yaani Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi na Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia

Katika sura ya tatu tumeeleza kirefu vipengele muhimu vya miundo ya kifonolojia ya lugha ya Kiswahili na Dholuo. Tumezitambulisha, kuzichunguza na kuziorodhesha fonimu za Kiswahili na tukatoa kauli msingi kuhusu kanuni za kifonotaktiki zinazotawala na kueleza ujenzi wa vipashio vikubwa zaidi kama silabi na hatimaye maneno ya Kiswahili na Dholuo.

Sura hii pia imetoa nafasi kwa uchunguzi wa baadhi ya mifanyiko mbalimbali ya kifonolojia ambayo huziathiri sauti na silabi za Kiswahili katika mazingira mbalimbali. Aidha dhana na matumizi ya mkazo imefafanuliwa kwa kutathmini kauli za wanaisimu mbalimbali. Tuliichunguza muundo wa kifonolojia wa lugha ya Dholuo katika sura hii kwa minajili ya kulinganisha na ule wa lugha ya Kiswahili. Imezingatiwa kwamba, tofauti za kimuundo baina ya lugha hizi ndio msingi ambamo imekita haja ya uchunguzi wa athari za kifonolojia. Katika mkabala huu, ufahamu mzuri wa miundo- kifonolojia ya lugha zote mbili umetuwezesha kuyabaini athari ya kifonolojia yanayotokea, pindi wanafunzi wazawa wa Dholuo wanapozungumza au kuandika maneno ya Kiswahili.

Tumezitalii fonimu za lugha ya Kiswahili kwa kurejelea orodha za wanaisimu Mgullu (1999), Aswani; (2001) Mfaume (1984), Mbaabu (1985) na Nchimbi (1992) fonimu ya Dholuo, Okombo (1982), Omondi (1982) Musau (1993) na Mudhune (1994). Zaidi ya hayo, tumezichunguza kanuni za mfuatano wa fonimu hizo katika ujenzi wa vipashio vikubwa kama silabi na maneno na tukaeleza mabadiliko ya sauti za Kiswahili na Dholuo kwa mujibu wa mazingira mbali mbali ya kifonolojia na kifonetiki. Muundo wa silabi ya Dholuo na Kiswahili umejadiliwa na kanuni za uwekaji mipaka ya silabi kufafanuliwa. Matumizi ya mkazo pia yamechunguzwa. Ulinganishaji wa miundo ya lugha hizi mbili umeibua tofauti za msingi ambazo zinaathiri kwa namna mbalimbali ujifunzaji wa Kiswahili kimatamshi.

- i. Kwamba lugha za Kiswahili na Dholuo zinatofautiana katika idadi ya fonimu (irabu na konsonanti)
- ii. Kwamba lugha za Kiswahili na Dholuo zinatofautiana katika kanuni za mfuatano wa sauti (fonotaktiki). Mfuatano huu ndio husababisha ujenzi wa vipashio vikubwa kabisa kama silabi na neno.
- iii. Tofauti hizi za kifonotaktiki hutofautiana katika miundo na maumbo na husababisha tofauti katika uwekaji mkazo na silabi.
- iv. Kwamba lugha ya Kiswahili na Dholuo zinatofautiana katika aina ya sauti kama Dholuo ina irabu ndefu lakini Kiswahili hakina irabu ndefu.

Kauli hizi ni kielelezo kwamba lugha ya Kiswahili na Dholuo zinatofautiana kifonolojia. Kutofautiana huku ndiko kumesababisha athari za kifonolojia kwa wasenaji wa L1 kwa L2.

Katika kuichunguza na kuchanganua mifanyiko ya kifonolojia, imedhihirika kwamba baadhi ya wanafunzi huhifadhi na kuongozwa na miundo na mifumo sauti ya lugha ya kwanza. Tumeleza kwamba hali hii ina misingi yake katika kauli zifuatazo.

- i. Katika kujifunza lugha ya pili mwanafunzi huwa amekwisha jifunza lugha ya Dholuo ambayo imekita mizizi, basi huhamisha maumbo ya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili.
- ii. Mwanafunzi huelekezwa na ubongo wake ambao una uzoefu wa sauti mahususi zipatikanazo katika lugha ya kwanza.

Katika sura ya nne, tumeeleza data tuliyokusanya ambayo imetuwezesha kuthibitisha madai ya wataalamu mbalimbali wa isimu linganuzi na isimu asilia kuhusu swala pana la athari ya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Data hii imeonyesha kwamba:

- i. Lugha ya Dholuo imeingiza kanuni zake katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wazawa wa Dholuo wanapojifunza Kiswahili huingiza kanuni ya Dholuo katika Kiswahili.
- ii. Athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili kifonolojia, yanasababishwa na hali ya sauti fulani ambazo zinapatikana katika lugha ya pili lakini hazipatikani katika lugha kwanza.

- iii. Athari za kifonolojia hutokana na tofauti katika mifumo lugha ya Dholuo na Kiswahili.

Matokeo ya utafiti huu yanaelekea kuthibitisha na kuweka bayana athari za kifonolojia kwa wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili. Data tuliyokusanya na kufanyia uchanganuzi ilituwezesha :

- i. Kutambulisha vitamkwa vinavyotatiza wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Vitamkwa hivi vilitambulishwa kwa kurejelea hazina ya kifonemiki ya Dholuo na Kiswahili kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali. Vitamkwa ambavyo havipatikani katika abjadi ya Dholuo huwatatiza wazungumzaji wazawa wa Dholuo kutamka (Tazama 2.2.1)
- ii. Kuchunguza tofauti za kifonolojia baina ya Dholuo na Kiswahili na jinsi tofauti hizo huathiri wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Lugha hizi mbili zimetofautiana katika idadi za fonimu. Kiswahili kina konsonanti ishirini na tisa na irabu tano pekee ( Nchimbi 1992.14) ilhali Dholuo ina konsonanti ishirini na sita na irabu kumi (Okombo 1992 . 19)
- iii. Kuchunguza na kueleza athari za matamshi mabaya katika maandishi. Baadhi ya watafitiwa waliziandika herufi fulani jinsi walizitamka yaani kwa misingi ya lugha ya Dholuo.

Aidha makisio yote ya awali tuliyoyaorodhesha kama nadharia tete ya utafiti yamethibitishwa. Tasnifu hii, ambayo ndiyo matokeo ya utafiti tulioufanya, imethibitisha kwamba:

- i. Baadhi ya vitamkwa vya lugha ya Kiswahili huwatatiza wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Kwa mfano [v, ʃ, x, z, ʒ] huwatatiza wasemaji wazawa wa Dholuo kutamka.
- ii. Tofauti za kifonolojia za lugha ya Kiswahili na Dholuo ndizo hutatiza wasemaji wazawa wa Dholuo wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. (Tazama sura ya nne).

- iii. Utamkaji mbaya wa baadhi ya vitamkwa vya Kiswahili na wasemaji wazawa wa lugha ya Dholuo wanaojifunza Kiswahili huweza kusababisha maendelezo mabaya katika maandishi. Baadhi ya wanafunzi wazawa wa Dholuo walifanya makosa ya hijai kama vile:

[ʃ] → [s] – [shamba] → [samba]

[v] → [f] – [vumbi] → [fumbi]

[z] → [s] – [zima] → [sima]

[ʒ] → [g] – [ghali] → [gali]

[x] → [h] – [kheri] → [heri]

### 5.3 Vikwazo

Ni muhimu kutaja kwamba ingawa nia yetu mwanzoni ilikuwa ni kufanya utafiti darasani pekee, hali halisi nyanjani ilionyesha kwamba mambo mengi yalijitokeza nje ya darasa kupitia uchunguzi shiriki. Athari nyingi hutokea wakati wanafunzi wanacheza viwanjani na kwingineko shuleni, (nje ya darasa).

Ingawa utafiti huu hauhusiani moja kwa moja na taaluma ya fonetiki majaribio, kulitokea upungufu mkubwa wa vifaa vya kumwezesha mtafiti kuona jinsi ala mbalimbali za kutamkia zinavyoathiriana katika utamkaji wa sauti mbalimbali.

Lugha ya Dholuo huzungumzwa katika mkoa wa Nyanza ambao ni mpana zaidi, kwa hivyo, kuna uwezekano kuwa, kuna tofauti za matamshi ambazo huenda zikawa ni za kimaeneo. Kutokana na upungufu wa kifedha na wakati, haikuwezekana kufanya utafiti katika kila sehemu ya mkoa wa Nyanza.

### 5.4 Mapendekezo

Ingawa kulikuwa na matatizo madogomadogo, utafiti huu kwa kiasi kikubwa, umefanikiwa kutupatia majibu ya yale maswali yaliyokuwepo mwanzoni mwa utafiti huu. Kwa hivyo, utafiti huu ulijitokeza na mapendekezo haya:

- i. Utafiti zaidi ufanywe kuhusu athari za Dholuo kifonolojia kwa Kiswahili hasa fonolojia arudhi.

- ii. Pia utafiti zaidi ufanywe kuhusu athari za Dholuo kifonolojia kwa semantiki ya Kiswahili. Ni muhimu kuchunguza matatizo ambayo huenda yakasababishwa na athari hizi kwa maana au semantiki.
- iii. Pia kuna haja ya kuchunguza zaidi uhusiano ulioko baina ya fonolojia ya lugha na muundo wa maandishi yaani othografia.
- iv. Utafiti zaidi ufanywe kuhusu athari za kifonolojia za lugha nyinginezo, ili , matokeo yanayopatikana yatumiwe kuibuka na njia za Kisayansi za kuwasaidia wanaojifunza Kiswahili. Wanaoandaa mitaala pamoja na walimu watumie data hizi kuibua mikakati ya kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili katika shule za msingi na za upili.
- v. Utafiti zaidi ufanywe kuhusu jinsi lugha ya kwanza hasa Dholuo inavyoweza kuchangia kwa ukamilifu kujifunza lugha ya Kiswahili.
- vi. Kwa kutumia data maalumu na wala si usawazishaji, sehemu hii , yaani athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili ishughulikiwe kwa kina hasa katika kozi ya walimu wa Kiswahili katika vyuo vya walimu na vyuo vikuu nchini Kenya. Kozi hii itawawezesha walimu kujihami na mbinu mwafaka za kuwasaidia wanafunzi wao wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

Kwa hivyo ni muhimu kuhitimisha kwamba utafiti juu ya athari ya kifonolojia haujitoshelezi. Bado kuna mwanya unaoitisha uchunguzi zaidi.

## MAREJELEO

- All Wright, D and Bailey, K.M (1991) *Focus on the Language Classroom; An Introduction of Classroom Research for Language Teachers*. New York. Cambridge University Press
- Altenberg, E.P and Vago, R.M. (1983) *Theoretical Implications of Second Language Phonology Language Learning*. Vol 33, No 4, 427 – 443.
- Anderson, S.R. (1985) *Phonology in the Twentieth Century*. London, University of Chicago Press.
- Aronoff, M (1985) *Orthography and Linguistic Theory*. Katika S.K Verma, S.K and Krishanswamy N. (1989), *Modern Linguistics: An Introduction*. Bombay. Oxford University Press.
- Aswani, F.O.B (1993) "Fonolojia ya Silabi ya Kiswahili Sanifu na ya Kimarama; Uchunguzi Linganishi". Tasnifu ya M.Phil (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Moi
- .....( 2001) "Uswahilishaji Kifonolojia wa Maneno Mkopo yenye Asili ya Kiingereza katika Kiswahili sanifu."Tasnifu ya uzamifu (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Egerton.
- Ashton , E.O. (1944). *Swahili Grammar* London Longman.
- Bakari, M, (1982) "The Morphology of the Kenyan Swahili Dialects". Unpublished Ph.D. Thesis, University of Nairobi.
- Besha, R, M (1991) *The Acquisition of Swahili by Adult Maasai Speakers; Possible Areas of Conflict*. Hekmut Velag Hamburg. In Rottaland, F, and Omondi, L (ed), Proceedings of the Third Nilo- Saharan Linguistics Collegutum, Kisumu, Kenya, August 4-9, 1986
- Bloomfield, L. (1933) *Language*. New York. Holt Rhine hart and Winston.

- Batibo H.M. (1980) *Je, Fonolojia ya Kiswahili ni ya kibantu (makala iliyochapishwa)*  
Dar-es-Salaam TUKI
- Clark. J.and Yallop, C. (1990). *An Introduction to Phonetics and Phonology*. London.  
Basil Blackwell,Oxford.
- Corders S.P (1978) “ *The Significance of Learners Errors*” In: RichardsJ.C (ed), *Error Analysis; perspectives on second language acquisition* London.  
Longman.
- Corders S.P (1983). “ *A Role of Mother Tongue In Class, S. and Selinker. (ed.)language Transfer in Language Learning*”. Newburry.Rowley
- Crystal; D, (1987),. *The Cambridge Encyclopedia of Language*. Cambridge.Cambridge University Press.
- Dell, F (1989), *Generative Phonology*. Paris. Cambridge University Press.
- Donegan, P na Stampe, D. (1979) *The Study of Natural Phonology*. In Dinnsen, D. ed.  
Current approaches to phonological theory. Blooming town. Indiana University Press.
- Dorand, J. (1990) *Generative and Non – Linear Phonology* .New York. Longman.
- Dulay H.C, Burt, M.and Krashen, S.O (1982) *LanguageTwo*. New York. Oxford University Press
- Dulay H.C. na Burt M.K. (1974) *Errors and Strategies in Child Second Language Learning*. TESOL Quarterly , Vol.8.
- Eckman, F.R. (1981): *On the Naturalness of Interlanguages Phonological Rules; Language Learning*, Vol.31, No. 1,195- 216.
- Ellis .R. (1985), *Understanding Language Two Acquisition* Oxford. Oxford University Press



- Faerch, C. and Kasper, G. (eds) (1984): *Strategies in Interlanguage Communication* London. Longman.
- Ferguson, C.A. (1988): Phonological process. In Greenberg (ed), *Universals of Human Language*. Vol 2, Phonology. Stanford California. Stanford University Press 401- 422.
- Fillmore, C.J. (1981), *Ideal Readers and Real Readers*. In George Town University Round table on languages and linguistics 1981, D.Tannen (Ed), 248 – 270. Washington D.C Georgetown University Press.
- Fisiak J. (1981), *Some Introduction Notes Concerning Contrastive Linguistics*. In Fisiak, J. (ed) *Contrastive Linguistics and the Language Teacher*, Oxford. Pergamon Press.
- Flege, J. (1987), *A critical Period for Learning to Pronounce Foreign Languages*. *Applied Linguistics*, Vol8, No.1 162 –177.
- Franklin V.A (1980), *Errors in Linguistic Performance, Slips of the Tongue, Ear, Pen and Hand*. New York. Academic Press.
- Fromkin, V, and Rodman, R, (1983) *An Introduction to Language*. New York. C.B.S College Press.
- Greenberg, J.H (ed) (1988): *Universals of Human Language*. Volume 2, Phonology. Stanford California. Stanford University Press.
- Gregerson, E.A (1962). "Luo" an Unpublished Ph. D. Dissertation, Yale University, Connecticut.
- Halliday, M.A. (1964), *Linguistic Science and Language*. London Longman.
- Hyman, L. (1975), *Phonology, Theory and Analysis*; Holt Rinehart and Winston.
- Hockett, C.F. (1958), *A Course in Modern Linguistics*. New York. The Macmillan Company.

- Hooper, J.B (1976), *Phonological Disability in Children* Edward Arnold, London.
- Halliday M.A (1964), *Linguistic Science and Language* . London Longman
- James, C. (1980), *Contrastive Analysis*; London Longman.
- Kapinga, M.C.(1983) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili .Dar es salaam.
- Kimani, S. (1971), *Problems in Swahili and Phonology*, *Kiswahili: Journal of The Institute of Kiswahili: Research*, University of Dar- es- salaam Vol, 41.No.1, 94- 99.
- Kimemia, J.N. (2001), *Kiswahili. The Dilemma of Developing the National Language*. Egerton University Press.
- Krashen, S.D (1981), *Second Language Acquisition and Second Language Learning*. Oxford. Pergamon Press.
- Lado, R. (1957), *Linguistics Across Cultures*. Michigan. University of Michigan Press.
- Littlewood, W. (1984), *Foreign and Second Language Learning*. Cambridge. Cambridge University Press.
- Larsen - Freeman, O. na Long.M.H. (1981) *An Introduction to Languages Through Acquisition Research* London Longman.
- Massamba, O. (1996), *Phonological Theory. History and Development*.Dar es salaam Dar es salaam University Press.
- Mbaabu, I (1985), *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.
- Mdee, A. (1986), *Kiswahili: Maana na Matumizi yake* Nairobi International Publishers.

- Musau, P.M. (1993), *Aspects of Interphonology. The Study of Kenyan Learners of Swahili*. Bayreuth. Bayreuth University.
- Mfaume, G.E (1984), *Misingi ya isimu ya Lugha ya Kiswahili Dar-es-salaam*. Utamanduni Publishers.
- Mgullu R.S. (1999). *Mtaala wa Isimu Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili* Nairobi Longhorn Publishers.
- Mudhune E.S. (1994), A contrastive Analysis Approach to the Learning of Swahili Morphosyntax by Luo learners Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa chuo kikuu cha Kenyatta.
- Mukuthuria M. (2004), Kuathiriana kwa Kiswahili na Lahaja ya Kitigania: Uchanganuzi wa Taathira katika Muktadha wa Shule za Msingi na Upili katika Tigania – Kenya. Tasnifu ya Ph.D. ( haijachapishwa ). Chuo Kikuu cha Egerton.
- Mangwa, D.O (2005), Athari za Ekegusii katika Kiswahili na zinavyochangia matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili kwa wanafunzi wa kisii wilayani. Kisii kusini. Tasnifu ya M.A (haijachapishwa). Chuo kikuu cha Egerton
- Ngero, S.Wa. (1996), Mifanyiko ya Kifonolojia Kitika Kinyala cha Kakamega. Tasnifu ya M.A (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton.
- Nchimbi A.S. (1992), *Mfumo wa matamshi ya Fonimu za Kiswahili katika Baragumu ; Jarida la Kiswahili Maseno* - Chuo Kikuu cha Maseno
- Odhiambo, A.J. (1981), *Dholuo Phonology: Major Vowel Processes*. M.A Dissertation (unpublished) University of Nairobi.

- Okoth – Okombo, D. (1982), *Dholuo Morphophonemics in a Generative Framework*. Berlin. Dietrich Reimer, Verlag.
- Onyango, J.O (1997), “Uziada wa kisarufi katika Kiswahili cha wanafunzi wa Kinyala”. Unpublished M.A. Thesis, Kenyatta University.
- Omondi, N.L. (1982), *The Major Syntactic Structures of Dholuo*. Berlin. Dietrich Reimer Verlag
- Phillipson R, Etal (1990), *Foreign Second Language Pedagogy Research*. Philadelphia. Multilingual Mater Ltd.
- Polome, E.C (1967) *Swahili Language Handbook*. Washington D.C. Centre for Applied Linguistics.
- Rivers W.M. (1983), *Communicating Naturally in a Second Language; Theory and Practice in Language*, Cambridge. Cambridge University Press.
- Sapir, E. (1921), *Language*, New York. Harcourt Brace.
- Seliger, H.W. and Shohamy, E. (1986), *Second Language Research Methods*. London Oxford University Press.
- Spolsky, B. (1989), *Conditions for Second language Learning*. Oxford. Oxford University Press.
- Stafford, R.C (1967), *An Elementary Luo Grammar*, London Oxford University Press.
- Stampe, D. (1979), *The Study of Natural Phonology: Current Approaches to Phonological Theory*, Chicago. University of Chicago.
- Simpson, J.M. (1979), *A First Course in Linguistics* Edinburgh. Edinburgh University Press.

- Schane, S. A. (1972), *Natural Rules in Phonology*. Katika stockwlee R.P. na Maccavley R.S.K (1972): *Linguistic change and Generative Theory*. Bloomington Indiana University press.
- Sridhar S.N. (1981), *Contrastive Analysis Error Analysis and Interlanguage Three Phases of One Goal*; katika Fisiak J. (Mhariri) *Contrastive Linguistics and the Language Teacher*. Oxford pergomon press.
- TUKI. (1981), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi. Oxford University Press.
- \_\_\_\_\_(1990), *Kamusi Sanifuy ya Isimu na Lugha*. TUKI Dar - es – salaam
- Verma S.K na Krishnaswamy, N.(1989), *Modern Linguistics: An Introduction*. Bombay. Oxford University Press.
- Vatile, A.J. (1985): "Aspects of Kiswahili Stress": *Kiswahili: Journal of The Institute of Kiswahili Research*. University of Dar es salaam. Vol .53.106-113.
- Van ELS T. na wenzake (1984), *Applied Linguistic and the Learning and Teaching of Foreign Languages*. London Edward Arnold.
- Wanyoike E.N. (1978). "Vikwazo katika Mafunzo ya Kiswahili Kenya". Katika *Lugha: A Journal For Language Teachers in Kenya*. Vol. 5-35-42.
- Wilkins, D.A. (1972), *Linguistic in Language Teaching*. London,. Edward Arnold.
- Weinreich, u. (1953), *Languages in Contact Publication of Linguistic*. Newyork. Circle of NewYork.
- Whitley W.H. (1974). *The Classification and Distribution of Kenya's African Languages*; katika Whitely W. H. (e.d) *Language in Kenya* . Nairobi Oxford university press.

## VIAMBATISHO

### KIAMBATISHO A

#### Hojaji

##### *Jibu maswali yote:*

Umri \_\_\_\_\_

Darasa \_\_\_\_\_

Shule \_\_\_\_\_

1. Lugha yako ya kwanza ni ipi?.....

2. Wazazi wako ni wa kabila gani?

Baba

.....

Mama

.....

3. Nyumbani , nyinyi hutumia lugha gani?

.....

4. Unaweza kuongea lugha gani nyingine?.....

.....

5. Wewe hutumia lugha gani shuleni ? .....

.....

## KIAMBATISE O B

### Hadithi za kusimulia

Toa hadithi fupi kuhusu:

- (a) Jinsi nilivyosherehekea sikukuu ya krisimasi mwaka jana.
- (b) Ajali mbaya niliyoshuhudia karibu na shule yetu
- (c) Ndoto ya ajabu

## KIAMBATISHO C

**Andika insha isiyozidi kurasa moja kuhusu:**

Ajali mbaya niliyoshuhudia karibu na shule yetu.



## KIAMBATISHO D

**Maneno ya kusomwa kwa sauti na kuandikwa (Imla)**

Soma maneno yafuatayo kwa sauti na kuandikwa (Imla)

1. Zusha	[ zuʃa ]	Shusha	[ ʃuʃa ]
2. Suka	[ su ka ]	Shuka	[ su ka ]
3. Fumba	[ fu mba ]	Vumba	[ vu mba ]
4. Zima	[ zi ma ]	Sima	[ si ma ]
5. Zuka	[ zu ka ]	Suka	[ su ka ]
6. Kivuli	[ kivu li ]	Kifuli	[ kifu li ]
7. Faa	[ fa a ]	Vaa	[ vaa ]
8. Ghali	[ ɣa li ]	Kali	[ ka li ]
9. Huzuni	[ huzu ni ]	Husuni	[ husu ni ]
10. Hizi	[ hi zi ]	Hisi	[ hi si ]
11. Kiza	[ ki za ]	Kisa	[ ki sa ]
12. Nzi	[ n zi ]	Insi	[ in si ]
13. Jivu	[ ji vu ]	Jifu	[ ji fu ]
14. Karambizi	[ kara mbizi ]	Karambisi	[ kara mbisi ]
15. Kazia	[ kazia ]	Kasia	[ kasi a ]
16. Kaza	[ ka za ]	Kasha	[ ka ʃ a ]
17. Mashaka shaka	[ ma ʃ aka ʃ a ka ]	Masakasaka	[ Masakasa ka ]
18. Mashizi	[ Ma ʃ i zi ]	Masizi	[ masi zi ]
19. Mazao	[ maza o ]	Masao	[ masa o ]

## KIAMBATISHO E

### Sentensi za kusomwa kwa sauti

*Soma sentensi zifuatazo kwa sauti:*

1. Mvuvi aliongozwa na yule mvulana kuvuka barabara
2. Mpangazi abebaye mizigo sharti awe na miraba mine
3. Tamthilia ni mchezo wa utunzi wa kisanaa ambao hueleza wazo fulani kwa matendo na mazungumzo.
4. Umepewa zawadi ya shilingi elfu kumi, utazitumiaje pesa hizo?
5. Akistushwa hujiingiza ndani ya gamba yake.
6. Mhandisi amenunua viti vipya lakini ameviweka katika vyumba vichafu.
7. Mchezo wa sarakasi ulituchekesha sana.
8. Alishusha mzigo uliokuwa juu ya baiskeli.
9. Tabia ya wizi hufungisha watu gerezani.
10. Gharama ya maisha imezusha hali ya wasiwasi hapa nchini.

## KIAMBATISHO F

Tangu kuumbwa kwa Adamu na Hawa, binadamu amejiendeleza kibinafsi kupitia kwa uzazi. Siku za zamani, binadamu alitakikana kupata watoto wengi kiasi alivyoweza. Nyakati hizo gharama ya maisha haikuwa juu. Mzazi aliweza kuwatunza watoto wake tangu wadogo hadi wakafikia utu uzima, kiasi cha kuoza au kuolewa na kushika mamlaka kama wazazi. Watoto wengi waliozaliwa nyakati hizo ni wachache waliwahi kufikia umri wa uzee. Vifo vilikuwa vikitokea mara nyingi sana. Maafa mengi yalitokana na ugonjwa. Pia kulikuwa na vita vya kikabila pamoja na vile vya kijamii. Na kwa sababu ya kuishi katika maskani yasiyo imara, wanyama wa mwitu mara nyingi waliwashambulia watoto na hata watu wazima.

KIAMBATISHO G

RAMANI YA SHULE TEULE KATIKA KATA YA GEM

